

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Sita – Tarehe 14 Juni, 2005**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA**

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa fungu la 15 la Sheria ya Tume ya kurekebisha Sheria, naomba kuwasilisha mezani katika Bunge lako Tukufu taarifa tano za Tume za Kurebisha Sheria Nchini. Taarifa hizo ambazo ziko katika lugha ya kiingereza ni kama ifuatavyo:-

- (1) Report on the Scheme for Provision of Legal Services by Paralegals.
- (2) Report on the Review of Legislation Relating to Corruption.
- (3) Report on the Flow of Justice in Tanzania.
- (4) Report on the Review of the Police and Prisons Legislation.
- (5) Report on the Introduction of Currency Points in Tanzania.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 51

**Madeni ya Wafanyakazi wa Mamlaka ya Mkonge Tanzania**

**MHE. JOEL N. BENDERA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipozungumza na na wawekezaji na viongozi wa Katani Ltd na wafanyakazi wa

Mamlaka ya Mkonge Tanzania katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe hapo mwaka 1997 aliahidi kulipa madeni yote yaishe, na kwa kuwa juhudini kubwa zimefanywa kupunguza deni hilo lakini bado kuna wafanyakazi wengi hawajalipwa hasa waliotoka katika mashamba ya *Ngombezi Estate*, *Rwengerwa Magunga Estate*, Mlemwa, Magoma, Hale na *Mruazi Estate* na majina ya wafanyakazi zaidi ya 100 yapo *PSRC* yakisubiri malipo yakiwemo mafao, nauli, *NPF* na kadhalika. Lakini hadi leo Serikali imeshindwa kulipa:-

(a) Kwa kuwa hiyo ilikuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais Je, lini wafanyakazi hao watalipwa hasa ukizingatia kuwa ahadi hiyo ni ya kipindi kirefu miaka 10 sasa.

(b) Je, Serikali inawaambia nini Wananchi hao ambao wamekata tamaa ya maisha?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joel Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliahidi kulipa madeni yote ya wafanyakazi wa Mamlaka ya Mkonge kwa awamu alipozungumza na wafanyakazi wa Mamlaka ya Mkonge mwaka 1997 katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa Mamlaka ya Mkonge katika vituo vya Makao Makuu, Dar es Salaam, Kibaranga *Sisal Estate*, Hale *Sisal Estate*, *Magoma Sisal Estate*, *Magunga Sisal Estate*, *Ngombezi Sisal Estate*, *Mwelya Sisal Estate*, *Kingolwira Sisal Estate*, *Kilosa/Myombo Sisal Estate*, *Monge Engineering Works Limited*, *Tanzania Carpet Company Limited*, *Tanzania Cordage Limited*, *Mruazi H.B.U*, Azimio/Kilapura, *Sisal Kamba - Mruazi*, *Mnazi Sisal Estate*, *Mkumbara Sisal Estate*, *Muheza/Kitisa Sisal Estate*, *Kange Dairy* na Msowero walilipwa mafao yao katika kipindi hiki. Baada ya malipo kufanyika chini ya usimamizi wa uongozi wa *Katani Limited* kulijitokeza malalamiko ya kupunjwa mafao kutoka mionganoni mwa wafanyakazi na matumizi yaliyokusudiwa kwa fedha zilizotolewa kulipia mafao hayo.

Katika hatua za awali za uchunguzi wa malalamiko hayo ilibainika kuwa uongozi wa *Katani Limited* ambao ulipewa dhamana ya kulipa mafao ya wafanyakazi ultumia shs. 700m ambazo ni sehemu ya fedha zilizotolewa kulipia gharama zote. Fedha hizo zimetumika nje ya matakwa yaliyokusudiwa. Hatua zinachukuliwa kuhakiki upungufu huo na pindi zitakapokamilika wale watakaobainika kupunjwa au kutolipwa watalipwa.

(b) Mheshimiwa Spika, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa madai katika mashirika ya umma ni mengi na kwamba Serikali ina nia thabiti ya kuwalipa wafanyakazi wote mafao wanayostahili kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizopo kwa wakati kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa kwamba zaidi ya milioni 700 zilitolewa kwa ajili ya kulipa wafanyakazi hao, lakini zikaenda kwenye mkondo mwingine kinyume cha utaratibu. Je, hao waliofanya utaratibu huo wa kuzipeleka fedha mahali ambapo sipo na kuzitumia kinyume na kuwatesa Wananchi hawa wanachukuliwa hatua gani na hela hizo wazirudishe haraka inavyowezekana?

La pili kwa kuwa hapa nilipo nina majina zaidi ya 100 akiwemo Mama Mwanahamisi, akiwepo Mohamed Mwinjori, Juma Mohamed, Said Abdallah na wengine. *List* ninayo hapa ambao wao kumbukumbu zao ni sahihi kabisa hazina matatizo. Je, ninaweza kumkabidhi Mheshimiwa Waziri akawalipa hawa? Kwa sababu nimechoka kuulizwa maswali kwenye Jimbo kuhusiana na masuala haya ya malipo. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi nimesema kwamba tunafuatilia uhakiki wa fedha ambazo hazikulipwa wale waliopaswa kulipa mafao hayo kutokana na Katani *Limited*. Kinachosemekana ni kwamba fedha hizi zilikuwa zipewe Tanzania *Sisal Board*, lakini wakati mafao haya yanatolewa Tanzania *Sisal Board* ilikuwa imevunjika na badala yake fedha hizi ikapewa Katani *Limited*. Katani *Limited* kwa sababu walikuwa wanaidai Tanzania *Sisal Board* wakaona wachukue shilingi milioni 700 kutokana na fedha zile. Sasa hili ni suala ambalo tunafuatilia kwa karibu kabisa. Niko tayari kuchukua majina hayo 100 kwa sababu tumekuwa tukishughulikia masuala haya pamoja na Mheshimiwa Joel Bendera na ninapenda kumuahidi kwamba tayari nimekwisha agiza *PCRC* Jumatatu ijayo waende Mkoa wa Tanga kufuatilia suala la hili kwa ukamilifu na baadaye waje wanipe majibu. (*Makofi*)

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa sababu tatizo hili linazidi kuigusa *Katani Limited*, na *Katani Limited* imepewa mashamba mengi hasa mashamba nane katika Mkao wa Tanga kwa nchi nzima na bado hawajatekeleza makubaliano ya mkataba, na leo wamekula na fedha za Watumishi. Hivi kuna tatizo gani la kuendelea kuwashifadhi hawa wasiondolewe kama *City Water?* (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, hadi sasa hivi tunavyozungumza hapa ni kwamba mashamba yote yaliyokuwa chini ya *Katani Limited* yamesharudishwa Serikalini, hawana mashamba sasa. (*Makofi*)

Tunachoangalia sasa ni jinsi gani tutaweza kuwasaidia wale wakulima wadogo wadogo wanaolima zao hili la katani pamoja na kuona ni utaratibu gani tutautumia ili

kuboresha zile mashine za kusindika katani ili tuzalishe mkonge kwa tija na kwa faida zaidi. (*Makofi*)

**MHE. ALHAJ SHaweji Abdallah:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa katika majibu yake ya msingi amesema wanazo kumbukumbu za watu waliokuwa wanaidai Mamlaka ya Mkonge. Naomba anieleze ni hatua zifi anachukua kwa mdai anayeitwa *Wincome Law* wa Kimamba Fibers anayedai Mamlaka ya Mkonge fedha kwa sababu alikuwa anatoa mafuta kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa shamba la Kimamba Fibers? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, taarifa aliyotoa ni husasan ni *specific*, kwa hiyo ningependa baada ya kipindi tukutane nijue jina la huyo mtu tuone tutafutiliae. Kwa sababu yako Mashirika mengi au yanadai Mamlaka za Mkonge au vile vile Mashirika mengi yanadaiwa na Mamlaka ya Mkonge, lakini hilo tatalifuatilia.

Na. 52

#### **Umaskini Uliokithiri kwa Wananchi wa Tanzania**

**MHE. SEMINDU K. PAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, inaelezwa kuwa wananchi vijijini ndio wanaishi katika ulingo wa umaskini uliokithiri kwa kuangalia vigezo vya kawaida tu kama mavazi, chakula, malazi, kiasi kwamba ukiita mukutano wa hadhara na ukitaka kujua ni watu wangapi wenye angalau Shs.1,000/- mfukoni utakuta ni watu wawili au watatu tu:-

- (a) Je, hali hii inatokana na nini wakati pato la kila Mtanzania tunaambiwa kuwa ni Shs.1,000/- kwa mwaka?
- (b) Je, kwa nini baadhi ya Watanzani wana fedha kupindukia wakati wengine hawana kitu kabisa – yaani wako mahututi wa kipato?
- (c) Kama ni mgao mbaya wa kipato, je, ni nani anayegawa mgao huo au ni ujanja wa kuwahi wa kupata na kuwaacha wengine hawana kitu; na kwamba Idara ya Kuondoa Umaskini kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais inashirikiana vipi na Wizara nyingine kama Wizara ya Fedha, Viwanda na Biashara, Ofisi ya Rais (Mipango na Ubinafsishaji), Kilimo na Chakula, Ushirika na Masoko pamoja na sekta nyingine katika kuinua hali ya maisha ya Mtanzania na kipato chake.

**SPIKA:** Sasa umesahisha nini, mbona ndivyo lilivyoandikwa. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali Na.3864 la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini-Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:

Serikali inatumia viashiria kadhaa kupima hali ya umaskini wa kipato na usio wa kipato hapa nchini. Baadhi ya viashiria vinavyotumika kupima umaskini wa kipato ni pamoa na asilimia ya watu walio chini ya ulingo wa umaskini kwa chakula na kwa mahitaji muhimu na pato la wastani la kila mtu. Kufuatana na savei ya mapato na matumizi ya kaya ya mwaka 2000/2001 asilimia 18.7 ya Watanzania iko chini ya ulingo wa umaskini kwa chakula na asilimia 35.7 chini ya ulingo wa umaskini kwa mahitaji muhimu. Aidha, savei inaonesha kwamba hali ya umaskini vijijini ni mbaya zaidi ukilinganisha na mjini na hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Asilimia 87 ya watu maskini wanaishi vijijini. Pia kuna tofauti za kipato kati ya kaya na jamii ya Watanzania kwa ujumla. Tofauti ya kipato inaongezeka zaidi mijini kwa kulinganisha savei ya mwaka 1991/1992 na ya 2000/01.

Kuhusu pato la wastani la kila mtu takwimu rasmi zinaonyesha kwamba pato la wastani la kila mtu kwa bei za mwaka 2003 lilikuwa Shs. 286,887/= au Shs. 57,370/= kwa bei za mwaka 1992 na limekuwa na ongezeko kila mwaka. Mwaka jana pato la wastani la kila mtu liliongezeka kwa asilimia 3.8 ukilinganisha na asilimia 4.0 mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa kama ifuatavyo: -

- (a) Kwanza, kufuatana na maelezo ya awali, pato la Mtanzania siyo Shs.1,000/= kwa mwaka. Pili, kuhusu umaskini kushamiri zaidi vijijini hali hii inatokana na ukuaji mdogo wa uchumi katika maeneo ya vijijini unaosababishwa na ongezeko dogo sana la uzalishaji wa bidhaa za kilimo, hali inayotokana na kutegemea mno hali ya hewa na teknolojia duni. Aidha, jitihada zaidi zimeelezwa katika kuimarisha masoko ambayo yanetetereka hasa baada ya Serikali kujitoa katika biashara.
- (b) Mheshimiwa Spika, kuhusu tofauti za kipato kwa baadhi ya Watanzania, napenda kutoa maelezo kuwa umaskini wa kipato unaondolewa kwa ongozeko la uzalishaji wa bidhaa na huduma. Aliye na uwezo wa kuzalisha zaidi na kuuza, kwa kawaida anapata kipato kikubwa zaidi. Mkulima atakayezingatia kilimo cha kisasa na kupata masoko bora, huyo lazima atapata mapato makubwa kuliko mtu ambaye hakufanya hivyo.

Aidha, kulingana na Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa 2000/2001, kipimo cha tofauti ya mapato katika jamii (*Gini Coefficient*) kimeongezeka kutoka 0.34 hadi 0.35. Watu wenye kipato cha juu ambao ni asilimia 20 ya idadi ya watu wote wanatumia jumla ya asilimia 44 ya matumizi yote ya kaya nchini, wakati wale maskini zaidi, yaani asilimia 20 ya watu wote, wao hutumia asilimia 7 tu ya matumizi nchini kote.

Ongezeko kubwa la tofauti ya matabaka lilikuwa zaidi katika maeneo ya mijini hususan Dar es Salaam.

(c) Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Semindu Pawa (Mbunge) kwamba hakuna anayegawa fedha na kuwafanya wengine wawe nazo tele wakati wengine wakikosa. Aidha, Idara ya Kuondo Umaskini kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, yenye dhamana ya kuratibu jitihada za Serikali za kupunguza umaskini, inashirikiana vizuri na Wizara za kisekta kuhakikisha kwamba maeneo yote ya kipaumbele katika masuala ya kundoa umaskini yanazingatiwa, Mkakati wa Taifa kwa Kupunguza Umaskini unatekelezwa, na maeneo yote ya vipaumbele katika kuondoa umaskini yanatengewa fedha kama ilivyokubalika ndani ya Serikali.

Jitihada za kuongeza kipato na hivyo kupunguza umaskini wa kipato ni za Wananchi wenyewe. Jukumu la Serikali ni kuweka mazingira bora ili Wananchi washiriki katika shughuli za kuleta maendeleo. Hivyo basi hakuna Wizara ya Serikali ama Halmashauri ya Serikali za Mitaa inayogawa fedha mikononi mwa watu moja kwa moja na kufanya watu wengine wawe nazo kwa wingi na wengine wakose kabisa.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais kuondoa umaskini, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

- (1) Katika vigezo vilivyotumika tulivyovizungumza katika jibu lake la msingi haoni kwamba moja inayopunguza fedha mifukoni ni kuchelewesha mafao ya watu ambao wanadai Mashirika kwa mfano wa *East African Community*, TES na Mashirika mengine kwa kuwacheleshea mafao yao kwa miaka 20 au 10 ni moja inayopunguza mifukoni pesa zao?
- (2) Kupunguza umaskini vijijini hii asilimia 18 najua ni Kata ya Mkulanzi, Kata ya Tegetero na Kata ya Ngerere, ndiko huko ambako umaskini ulikithiri kwa sababu wanakopwa mazao yao hakuna soko lilitokuwa na uhakika. Je, hiyo ni moja ya sababu ambayo inachukua fedha za Wananchi na kutoa mgao mbaya? Kwa sababu hawajui kama kila mtu anapata 286,000 kwa mwaka. Kwa hiyo, fedha hii inakwenda kwa wajanja wengine kutokana na ulangizi wa mazao yao kwa bei ya chini kutokuwa na soko la uhakika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, ningependa kumjibu Mheshimiwa Semindu Pawa maswali yake ya nyongeza mawili kama ifuatavyo:-

- (1) Kwa kiasi fulani nakubaliana kwamba kama mafao ya wastaifu yanacheleshwa kwa sababu yoyote ile, kwa vyovyote mhusika atakuwa ameathirika kutokana na kipato chake. Lakini hata hivyo natumaini Mheshimiwa Semindu Pawa amekwishafarijika na maelezo yaliyotolewa na Waziri wa Fedha kuhusiana na malipo yatakayofanywa kwa wale wastaifu wa Afrika Mashiriki. Vile vile hapa

sasa hivi tumemsikia Mheshimiwa Waziri wa Mipango ambapo tumelezwu jinsi wanavyofuatiliwa mafao ya watu mbalimbali, na vile vile zoezi sasa hivi linaendelea la kuhakikisha wale wastaa fu amba walilipwa kwa mkupuo wanarudia katika orodha ya kulipwa mafao yao. Kwa hiyo, Serikali inachukua hatua ya kupunguza umaskini huo kwa upande huo. (*Makofi*)

(2) Kukopwa kwa wakulima mazao yao na vile vile kukosa kwa soko la uhakika kunaweza pia kuathiri mapato au juhudhi za kuondoa umaskini wa kipato. Lakini ningependa vile vile nitoe mwito kwa Mheshimiwa Semindu Pawa na Wabunge wenzangu kwamba kwa kushirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko, na vile vile kutumia utawala Wilayani kwetu tuweke mikakati ya kufuatalia ununuzi wa mazao hatua kwa hatua ili Wananchi wasiweze kupunjwa. Mara nyingi wanunuzi wa mazao wakishaenda kununua vijijini utakuta hakuna anayewafuatalia kwa ukaribu ili kuhakikisha kwamba hawakopwi na vile vile hawapunjwi kwa kuza mazao hayo chini ya bei ambayo inakubalika katika masoko ya hapa ndani na hata ukilinganisha na masoko yale ya nje. Kwa hiyo, tuwasaidie wakulima kuondokana na tatizo hilo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, suala la kuondoa umaskini ni pana tutapata nafasi kulijadili wakati wa kujadili hoja ya Waziri mhusika. Kwa sasa hivi tuendelee na maswali mengine.

Na. 53

### **Ukataji Holela wa Miti**

**MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN** aliuliza:-

Kwa kuwa suala zima la hifadhi ya mazingira ni pamoja na uhifadhi wa misitu na kwa kuwa ukataji holela wa miti kwa ajili ya uchomaji mkaa, hasa mjini ni moja ya sababu kubwa ya uharibifu wa mazingira:-

- Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kudhibiti ukataji ovyo wa miti ili kunusuru mazingira yetu?
- Endapo sababu kubwa ya ukataji holela wa misitu ni kwa ajili ya nishati ya kutumia majumbani. Je ni lini Serikali itatimiza matumizi ya nishati mbadala kama vile umeme, gesi asilia, makaa yam awe na kadhalika ili tuachane na matumizi ya mkaa na kuni na hivyo kuinusuru misitu yetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nitakosa fadhila nisipokushukuru kwa kuniokoa na Tsunami ya maswali ya nyongeza. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, Mbunge wa Ngorongoro, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mathew Ole-Timan kwamba suala la ukataji miti ovyo linachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira, na kwamba mahitaji ya nishati ni chanzo kikubwa cha ukataji miti. Hii ni kwa sababu zaidi ya asilimia 90 ya nishati inayotumika nchini, inatokana na miti. Hata hivyo, zipo sababu nyingine zinazosababisha uharibifu wa mazingira kama vile ukataji miti kwa shughuli za kilimo na makazi, mbao, na uchomaji hovyo wa misitu na vichaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kudhibiti ukataji miti hovyo:-

- (1) Ili kudhibiti utoaji holela wa leseni za uvunaji katika misitu ya asili. Kamati za wilaya za utoaji leseni zimeundwa. Kamati hizi zina jukumu la kudhibiti uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002. Wajumbe wa Kamati ni:
  - (i) Afisa Tawala wa wilaya – Mwenyekiti;
  - (ii) Mkuu wa upelelezi wa Wilaya;
  - (iii) Mwakilishi wa Idara ya Maji;
  - (iv) Maafisa watendaji wa vijiji vinavyopatikana katika maeneo ya msitu husika;
  - (v) Afisa maliasili wa wilaya;
  - (vi) Afisa Misitu wa wilaya – Katibu.
- (2) Kikosi maalum cha doria cha kudhibiti uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu ambacho kinafanya kazi saa 24 kimeanzishwa chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii.
- (3) Kuhimiza ushirikishwaji wa wananchi katika utunzaji wa misitu na mazingira. Wananchi wanahimizwa kutenga maeneo yao yenye misitu ya asili na kuyahifadhi kwa manufaa yao. Pia, wananchi wanashirikishwa katika kuitunza na kuiendeleva misitu ya hifadhi ya Serikali kwa njia shirkishi.
- (4) Serikali inaendelea kuhimiza utelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji wa miti na Wananchi wanahimizwa kupanda miti na kuitunza, kama njia mojawapo ya kupunguza ukataji hovyo wa miti ya asili.
- (5) Elimu ya matumizi endelevu ya mazao ya misitu na utunzaji wa mazingira inatolewa kwa wananchi kwa njia mbalimbali kama vile mafunzo kwa vitendo, mikutano na wadau, majarida, vipeperushi, redio na televisheni.

Serikali inaendeleza na kuhimiza matumizi ya teknolojia ya vyanzo mbadala vya nishati kama vile makaa ya mawe, bayogesi, tungamoto nyingine (*other biomass*), matumizi ya mafuta ya mmea uitwao Jetropha matumizi ya pumba za mbao (*sawdust*) na mpunga, nishati ya maporomoko ya maji, nishati ya jua (*solar energy*) na nishati itokanayo na upepo. Aidha Serikali inaendeleza kuhamasisha matumizi fanisi ya nishati (*energy efficiency and conservation*), kama vile:-

1. Uendelezaji majiko sanifu ya mkaa na kuni.
2. Uendelezaji teknolojia bora za uchomaji mkaa hasa kwa mikoa ya Pwani, Tanga, Iringa na Kilimanjaro.
3. Uendeshaji wa makaushio ya mazao yatumiayo nishati ya jua (*solar crop driers*).
4. Uendeshaji matumizi ya masalio ya mazao ya misitu kwa kutengeneza vitofali (*briquettes*).
5. Uzalishaji umeme kwa kutumia mionzi ya jua, maporomoko ya maji, mabanzi ya miti na masalio ya miwa katika viwanda vya sukari.
6. Kufanya utafiti wa vyanzo vingine vya nishati kama vile jotoardhi (*geothermal*).
7. Kutafiti teknolojia bora katika kutumia makaa ya mawe kwa kupikia na matumizi viwandani.
8. Kuhamasisha matumizi ya gesi ya mafuta (*liquefied petroleum Gas*) pamoja na gesi asilia.

**MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumepata fedha nyingi bila kutarajia kutokana na kusamehewa madeni. Je, sehemu ya fedha hiyo inaweza kutumika kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza nishati mbadala ili tuweze kunusuru misitu yetu?

Je, ni lini Serikali itaweka mpango wa kupunguza bei ya umeme, ili umeme huo utumike majumbani zaidi kuliko kuendelea na ukataji holela wa miti? Ahsante (*Makofî*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi natumia nafasi hii katika kumjibu Mheshimiwa Mathew Ole-Timan maswali yake ya nyongeza mawili kumpongeza Mheshimiwa Rais William Benjamin Mkapa kwa kufanikisha Tanzania kusamehewa madeni yake. (*Makofî*)

Sasa akisema kwamba fedha zitakazokuwa zimetolewa au zimetokana na kupunguzwa madeni zitumike katika suala zima la kutafuta nishati mbadala, natumaini

sisi wote tunaelewa kwamba madhumuni ya kusamehewa madeni ni kuiwezesha Serikali yetu kutumia fedha ambazo zingelipa madeni katika Taasisi mbalimbali za kifedha za Kimataifa kuelekeza kwa maendeleo ya jamii na miradi mbalimbali nchini.

Kwa hiyo, bila shaka Bunge na Serikali kwa ujumla zitatafakari namna ya kuboresha zaidi huduma hizo kwa kutumia fedha hizo.

Suala hilo litafanyiwa kazi haliwezi likajibowi hapa sasa hivi, tumesamehewa jana halafu tunatumbukia tumbukia kwenye matumizi yake. Litafanyiwa kazi na muafaka utapatiwana wa matumizi bora zaidi ya fedha hizo.

La pili kuhusiana na kwamba sasa kwa nini basi bei za umeme zisipunguzwe. Natumaini Waziri muhusika atakapofika kuja kutoa hotuba yake atapata nafasi kufafanua mikakati yake na Serikali kwa ujumla ya kuendelea kuupunguza bei za umeme nchini ili ziweze kusaidia kuondokana na matatizo haya ya kuchafua au kukata miti kwa ajili ya nishati.

Na. 54

### **Mradi wa Maendeleo wa Ukanda wa Mtwara**

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mradi wa Maendeleo wa Ukanda wa Mtwara (*MTDC*) uliobuniwa na nchi nne za *SADC* ulikubalika vizuri na Serikali ikawekeana saini na wawekezaji hapo Julai mwaka 2002 lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika:-

- (a) Je, Serikali inaweza kutoa tamko juu ya mradi huo?
- (b) Je, Wizara iliyopewa jukumu ka kusimamia utekelezaji wa mradi huo inasaidiwa vipi na Wizara nyingine husika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Simon M. Mbilinyi, Mbunge wa Peramiho, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali za Msumbiji, Malawi na Zambia, inashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali chini ya Mradi wa Maendeleo wa Ukanda wa Mtwara ambapo tarehe 15 Desemba, 2004, Wakuu wa nchi wanachama walikutana mjini Lilongwe nchini Malawi na kusaini Mkataba wa Makubaliano wa kuanzisha Mradi wa Maendeleo wa Ukanda wa Mtwara. Kusainiwa kwa Mkataba huo, kumefanya mradi huu sasa utambuliwe kisheria na nchi zote nne.

Mheshimiwa Spika, miradi mbalimbali imebuniwa chini ya Ukanda wa Maendeleo ya Mtwara, ikiwemo miradi ifuatayo:-

- (i) Ujenzi wa daraja la Umoja (*Unity Bridge*) ambalo litaunganisha Tanzania na Msumbiji kupitia Mto Ruvuma. Mradi huu unakadirwa kugharimu kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 33. Wakuu wa nchi hizi mbili wamesaini makubaliano ya kushirikiana katika kutekeleza ujenzi wa daraja hilo kutafuta fedha za wahisani au hata kutumia rasilimali zetu wenyewe. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Serikali zote mbili zimekubaliana kutenga katika bajeti zao kiasi cha shilingi bilioni 4.5 kwa kila nchi. Mkataba wa Usanifu umetiwa saini tarehe 02 Juni, 2005 Mjini Dar es Salaam. Usanifu unategemewa kukamilika katika kipindi cha miezi mitatu ambapo kazi ya ujenzi wa daraja hilo utanza na tunategemea utanza kati ya mwezi September na October mwaka huu.
- (ii) Ujenzi wa barabara ya Mtwara hadi *Mbamba Bay*. Barabara hii yenye urefu wa km 833 itaunganisha Tanzania na Msumbiji kupitia Daraja la Umoja na Malawi kupitia *Mbamba Bay*. Kiasi cha Dola za Kimarekani milioni moja zilipatikana kutoka mfuko wa Kuwait. Fedha hizo zimetumika kufanya upembuzi yakinifu na kazi hiyo imekamilika tangu Aprili 2004. Upembuzi huo ulionyesha kuwa mradi huu unafaa kutekelezwa kwa kiwango cha lami. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, jumla ya shilingi bilioni 5.1 zimetengwa kwa ajili ya kutayarisha usanifu na nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Masasi – Songea – *Mbamba Bay* kwa kiwango cha lami. Kati ya fedha hizo, bilioni 4.1 ni za ndani na bilioni 1.0 ni za nje.
- (iii) Mradi wa Uzalishaji Umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma. Serikali ilitiliana Mkataba wa Nia (*Agreement of Intent*) na Wawekezaji wa mradi huu mnamo tarehe 02 Julai, 2001 Mjini Dodoma. Mradi huu utagharamiwa na kuendeshwa na sekta binafsi na unategemewa kuzalisha *Megawatt 400* za umeme. wawekezaji wa mradi huu ni makampuni ya *SIEMEN Ltd, GRINAKER – LTA Limited* na Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*). Gharama za kuendeleza mradi huu inakisiwa kuwa Dola za Kimarekani milioni 612.

Kimsingi, Serikali imekwishakubali utekelezaji wa Mradi huu na ilitoa agizo kupitia Wizara ya Nishati na Madini ili iweze kuwasiliana na wawekezaji wa mradi na kutoa kibali kwa waendelezaji wa mradi waruhusiwe kutafuta soko la umeme nchi jirani na kwa wateja wakubwa nchini. Mazungumzo yanaendelea kati ya wawekezaji wa mradi na taasisi za nishati nchini Kenya na Uganda na watumiaji wa jumla kuhusu mahitaji yao ya umeme. Miradi mingine iliyobuniwa kupita mradi huu ni kuendeleza utalii, ujenzi na ukarabati wa bandari za Mtwara, Manda, *Mbamba Bay*, Lindi na Kilwa, ujenzi wa barabara kutoka Mchuchuma hadi Mlimba na uchimbaji wa chuma cha Liganga.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania, Wizara ya Ujenzi ndiyo Mratibu Mkuu wa miradi ya Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara na Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) limepewa jukumu la kusimamia, kuendeleza na kutafuta wawekezaji wa miradi mbalimbali katika Ukanda huu. Wizara zingine zinazoshirikishwa katika utekelezaji wa miradi ya Ukanda huu ni pamoja na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafishajji. Vilevile Wakuu wa Mikoa ya Mtwara, Lindi, Iringa, Pwani, Ruvuma, Mbeya na Morogoro pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa hiyo wanashirikishwa kikalimifu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa kumekuwa na ushirikiano wa kutosha baina yetu wote na Serikali inaendeleza mradi huu kwa nguvu zake zote kama nilivyoeleza awali katika kipengele (a). Pamoja na hiyo, napenda kumshukuru Profesa Mbilinyi kwa jinsi anavyofuatalia suala la *Mtwara Corridor* na maendeleo yake.

**SPIKA:** Waheshimiwa saba wa *Mtwara Corridor* wanataka kuuliza maswali lakini muda hauruhusu na leo majibu yamekuwa marefu kuliko kiasi. Kwa hiyo, mnisamehe nitampa nafasi muuliza swali la msingi peke yake. Mheshimiwa Profesa Saimon Mbilinyi, swali la nyongeza?

**MHE. PROF. SAIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa mradi huu unatekelezwa kwa niaba ya Serikali na Shirika letu kubwa la *NDC*, kuna tatizo kuwa mara nyingi Wizara zinazohusika na sekta au *activity* fulani zinapenda kuingilia kazi hiyo ya *NDC*. *NDC* ikifanya kitu mpaka mahali fulani Wizara inayohusika inasema hiyo ni kazi yetu sisi. Sasa sijui kama kiongozi upande wa Wizara anali-*coordinate* viyi suala hili la kila Wizara kudai kuwa huu ni mradi wa Wizara yao, huu ni mradi wa Wizara yao badala ya kuliachia shirika hilo liendelee na kazi yake kikamilifu? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tumepata tatizo hilo. *NDC* wamewasiliana na sisi na baada ya kutafakari vyta kutosha tumewaomba *NDC* kila wanapokwama wawasiliane na Wizara ambayo ndio mratibu mkuu ili Wizara iwasiliane na Wizara inayosema mradi huo ni wao kwa sababu miradi yote ni ya Taifa kwa yejote atakayetekelza miradi hii kwa uhakika ni kwa faida ya Taifa.

Na. 55

#### **Sheria ya Ndoa Inavyomtambua Mtoto**

**MHE. HAROUB S. MASOUD (k.n.y. MHE. PONSIANO D. NYAMI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inamtambua mtoto wa kike wa miaka 14 kuwa ni mtu mzima anayefaa kuolewa na kumhudumia mume, lakini wakati huo huo Sheria ya Makosa ya Kujamiihana ya mwaka 1998 inasema kumwingilia msichana aliye chini ya umri wa miaka 18 ni kosa la jinai na la ubakaji hata kama ameridhia mwenyewe; na sheria zote hizi zimetungwa na Serikali hiyo hiyo ambayo inamkataa msichana wa chini ya miaka 18 kuwa ni mtoto:-

- (a) Je, huko si kujikanyaga kwa Serikali na kuhalalisha watoto kati ya miaka 14 na 17 wabakwe?
- (b) Je, Sheria hizi zitaendelea kukinzana kama ilivyo au ni ipi itafutwa kati ya hizo?

#### **WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA alijibu:**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inaruhusu binti mwenye umri wa kati ya miaka 14 na 17 kuolewa. Kwa kutambua kuwa binti mwenye umri huo bado hajawa na uwezo wa kutosha kupambanua na mambo, Sheria hiyo imeweka vigezo vya kumlinda. Vigezo hivi ni kwamba kama umri wake ni kati ya miaka 15 na 17, lazima binti huyo apate ridhaa (*consent*) ya wazazi au mlezi kabla ya kuolewa na yule wa miaka 14 lazima apate kibali cha Mahakama.

Mheshimiwa Spika, sheria yoyote inatokana na matakwa ya jamii. Sheria yetu ya Ndoa inazingatia mila na dini mbalimbali zilizopo nchini ambazo zinatambua umri tofauti wa binti kuolewa. Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inatokana na matakwa ya jamii ya Kitanzania. Kama jamii imebadilika sasa, basi itakuwa ni muda muafaka kuangalia upya umri huu na Tume ya Kurekebisha Sheria imekwishaanza kulifanyia kazi suala hili.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Makosa ya Kujamiihana ya mwaka 1998 inaeleza kuwa kumwingilia msichana aliye chini ya umri wa miaka 18 kama si mke wako linakuwa ni kosa la jinai la ubakaji hata kama ameridhi mwenyewe. Hii ni kwa sababu inachukuliwa kwamba msichana mwenye umri huo hana uwezo wa kutoa ridhaa hiyo kwa hiari.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia niliyoyaeleza, sheria hizi mbili hazikwaruzani wala kugongana kwani hakuna kitendo kinachokuwa halali chini ya sheria moja lakini kinakuwa haramu katika sheria nyingine. Sheria hizi zingekwaruzana pale tu sheria ya Makosa ya Kujamiihana ingefanywa kuwa tendo la kubaka endapo mume wa binti mwenye umri wa kati ya miaka 14 na 17 angeshtakiwa kosa la kubaka eti kwa sababu amefanya tendo la ndoa na mke wake huyo. Lakini kwa jinsi sheria ilivyo leo, ruksa! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kufutwa kwa sheria yoyote hutegemea kuisha kwa umuhimu wake. Tafiti lazima zifanyike katika jamii kuona kama sheria bado ina umuhimu ua la. Kwa sababu hakuna tafiti zinazoonyesha kuwa sheria zote mbili ama zote au sehemu yake zimekwisha umuhimu wake. Hivyo zote zitaendelea kuwepo mpaka hapa itakapotokea umuhimu wa kuzifuta zote au mojawapo.

**MHE. HAROUB S. MASOUD:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

- (a) Kwa kuwa haki ya mtoto ni pamoja na ulinzi wa afya yake na kwa vile kwa mujibu wa utafiti wa Madaktari ulimwenguni kote umeonyesha dhahiri kwamba mtoto wa kike anakuwa tayari kwa kitendo cha ndoa anapotimiza miaka 20. Sasa, je, Mheshimiwa Waziri sheria hiyo anakiuka haki za kumlinda mtoto? (*Makofi*)
- (b) Kwa kuwa kwa mujibu wa sheria zote mbili hizo, mtoto mdogo ambaye hajafikisha miaka 18 anaruhusiwa kuolewa kwa idhini ya wazee wake au walezi wake lakini mtoto huyo huyo inakuwa kimefanywa kitendo cha ubakaji kama ameingiliwa bila ridhaa za hao niliowataja sasa je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba hii sheria bado inataka marekebisho hasa katika tendo la ubakaji kwa vile bado Serikali ina kigeugeu kwa watu wa aina hiyo kupata hukumu ya adhabu ya kifo? (*Kicheko/Makofi*)

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza suala la kusema mtoto ni nani, ni suala ambalo sasa hivi Serikali inalitazama. Kwa nchi nyingi mtoto ni yule ambaye yuko chini ya miaka 18 na katika nchi nyingine inakwenda mpaka miaka 21. Kwa hiyo, suala hili bado tunalifanyia utafiti kuweza kupata muafaka katika nchi yetu kwa sababu *definition* ya mtoto katika sheria mbalimbali zinatofautiana. Kwa hiyo tunachotafuta hapa ni kupata *definition* mtoto ni miaka mingapi lakini ilivyo kwa sasa hivi pamoja na hayo, lazima tutizame mambo haya.

Mheshimiwa Spika, nani ni mtoto aruhusiwe kuolewa, hili linaendana na mila zetu kama nilivyojibu katika swali langu la msingi na pia katika dini ya Kiislam mtoto anapofikisha miaka 18 basi anakuwa tayari kuolewa. Kwa hiyo, tuna mambo haya mengi ambayo inabidi tuyatizame sio kuchukulia tu kwamba hii ni haki za binadamu kwa upande wa dunia basi na sisi tukaweza kuzi-copy katika sheria zetu.

Swali la pili, nadhani hili nimekwishalijibu katika swali langu la msingi na katika hili jibu la swali la nyongeza.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunazingatia muda sio kwamba nawaonea, swali linalofuata Mheshimiwa Khalid Suru.

Na. 56

#### **Utoaji wa Vyeti vya Kuzaliwa**

### **MHE. KHALID S. SURU aliuliza:-**

Kwa kuwa, Ofisi za Makatibu Tarafa na zile za Maafisa Watendaji wa Kata nchini kote haziruhusiwi kuandika na kutoa vyeti nya kuzaliwa kwa watoto na watu wazima ambao hawana vyeti hivyo:-

- (a) Je, ni sababu gani zinazozua ofisi hizo zisiruhusiwe kushughulikia utoaji wa vyeti hivyo kwa hao niliowataja?
- (b) Kwa kuwa, Makao Makuu ya Wilaya mara nyingi yapo mbali sana na Tarafa, Kata, Vijiji na Mitaa kiasi kwamba sio rahisi wananchi maskini na wanyonge kufuatilia vyeti vyao Wilayani. Je, Serikali haioni kwamba, hali hiyo inawapa wananchi wake kero na bughudha kubwa?
- (c) Je, sasa Serikali inachukua hatua gani kuondoa kero hiyo?

### **WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalid Suru, Mbunge wa Kondo Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, suala la kuandikisha na kutoa vyeti nya kuzaliwa linasimamiwa na Sheria ya Uandikishaji Vizazi na Vifo (Sura 108) ya Sheria za nchi. Sheria hii inaweka bayana kuwa Msajili wa Vizazi na Vifo katika Wilaya ni Katibu Tawala wa Wilaya au Afisa aliyeteuliwa na Msajili Mkuu wa Vizazi na Vifo. Msajili wa Wilaya ndiye mwenye mamlaka ya kutoa vyeti nya vizazi na vifo katika Wilaya husika.

Hata tungerekebisha Sheria ya Uandikishaji Vizazi na Vifo kuruhusu Makatibu Tarafa na Watendaji wa Kata kuwa Wasajili wa Vizazi na Vifo, vyeti nya kizazi na kifo ni nyaraka nyeti kiasi kwamba kwa kuzingatia kuwa ofisi zetu nyingi a Tarafa na Kata hazina ulinzi wa kutosha kama ilivyo Makao Makuu ya Wilaya, itakuwa vigumu kuhakikisha usalama wa vyeti hivi.

- (b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa Makao Makuu ya Wilaya yako mbali na hivyo wananchi wanaweza kupata shida wakati wa kufuatilia vyeti nya kuzaliwa au vifo na ndio maana imesogezza huduma za kuandikisha vizazi karibu zaidi na wananchi.

Tofauti na ilivyokuwa zamani, sasa kizazi au kifo kinaandikishwa pale kilipotokea yaani hospitalini, zahanati, au kwa Mtendaji wa Kijiji au Kitongoji kwa kifo au kizazi kilichotokea nyumbani. Katika mazingira hayo, mhusika atakwenda Wilayani kufuata cheti

tu na si kuandikisha, isipokuwa kwa wanaoandikishwa wakiwa wakubwa yaani kizazi kinachoandikishwa zaidi ya siku 90 na kifo siku 30 tangu kitokee.

- (c) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa siku zote ikifanya jitihada za kuwaondolea kero wananchi wake kwa kuwasogezea huduma. Karibuni, Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu, ambayo ndiye mwenye kusimamia Sheria ya Uandikishaji Vizazi na Vifo, inatarajia kuanzisha huduma za magari (*mobile services*) ili huduma hiyo iwe karibu na wananchi waliko, kulingana na uwezo wa kifedha utakavyokuwa.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

- (a) Kwa kuwa nchi yetu ina watu matajiri sana, wengine wana uwezo wa kawaida na wengine maskini, sasa hawa maskini watasaidiwaje ili kuweza kukomboa vyeti vya watoto wao ambavyo vimekwama kwenye Ofisi za Vizazi na Vifo kwa sababu hawana pesa za kukomboa vyeti hivyo? (*Makofi*)
- (b) Kwa kuwa vyeti vya kuzaliwa ni muhimu sana kwa watoto na watu wazima, hivi Serikali inaona hasara gani hasa kufuta kabisa ada hii ili vyeti hivyo vitolewe bure? (*Makofi*)

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, gharama ya kusajili vizazi kwa kweli si kubwa sana. Usajili ni Sh.2,000 na cheti ni Sh.1,500 ni jumla ya Sh.3,500. Nasema kwa kweli hakuna umaskini wa kiasi hicho hapa Tanzania kwa mtu kutomudu gharama hii.

**WABUNGE FULANI:** Wanazaa kila mwaka.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Hata kama unazaa kila mwaka, mwaka mzima huna Sh.3,500 basi uache hata hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la kufuta ada ya vyeti hivi ni kusema kwamba hata mahari nazo tuzifute maana kama unaweza kumudu mahari kwa nini ushindwe kumudu matunzo ya mtoto wako? (*Kicheko*)

Na. 57

#### **Ukaguzi wa Madereva Baada ya Mafunzo**

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa, ili kuhakikisha usalama barabarani ni lazima madereva wawe na leseni baada ya kufuzu mafunzo ya udereva na kuditishwa na wakaguzi kabla ya kupatiwa leseni; na kwa kuwa, jambo hilo linakamilika tu baada ya mtu anayepimwa kwenda Polisi akiwa na vyeti alivyopewa kutoka Chuo cha Usafirishaji, Shule ya Udereva (*Driving School*) na kufanyiwa majaribio:-

- (a) Je, ni madereva wangapi wamefanyiwa majaribio (*test*) na kuonekana hawajafuzu na hivyo kukosa sifa ya kupatiwa leseni katika kipindi cha mwaka 2002/2003 na 2003/2004?
- (b) Je, ni kweli kwamba, katika vyuo vingi vya *Traffic* hakuna magari ya kufanya majaribio?
- (c) Kama jibu katika sehemu (b) ya swali hili ni “ndiyo”. Je, ni vipi Serikali itatuhakikishia kuwa wale wote waliopata majaribio hayo na hatimaye kupewa leseni, wamefaulu kwa sifa za kupewa leseni?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda (Viti Maalum) lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani Na.30 ya mwaka 1973 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Usalama Barabarani Na.16 ya mwaka 1996, kila mwombaji wa leseni ya udereva anatakiwa apate mafunzo katika shule ya udereva iliyosajiliwa na wakufunzi nao wawe wamesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Shule za Udereva Na.14 ya mwaka 1965. Waombaji pia wanatakiwa wafanyiwe majaribio na Polisi wa *Traffic* kabla ya kupata leseni.  
  
Katika kipindi cha mwaka 2002/2003, waombaji wa leseni waliofanyiwa majaribio na Polisi ni 25,115, kati yao waliofaulu ni 17,949 na walioshindwa na kwa hiyo hawakupata leseni ni 7,166. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004 waombaji waliofanyiwa majaribio ni 36,572, waliofaulu na kupata leseni ni 22,665 na walioshindwa na kwa hiyo hawakupata leseni ni 13,907.
- (b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kwa sasa katika vituo vingi vya Polisi (*Traffic*) hakuna magari ya majaribio kwa madereva na kwa sababu hiyo shule za udereva zinapopeleka wanafunzi wao Polisi kwa majaribio, hutakiwa kwenda na magari yao kwa ajili ya majaribio hayo. Shule ya udereva hutakiwa kwa mujibu wa sheria iwe na magari ya mafunzo na hili ni moja ya masharti ya kusajiliwa kwa shule hizo.

(c) Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa katika vituo vya Polisi hakuna magari ya majoribio, Serikali inahakikisha kuwa wale wote waliofaulu majoribio hayo na hatimaye kupewa leseni, wanazo sifa za kupewa leseni kutokana na ukweli kwamba kila shule ya udereva inawajibika kupeleka Polisi wanafunzi wao kujaribiwa wakiwa na magari yanayolingana na mafunzo waliyoyatoa kwa wanafunzi hao na pia kulingana na daraja la leseni wanayohitaji watahiniwa hao Aidha, majoribio katika vituo vya Polisi huendeshwa na wakaguzi (*vehicle inspectors*) wawili ambao lazima wawe wamefuzu rasmi na kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Kwa hiyo, waombaji wa leseni za udereva wanaofaulu majoribio haya na kupewa leseni kwa kweli wanazo sifa za kupewa leseni hakuna kubahatisha wala kubabaisha.

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Kwa kuwa zamani kulikuwa na utaratibu mzuri wa kufanya majoribio kwa madereva wapya kwa kutumia magari makubwa ambayo yalikuwa yanafanyika pale pale kwenye kituo cha Polisi na kutokana na hali hiyo madereva wengi walikuwa wanapatikana wakiwa wazuri kutokana lakini hali ilivyo sasa madereva wengi wanajaribiwa kwa magari madogo kiasi ambacho wakipewa magari makubwa kama mabasi wanashindwa kufanya kazi. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kurudisha utaratibu wa zamani wa kutoa magari makubwa kwa ajili ya majoribio kwa madereva wapya ili wasisababishe ajali?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba majoribio haya yanafanywa kulingana na aina ya leseni ya mtahiniwa anayotaka na vile vile aina ya magari ambayo amefundishwa.

Kwa hiyo, kama mtahiniwa anataka leseni *class ‘C’* aendeshe mabasi atatahiniwa kwa kuendesha mabasi na kama mtahiniwa anafanya majoribio kwa leseni la daraja “D” kuendesha magari madogo madogo basi atatahiniwa kwa yale magari madogo anayoendesha hatatahiniwa kwa malori wala mabasi.

Na. 58

#### **Chakula cha Mahabusu**

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD (K.n.y. MHE. RAMADHAN N. PANDU)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya Askari wana tabia ya kuwanyima/kutowapa chakula watuhumiwa wanapokuwa mahabusu/rumande katika Vituo vya Polisi na hasa chakula hicho kinapotoka kwa familia zao na kusababisha mahabusu hao kulala na njaa:-

- (a) Katika utawala bora wa sheria na kwa mujibu wa kanuni, sheria na taratibu za Jeshi la Polisi; je, mahabusu kama binadamu ana haki gani anazostahili kupata na ni zifi asizostahili kupata anapokuwa chini ya ulinzi wa Polisi mahabusu?
- (b) Iwapo kitendo cha kutompa chakula mahabusu ni kosa; je, mahabusu huyo atakuwa na haki gani dhidi ya kosa hilo?
- (c) Je, ni hatua gani za kinidhamu zinazopaswa kuchukuliwa na Jeshi la Polisi kwa Askari aliyehusika na kosa hilo?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge Ramadhani N. Pandu, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria na kanuni za Jeshi la Polisi (*PGO No.353*) mahabusu kama binadamu ana haki zifuatazo anazostahili kupata anapouwa rumande chini ya ulinzi wa Polisi:-

- (i) Kupelekwa hospitali haraka kama akiugua.
- (ii) Kupewa blanketi la kujifunika katika sehemu za baridi kali.
- (iii) Kupewa chakula kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa.
- (iv) Kusikilizwa na kuonana na Wakuu wa Kituo endapo ana shida au malalamiko.
- (v) Kutokuteswa anapokuwa mahabusu.
- (vi) Kuletewa chakula na ndugu zake au jamaa zake.
- (vii) Kuruhusiwa kushauriana na Mawakili wake.

Mheshimiwa Spika, aidha haki zifuatazo hastahili kupata akiwa mahabusu:-

- (i) Haruhusiwi kuvuta sigara au kunywa pombe wala kuendesha burudani na starehe zozote akiwa ndani ya mahabusu.

- (ii) Haruhuswi kufanya kitendo kingine chochote kinyume cha sheria kama kupigana na mahabusu wengine au kujaribu kumpiga Askari au kuhanribu mali kama kuvunja mlango, ukuta, paa la jengo la mahabusu na kadhalika.
- (b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kitendo cha kutompa mahabusu chakula ni kosa kisheria na kwa mujibu wa kanuni za Polisi (*PGO*) Na. 353 kifungu kidogo cha 25. Mahabusu anapofanyiwa hivyo, anayo haki ya kufikisha malalamiko yake kwa uongozi wa juu wa Polisi, kwa Wakili wake au Mahakamani.
- (c) Mheshimiwa Spika, iwapo tuhuma zitatolewa dhidi ya Askari kuhusu kumnyima chakula mahabusu hatua za kinidhamu zitachukuliwa mara moja dhidi ya Polisi anayetuhumiwa kwa kufunguliwa mashtaka katika Mahakama ya Kijeshi kwa mujibu wa kanuni za Jeshi la Polisi (*PGO*) Na.106 kifungu cha 47. Iwapo Askari huyo atapatikana na hatia, ataadhibiwa kwa mujibu wa kifungu cha 47 cha kununi hiyo.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kuwa chakula wanapelekewa lakini kilikuwa kinasuasua na kwa muda mrefu walikuwa hawapati chakula kwa utaratibu uliowekwa. Je, matatizo kama haya anahakikishaje kuwa hayatatokea tena?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba kupewa chakula ni moja ya haki ya mahabusu anapokuwa mikononi mwa Polisi.

Ni kweli kule nyuma kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge liliwahi kutokea tatizo hilo katika baadhi ya vituo vya Polisi lakini hivi sasa baada ya Bunge hili hili kuboresha bajeti ya Jeshi la Polisi moja ya vifungu katika bajeti ile ambayo mnaipitisha hapa ni chakula kwa ajili ya mahabusu.

Kwa hiyo, napenda kulihakikishia Bunge hili Tukufu kwamba sasa utaratibu uko madhubuti kwamba katika kila kituo cha Polisi, mahabusu wanaolala pale wanlishwa na Polisi kwa sababu sasa wanayo mafungu ya kulisha mahabusu.

Na. 59

#### **Umeme Kata ya Kikwe**

**MHE. TALALA B. MBISE aliuliza:-**

Kwa kuwa, Kata ya Kikwe – Arumeru Mashariki imeomba kupatiwa umeme kwa muda mrefu:-

Je, ni lini maombi yao yatakelezwa?

### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Profesa Talala Bana Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba *TANESCO* imepokea maombi ya kupeleka umeme katika baadhi ya vijiji nya kata ya Kikwe. Maombi hayo yamepokelewa na makadirio ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo yameshafanyika na taarifa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni kupeleka umeme Manyata, ujenzi wa *line* ya *Kv* 33 yeny urefu wa kilomita tano na ufungaji wa *transforma* mbili zeny uwezo au zeny nguvu ya *KVA* 100 kila moja na *line* ya kupeleka umeme wa majumbani zeny urefu wa kilomita sita unahitajika, gharama za mradi huu ni kama shilingi milioni 119,680,874.29 Sehemu ya pili ambayo imefanyiwa kazi ni kupeleka umeme Magadini laki tatu. Hapa panahitajika ujenzi wa *kilovolt* 33 yeny urefu wa kilomita 14, uwekaji wa *transforma* moja zeny uwezo wa *Kv* 200, *line* ya umeme wa majumbani zeny urefu wa kilomita 2.6 na gharama za mradi huu ni zaidi kidogo ya shilingi milioni 300.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu utatekelezwa baada ya fedha kupatikana (*Kicheko*)

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako mazuri sana na ambayo kwa kweli yanatutia moyo sana watu wa Kikwe sasa kidogo naona matumaini imbele. Viswali viwili vidogo, kwanza nakuomba tu utuhakikishie kwamba tutazamie kwamba ni lini tunaweza tukaona nishati ya umeme kata ya Kikwe, hiyo mipango tunatazamia ni lini tutaanza kuona matunda yake.

Pili, ni kwamba Wizara ilituahidi wakati fulani kwamba Seela umeme wake unaweza ukawa umeanza kujitokeza kuanzia mwezi Novemba mwaka jana na vipimo vyake vikafanyika, tunakuomba Mheshimiwa Naibu Waziri wananchi wamekuomba uwasaide kufuatilia ili kama inawezekana mpango huo utekelezwe mpaka sasa hivi wanasubiri na wanaomba washangilie kabla ya mwezi wa nane au tisa. (*Kicheko*)

Ahsante Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Profesa Talala Bana Mbise kama ifuatavyo:-

Kwanza kuhusu lini ni matarajio yetu kwamba mwakani wakati mradi mkubwa wa kuanza kupeleka umeme vijijini utakapoanza basi maeneo kama haya ya kata ya

Kikwe yatatiliwa maanani. Kwa hiyo, nimatumaini yangu kwamba wananchi wa maeneo hayo watafaidika na mradi huo utakapoanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu maeneo ya Seela kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba wakati hadi wakati hutoa matumaini kulingana na mipango iliyopo na mwaka jana tulitarajia kwamba pangeweza kufanyika kazi kama hii lakini kwa bahati mbaya kutokana na hali ya uendeshaji wa Shirika la TANESCO ulivyokuwa kutokana na ukame na kuhitaji fedha nyingi katika kupata umeme kwa njia nyingine baadhi ya miradi nchini ilikuwa imesimamishwa ili kuweza kutoa nafasi ya kuzalisha umeme. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ambaye najua amekuwa akishughulika na mimi na Wizara kwa ujumla sana katika masuala haya ya umeme kwamba pale ambapo nafasi itakapopatikana basi suala hili litashughulikiwa na wananchi wa Kikwe kwa kweli waweke matumaini kwa Mbunge wao ambaye amekuwa anashughulikia masuala haya. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Kuna matangazo matatu yafuatayo:-

La kwanza linatoka kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala anaomba anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 14 kutafanyika kikao cha Kamati chumba namba 231 ghorofa ya pili mara baada ya kipindi cha maswali. Agenda ni kupitia masahihisho ya fungu namba 92 Tume ya Kudhibiti UKIMWI, kwa hiyo Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala mara baada ya kipindi cha maswali mkutane. Tangazo la pili linatoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya anasema leo tarehe 14 Juni, ni siku ya maadhisho ya kuwaenzi watu wanaojitolea kutoa damu Hospitalini kwa dunia nzima. Anasema Watanzania wote wanaombwa kujitokeza kwa wingi siku hii kujitolea kutoa damu, anawaomba Waheshimiwa Wabunge wajijunge na Watanzania wenzao siku hii kujitolea kutoa damu. Hospitali ya Mkoa wa Dodoma imeandaa taratibu zitakazowawezesha Waheshimiwa Wabunge kutoa damu hapa hapa katika majengo ya Bunge. (*Makofi*)

Tangazo la tatu linatoka kwa Spika, nalo ni kwamba ngoja tuone, aah! kasi yetu ya kujadili bajeti inakwenda vizuri leo tarehe 14 waliojiandikisha kuomba kuchangia nimebaki na Waheshimiwa Wabunge 27. Kwa namna tunavyokwenda huwa wanapata nafasi kuchangia Wabunge wasiopungua 20, jana walichangia Waheshimiwa Wabunge 21 kwa hiyo kwa siku tunaweza tukatoa nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge 21 wakachangia. Leo tarehe 14 endapo watachangia Waheshimiwa Wabunge 21 maana yake watabaki Wabunge sita wa kuchangia siku ya kesho na huwa tunapanga muda kulingana na maombi ya kuchangia yaliyopo.

Kwa hali hii inaelekea mjadala wa bajeti unamalizika kesho badala ya alhamisi kama ilvyo kwenye ratiba yetu, kwa hiyo nawaomba basi sana tukumbuke kwamba kupiga kura ya kupitisha bajeti au kutokupitisha bajeti ni kura ya kikatiba. Tunatakiwa tuwaite majina mmoja mmoja ili kuhakikisha kwamba bajeti imepita. Kwa hiyo, ratiba ilisema kura za kupitisha bajeti zitapigwa siku ya alhamisi kwa hali niliyoieleza sasa hivi

itabidi kura hizo zipigwe kesho siku ya Jumatano kipindi cha jioni ili kutoa nafasi kwa watoa hoja kukamilisha au kuhitimisha hoja yao na wengine waliobaki kuchangia.Kwa hiyo, nawaomba basi tuzingatie tuweke akilini mwetu kwamba kesho kipindi cha jioni ndiyo muda wa kupiga kura za kuptitisha bajeti.

Mwisho wa Matangazo Katibu tuendelee na *Order Paper*.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mwongozo wa Spika

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Mutungirehi.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, naomba radhi. Tulikuwa na barua pale kwenye *Pigeon-Hole* kwamba atakuja Waziri wa Uingereza wa Masuala ya Afrika kesho sasa sijui na hiyo ikoje maana yake inaingiliana na hiyo au itakuwa tofauti?

**SPIKA:** Hapana haiingiliani kwa sababu huyo mgeni tumempa nafasi wakati Bunge halikutani yaani ni kipindi cha saa tisa na nusu mpaka saa kumi na nusu kwa hiyo sisi tunarejea saa 11:00 kama kawaida.

#### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2004, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2005/2006 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006**

*Majadiliano yanaendelea*

**SPIKA:** Waheshimiwa wanaokwenda kunywa chai wanaweza kwenda Msemaji wa kwanza ni Dr. Lucy Nkya, wa pili Mheshimiwa Mariam Mfaki, wa tatu Mheshimiwa Bernard Membe na wa nne ni Mheshimiwa Juma Kidunda, lakini nitamwita Msemaji wa kwanza baada ya wanaokwenda kunywa chai kuondoka.

Mbona siwaoni Bungeni? Mheshimiwa Dr. Lucy simwoni, Mheshimiwa Mariam Mfaki simwoni, Mheshimiwa Bernard Membe simwoni, sasa Mheshimiwa Juma Kidunda vilevile hayupo, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni namuona yupo unawenza kupata nafasi sasa. Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, atafuatiwa na Mheshimiwa na Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Remidius Kissassi na Mheshimiwa Profesa Mbilinyi. Sasa tunaanza na Mheshimiwa Dr. Chegeni naona hajajiandaa sawasawa, unawenza? Kama unawenza haya endelea.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotua mbili za Mipango na Fedha.

Kwanza ningependa kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wawili pamoja na wasaidizi wao kwa kuandaajabeti ambayo imekuwa ni kielelezo kizuri cha mwenendo wa hali ya uchumi hapa nchini na jinsi ustawi wa jamii unavyoendelea hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea kusema napenda vilevile niungane na Waheshimiwa wenzangu kwa kutoa rambirambi kwa mwenzetu Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga wa Jimbo la Kilombero. Naomba Mwenyezi Mungu ailaze pema roho yake peponi.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda niwapongeze wana CCM wote kwa kuweza kumchagua Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuwa mgombea mteule wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi.

Vivyo hivyo napenda niwapongeze Mgombea mwenza Mheshimiwa Dr. Shein, pamoja na Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Aman Abeid Karume.

Mheshimiwa Spika, kwa vile umeni *high jack*, umeniteka nyara sikuwa nimepangilia sana lakini nitajitahidi kusema kwa sababu ni wajibu wangu niseme na vile vile nilikuwa nimeomba kuchangia katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii mimi napenda niseme kwamba kwa Mtanzania yeoyote ambaye anajaribu kufuatilia mlolongo wa bajeti toka mwaka 2001 mpaka sasa hivi nadhani ataungana na mimi kusema kwamba bajeti hii ni bajeti ambayo inaonyesha ukomavu. Ni bajeti ambayo inaonyesha mwelekeo mzuri sana, lakini bajeti hii imezidi kulenga zaidi jinsi ambavyo nchi hii imejitahidi katika suala zima la kupambana na umaskini, suala zima la kuboresha Ustawi wa Jamii na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hivi leo hii Mtanzania gani anaweza kuona kwamba hatujapiga hatua, kwa sababu ukiangalia uwezo wa nchi inategemea na mapato yake. Wakati naingia Bungeni hapa mwaka 2001 tulikuwa na utegemezi wa bajeti kwa asilimia 48 sasa tuko asilimia 41 hii ni hatua moja kubwa sana na hii lazima tuwapongeze watendaji wote, tuipongeze Serikali ya awamu ya tatu kuanzia kwa Rais wake, Mawaziri wake, Makatibu Wakuu wote kwa sababu hii ni timu hawawezi kufanya mtu mmoja peke yake kuleta mafanikio yote haya.

Lakini pongezi za pekee nimpongeze Waziri wa Fedha, Waziri wa Fedha kwa kweli amekuwa *very consistent* katika bajeti zake na hii inaonyesha jinsi *trend* ya bajeti inavyozidi kukua. Unapoona kwamba ukusanyaji wa mapato umeongezeka nidhamu ya matumizi ya fedha imeongezeka na sasa hivi tumeweza kufanikiwa kupata msamaha wa madeni.

Hii siyo kwamba tunapata hela mpya, hapana. Ni uwezo wa Serikali sasa kutokulipa yale madeni tuliyosamehewa ambayo ni kama Dola za Kimarekani milioni 170 kwa mwaka, badala ya kuzilipa hizo fedha sasa tutazitumia kwa ajili ya kutengeneza

miundombinu yote ya uchumi na kukuza pato la Taifa na kupunguza umaskini. Huo ndio mkakati ambao sasa tujielekeze pale Watanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo nizungumzie mambo ambayo ni ya msingi. Katika mgao wote huu tunazungumzia kuboresha miundombinu ili tuweze kweli kupambana na umaskini, tuweze kweli kukuza pato la Taifa. Mimi napenda nijielekeze katika mikoa ya kanda hii ya *Central Corridor* mpaka Kanda ya Ziwa na Magharibi

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ningependa zaidi ijaribu kuelekeza namna gani ya kuweza kufumua au kutengeneza miundombinu sahihi. Tunazungumzia kwamba barabara, viwanja vya ndege, kufunua miundombinu ya elimu, afya, na hata nishati.

Mheshimiwa Spika, mimi sielewi mpaka leo hii unaposema kwamba katika nchi hii Mwanza ni Jiji, ni Jiji ambalo bado halijapewa hadhi yake kwa muda mrefu sana. Mwanza kuna uwanja wa ndege, ambao na wewe huwa unatua wakati ukienda Ukerewe, ule uwanja haufanani ile *terminal* yake haifanani na Jiji la Mwanza lakini nilisikitika sana kuona kwamba badala ya kujaribu kuelekeza zaidi mapato ili tuweze kupata mapato mengi katika kiwanja cha Mwanza tukaanza kujenga viwanja vingine vya ndege.

Tumeanza kujenga Songwe kule Mbeya, uwanja wa Arusha, Uwanja wa Moshi sasa vyote hivi kwa nini tusinganezia kwanza kuboresha pale ambapo tunataka tumnenepeshe ng'ombe tukamue maziwa? Uwanja wa Mwanza wa Ndege, una vivutio vingi, kuna utalii, samaki, madini kuna biashara nyingi sana mimi nadhani ningeomba sana katika bajeti hii Wizara ya Fedha watafute fedha kwa ajili ya kuboresha kiwanja cha ndege cha Mwanza na tujaribu kutokuji – *overstretch* (tusijipanue).

Leo unajenga kiwanja cha Songwe, mara cha Arusha lakini ukiangalia Arusha pale na Kilimanjaro kuna uwanja mkubwa wa Kimataifa, kuna haja gani ya kutoa kipaumbele katika kiwanja kingine cha Arusha badala ya kufanya Mwanza kwanza. Mimi ningeomba sana hili suala tujaribu kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile wananchi wa mikoa ya Singida, Tabora, Kigoma, Shinyanga na Mara wana matatizo makubwa ya gharama kubwa za bidhaa, leo bidhaa inapotoka Dar es Salaam inaletwa mpaka hapa Dodoma. *Loading points* ya vifaa hivi ni kuanzia hapa Dodoma kwenda mikoani huku huwezi ukapata mabehewa mpaka ulete kwa magari. Hii yote inaongeza gharama kwa watumiaji wa bidhaa kutoka bandari ya Dar es Salaam na hawa Watanzania wa Mikoa hii hawana matatizo na nchi yao, kwa nini Serikali sasa isijaribu kuwapunguzia gharama hizi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano pale Ukerewe mfuko mmoja wa *Cement* ni shilingi 15,000/= wakati Dar es Salaam mfuko wa *cement* ni shilingi 7,800/= mpaka 8,000/= huyu mtu anabeba gharama ya zaidi, sasa ukija bidhaa nyingine mbalimbali unakuta gharama ni kubwa zaidi. Mimi ningeomba kwa kweli Wizara ya Fedha kupitia bajeti hii watafute jibu mbadala kupunguza gharama kwa wananchi wanaokaa kwenye mikoa hii ambayo nimeitaja.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile ningependa kusema kwamba kuna hili suala la madini, mimi mpaka leo hainjii akilini tukisema kwamba sawa tumerahisisha wawekezaji katika sekta za madini, wamewekeza tunapata kodi kutokana na *payment* labda mishahara na *VAT* lakini bado hawa wawekezaji tumewapa migodi hii bure. Mwekezaji anakuja hapa na *briefcase* anapewa eneo la kuchimba lakini anapopewa Serikali haina *concern* yoyote pale. Kwa hiyo, asilimia mia moja huyu mtu ana *own* ule mgodi.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Ghana, mimi nimeshawahi kukaa Ghana Serikali ya Ghana ilikuwa bado inahifadhi asilimia 20 ya *ownership* ambayo inakuwa ni *golden share*, maamuzi yoyote muhimu hayawesi kufanyika bila kwanza Serikali yenyewe kukubali lakini sisi tunatoa migodi kwa asilimia 100. Mimi nadhani katika kujaribu kupitia suala zima la uwekezaji tujaribu kuboresha baadhi ya vipengele ambavyo vitatoa ridhaa kwa Watanzania kuweza kumiliki raslimali zao badala ya kuachia tu wageni wanamiliki.

Mheshimiwa Spika, Suala hili nimeongea hata kwenye Kamati na Mheshimiwa Waziri wa Mipango alilijibu na katika kulijibu akasema kwamba Serikali ya Ghana inatoza mrabaha kwa asilimia tatu kama sisi. Ni sawa lakini sisi tumewapa kwa asilimia mia kwa mia kwa nini Serikali isijaribu kuona upya ni namna gani Watanzania washirikishwe katika kumiliki raslimali zao.

Mheshimiwa Spika, tunasema kwamba nchi yetu kwa mfano mwaka jana ile *Net Export* ya madini inafikia takriban dola za Kimarekani milioni 680 sawa tumeuza, lakini hoja yangu ni kwamba ni hela ngapi imekuja hapa Tanzania? Kwa sababu hawa watu wawekezaji wanakuwa wana *foreign accounts*, wana *off shore account*, wanaleta makampuni kutoka nje ambayo yanajaribu vile vile kufanya kazi na kupeleka pesa nje. Hela inayokuja hapa Tanzania ni ndogo sana, leo hii wenzangu wa Geita Mheshimiwa Mabina na watu wake kila siku wana kelele, hivi Geita mmefaidika nini na mgodi wa Geita?

### **WABUNGE FULANI:** Hakuna!

**MHE. DR. RAPHEL M. CHEGENI:** Leo hii ukimwambia mwananchi wa Mwanza kwamba tulipoona tunajenga migodi Shinyanga, Kahama, Biharamulo, Nzega kwamba mikoa kama Mwanza ni Jiji ni *Center* ungepanuka. Hawa watu wanajenga vijiji vyao, vijiji ambavyo bado havitoi nafasi kwa Watanzania kushiriki vizuri zaidi, hata nyanya zinaagizwa kutoka nje, hata pilipili inatoka nje, nyama inatoka nje, sasa kweli watanzania wanashirikishwa vipi katika kufanya biashara na kuleta mzunguko wa fedha katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa sanasana tujaribu kuyaangalia tusiende kwa vigezo vya takwimu peke yake bali tujaribu vilevile kuangalia ni namna gani watanzania wananzaika.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika bajeti hii sijaona ni namna gani vijana wameelezewa jinsi ambavyo watanufaika na mtazamo mzima wa bajeti hii. Hivi leo hii vijana hawa tunawapeleka wapi? Kwa sababu zaidi ya asilimia 28 ya vijana wengi wanatoka vijijini kwenda mijini kwa sababu ndiko kwenye raha huko ndiko kwenye maisha, vijijini hawana umeme, hawana maji safi na miundombinu haipo. Sasa ni namna gani tatizo la vijana limekuwa *addressed* katika bajeti hii, hao vijana ndiyo wanaokuja kwa kasi na ari na kila kitu. Ndiyo vijana hawa.

Mheshimiwa Spika, lakini ni vizuri zaidi katika bajeti nadhani labda Mawaziri husika wajaribu kuelekeza hizi Wizara za kisekta kweli wajaribu kuainisha ni namna gani vijana watashirikishwa katika mchakato wote huu wa bajeti, wasipopata ajira ni tatizo na ili ndoto iweze kutimia Watanzania kwamba wanapata ajira inavyotakiwa basi ni vema bajeti hii ijaribu kubainisha tatizo la ajira ya vijana itashughulikiwa kwa kujenga mfumo imara na endelevu wa kuwapatia ajira.

Mheshimiwa Spika, suala jingine ambalo ningependa kulizungumza haraka haraka ni suala la kilimo. Hii bajeti tumesema kwamba inaboresha miundombinu lakini sielewi kilimo ni namna gani kitaboreshw, wakulima kila leo tunarudia hivi mimi nina miaka minne sasa Bungeni, mkulima kila leo hajanufaika na kilimo cha Tanzania lakini Wizara ya Kilimo ipo siku zote.

Wanafanya nini sielewi, kila mwaka tunatenga bajeti mimi nadhani tungakuwa na makusudi kabisa ya kuanzisha kilimo ambacho kitaonekana kwamba watanzania tuna *move* kutoka *point one* kwenda *point B* ili mkulima huyu aweze kunufaika na hata kama ni ubora wa kilimo uweze kuonekana.

Sasa inakuwa kila siku ni mikakati tunapanga tuko mbioni, Keenja anamaliza miaka mitano sasa hivi ukimwambia leo hii Mheshimiwa Keenja umefanya nini kama Waziri wa Kilimo sijui kama Watanzania watamwelewa kila leo Watanzania kukicha wakulima wana malalamiko, kila kukicha wana malalamiko na ndiyo sekta kubwa zaidi na tuna *target* kupata mapato mengi zaidi kutokana na kilimo kwa sababu uchumi wetu unategemea zaidi kilimo.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa zaidi hili suala la kilimo vile vile lijaribu kuzungumziwa kwa upana zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini katika hili bado vile vile nizungumzie kwamba uchumi wetu unategemea zaidi misaada kutoka nje. Ndiyo hatuna jinsi ya kujikomboa lakini ndiyo hatua ambayo tumeifanya sasa hivi kwa hiyo mtu anasema kwama uchumi wetu ni tegemezi, ndiyo ni tegemezi tumeanza kupata faida ya kuanza kufutiwa madeni na Mheshimiwa Mramba nilimwona kwenye *TV* jana akijaribu kuelezea jinsi watu wanajaribu kuwa *confused* wanadhani kwamba hizi fedha tunazo sasa tunataka kutumia, hapana. Ndiyo badala ya kulipa ndiyo tuzitumie katika kuelekeza katika sekta ambazo ni muhimu zaidi.

Lakini nadhani ni vema zaidi sasa uchumi wetu huu ujaribu sasa kuwianisha matakwa ya Watanzania, sasa tumepata unafuu wa madeni bado tuendelee kuwaomba wakubwa watufutie madeni hata wale *donors* wengine, wahisani wengine ambao wanatufadhili tuwaombe watufutie madeni.

Haya madeni mengi ni kwa faida yao si kwa faida yetu kama ni kukosa sisi upande wa *TASAF* tumekopa na tumeona matunda nani asiyejua mpango wa *TASAF* hapa sasa hivi, mpaka kijijini mpaka sasa wameshaona umuhimu wa *TASAF* leo hii katika bajeti hii tunaambiwa kwamba mpaka kijiji kitakuwa kinaendesha pesa yake yenyewe, kitakuwa na mfuko wa kuendesha pesa huu ni kujenga uwezo kwa wananchi na ndiyo ilikuwa *drive* kubwa kwa nchi hii kujua kwamba wananchi sasa wanapewa uwezo wa kuweza kuendesha nchi yao.

Mheshimiwa Spika, katika hili mimi nawapongeza sana na ningependa kusema kwamba yote haya yatakuwa vizuri tu kama nishati na yenyewe itazingatiwa. Kwa sababu bila kuwa na nishati jitihada zote hizi bado haziwezi kutimilika.

Ombi langu kubwa zaidi ni kwamba matatizo kama *IPTL* tuyatafutie ufumbuzi, hatuwezi kuwa tuna huyu mnyama *IPTL* tunaendelea kumfuga kila siku. Huyu anakula zaidi kuliko tunachopata sisi hebu tuwe na mkakati wa kuweza kumwondoa moja kwa moja kama ni kumnunua basi tumnunue kama ni viyi basi tupate njia nyingine mbadala ya kupata umeme na nishati, hii itazidi kupunguza gharama ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machaache naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi kuchangia hoja hizi mbili zilizo mbele yetu. Kabla sijafanya hivyo nami ningependa kuchukua fursa hii kutoa rambi rambi zangu za dhati kwa msiba uliotupata sisi Wabunge kwa kifo cha Marehemu Ndugu yetu Abu Kiwanga. Namwombea Mwenyezi Mungu amweke mahali pema peponi na awape familia yake subira.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua fursa kutoa pongozi zangu za dhati sana kwa Mawaziri wa Mipango na Fedha pamoja na Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na wataalam wote ambao wameshiriki katika kuandaa mipango na bajeti hii. Kusema kweli mipango hii ni mizuri sana na bajeti ni tulivu na iliyoelekezwa katika kupambana na umaskini katika kujenga uchumi wetu na kutoa watu wetu katika umaskini.

Vigezo vyote ambavyo vimetumika na viashiria mbalimbali na takwimu zilizotolewa zinadhihirisha ukweli huo. Ninashukuru kwamba Waheshimiwa Mawaziri wameeleza hayo kwa undani katika hotuba zao walizotoa na vile vile Waheshimiwa Wabunge waliotangulia wameeleza haya kwa undani sana.

Mheshimiwa Spika, wale Ndugu zetu ambao wanabisha kwamba hakuna lolote lililofanywa na Serikali ya CCM awamu ya tatu wanasutwa na takwimu na viashiria

vilivyotolewa humu ndani ambavyo vinaonyesha dhahiri maendeleo makubwa yaliyopatikana.

Ukiachilia mbali vishiria hivi na takwimu zilizotolewa bila shaka tumajionea maendeleo mengi na makubwa ambayo yamepatikana katika kila upande wa nchi yetu kama vile barabara, hospitali, zahanati, vituo vy'a afya, shule, maji safi na vitu mbalimbali ambavyo vinaonekana dhahiri kabisa ambavyo vinaonyesha maendeleo makubwa yaliyopatikana.

Zaidi ya hiyo ni kwamba nchi yetu imejipatia heshima kubwa sana katika nchi za jirani za Afrika na nchi nyingine za dunia. Tanzania kuwepo moja ya nchi 18 za Afrika zilizosamehewa madeni kwa asilimia 100 ni sifa kubwa sana kama ambavyo Mgeni wetu aliyejukua mgeni wa Rais aliyejukua Jumamosi iliyopita alielezea.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua fursa hii kutoa pongozi kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais, Jemedari wetu hodari ambaye ameweza kuongoza Taifa letu hili kwa ufanisi mkubwa na mafanikio makubwa kama haya ambayo yamepatikana.

Takwimu zilizopo na viashiria vinaonyesha dhahiri ni hatua gani zimechukuliwa kuimarisha uchumi wetu mkuu, kuweka misingi imara kwa kuleta maendeleo endelevu ya kasi kubwa zaidi ya uchumi wetu na huduma za jamii na ustawi wa jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda kusema kwamba, kama walivyoeleza Waheshimiwa Mawaziri na kama walivyoeleza baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kabla yangu kwamba, bado zipo nafasi nyingi za kuendeleza zaidi. Kama nilivyosema, tumeptata maendeleo makubwa lakini kasi yetu ya maendeleo bado haitoshi, bado tunahitaji kasi kubwa zaidi ya asilimia kumi. Sasa ili tufanye hayo hatuna budi kwanza kujidhatiti vizuri kwa mafanikio mema tuliyoyapata. Mafanikio mema tuliyoyapata ili kuyaendeleza mageuzi yanahitajika katika sehemu zote na kuweza kuwa na nidhamu zaidi, utaratibu mzuri zaidi na kupambana na maovu na mianya yote ambayo ilikuwepo katika masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo ambayo pengine tungeweza kufanya vizuri yametajwa kwa sehemu kubwa nisingependa kurudia. Labda nirudie yale maeneo ambayo nadhani kwamba yangeweza kuchangia zaidi. Katika Ilani ya CCM ya mwaka 2000 tumezungumzia habari ya *modernization*. Neno la kizungu *modernization* tukalifanya kwa Kiswahili modenizesheni. Ni kweli jitihada nyingi zinafanywa, lakini naona bado tuko mbali sana kutokana na jinsi tunavyofanya *modernization* kwa sababu hapo bado shughuli yetu kuu ya uchumi kilimo bado inafanyika katika hali ya kizamani kabisa. Vyombo vy'a kisasa vy'a kilimo, pembejeo, utaalami mbalimbali ambao unatakiwa bado haujapatikana kufikia kiwango kinachotakiwa. Sasa hilo ni suala ambalo tulitakiwa tulifanyie kazi kwa karibu zaidi ili tuhakikishe kwamba kilimo chetu kinakuwa cha kisasa na cha kuaminika, bila kutegemea mvua. Mambo kama hayo yafanyike vizuri kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, pili, tunafurahi kwamba ubinafsishaji umesaidia sana na umeleta manufaa mengi kama hivi ambavyo Mawaziri wameeleza katika hotuba zao. Kwa sehemu kubwa tumepata faida kubwa sana, lakini kuna sehemu katika ubinafsishaji ambayo inatokana na binafsi kwa binafsi ambayo mara nyingi Serikali au vyombo vyta Serikali kama *PSRC* au *LART* haishughulikii. Huko mara nyingi kumekuwa na usumbu na mianya ya kuweza kuhujumu uchumi. Kwa mfano, tunajua mambo yaliyotokea katika mashamba yale ya mkonge ya Chavda, ni mfano ambao si mzuri na hivi karibuni umetokea mfano mwengine wa mashamba yaliyokuwa ya *Amboni Limited* wamefanya mambo ya kiajabu ajabu na kuweza kuchukua fedha nyingi sana kutoka nje nje kwa utaratibu usiokubalika.

Mheshimiwa Spika, sasa nadhani kwamba ipo haja kwa Serikali kuona utaratibu, kama si Wizara hii Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kikawepo chombo maalum au Idara maalum ya kuweza kusimamia sekta ya binafsi ambayo haitopitia chini ya *PSRC* au utaratibu wa Kiserikali ambao tunaufahamu rasmi, kwani kwa kufanya hivyo pamoja na kwamba tuna uchumi huru na utandawazi lakini katika utandawazi humo humo kunaweza kuwa na utandawizi. Kwa hiyo inakuwa ni vizuri tukiwa macho juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la ushirikiano na nchi jirani. Nashukuru tumefanya jitihada nyingi sana kushirikiana na nchi jirani za Kenya, Uganda na vile vile nchi za *SADC* na nchi zingine za Maziwa Makuu. Nafasi nzuri sana zimejitokeza za kuongeza biashara zetu. Kwa jumla kwa hawa wenzetu tumekwenda nao vizuri sana na bado nafasi nzuri sana zinajitokeza, lakini bado nafikiri sisi tunahitaji kufanya maandalizi wenyewe humu ndani ya kuweza kijiandaa kuchukua hatua za kuboresha bidhaa zetu, huduma zetu, za kuwa na bei nzuri ili masuala hayo yaweze au bidhaa zetu na huduma zetu ziweze kuwa za ushindani katika masoko ya nje hasa ya nchi jirani. Kwa nchi za nje bado tumekuwa na matatizo makubwa sana na vizuizi mbalimbali visivyo vyta kiushuru na nchi zilizoendelea, nchi zilizoendelea zina vikwazo ambavyo wanaitwa *technical barriers to trade* na vitu kama *sanitary* na *fatal sanitary barriers* ambazo ni nyingi sana na zinatuletea vikwazo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mazungumzo yetu katika *world trade Organization* mazungumzo yetu tunapozungumza na *European Union* katika masuala ya *Economic Partnership Agreement* ni vizuri yawe yanazingatia kuangalia sisi kuchukua nafasi. Nafasi zile tulizopewa na *EBA* au *AGOA* kusema kweli zipo lakini hazitoshi kiasi chake na kwa bahati mbaya kwa upande wake mwengine hatujajiandaa vyta kutosha kuchukua nafasi hizo. Kama alivyoleza mgeni wetu aliyepeita hapa kwamba moja ya changamoto kubwa tuliyonayo sisi ni kuhakikisha kwamba tunapata bidhaa nyingi zaidi tuongeze mauzo yetu ya nje na kupata wawekezaji zaidi. Lakini sasa hao wawekezaji watakuja vizuri na mauzo ya nje tunaweza kuongeza, lakini wenzetu nje tuwashauri au tuwaombe na katika Tume hiyo ambayo Mheshimiwa Rais wetu alikuwa Kamishna, natumaini suala hilo alilijibu Mheshimiwa Rais kwamba yapo mazungumzo ya masuala ya *fair trade* kwamba iwepo *a fair trade* ama sivyo tutaendelea kupata vikwazo. Tumeona kwa mfano, alipozungumza mgeni wetu pale jinsi ambavyo China wamejitatihidi kutengeneza bidhaa za nguo vizuri na bidhaa nyingine nyingi, lakini sasa nchi

zilizoendelea zinaweka vikwazo ambavyo si vya kawaida. Kwa hiyo, hayo ni masuala ambayo pengine tunahitaji kuyashughulikia vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, ni suala la uwezeshaji wananchi. Nashukuru kwamba Serikali imefanya jitihada kubwa sana kuwawezesha wananchi kwa kuongeza wataalam wa fani mbalimbali katika shughuli za ugani. Vile vile imejaribu kutafuta taratibu za mikopo kwa kupitia vituo mbalimbali na taasisi mbalimbali. Suala hili linahitaji liboreshwe zaidi ili kuhakikisha kwamba Serikali inawasaidia wananchi kuunda Vyama vya Ushirika ambavyo lazima vijidhatiti kufanya masuala haya.

Mheshimiwa Spika, suala moja la kufurahia na kujivunia katika mafanikio makubwa ambayo yamepatikana ni kwamba, zaidi ya kuwapunguzia kodi wananchi, kodi ya maendeleo, vile vile Serikali imefanya jitihada kuwalipa wastaifu wa zamani ambao hawakuwapo katika orodha na kuwarudisha katika orodha. Ni jambo la kupongeza na la faraja kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile inafurahisha kuona kwamba, katika bajeti ya mwaka huu zimetengwa shilingi hamsini milioni kwa ajili ya kuwalipa wastaifu waliokuwa watumishi wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ya zamani. Kweli ni hatua nzuri iliyofanyika, lakini ninavoyelewa mimi ni kwamba deni hilo ni zaidi ya shilingi mia nne na hamsini bilioni na hii hamsini milioni ni kiasi kidogo tu, sijui utaratibu gani utakaofanywa juu ya suala hilo. Kwa hiyo, hilo ni suala ambalo naomba Serikali ilitazame.

Mheshimiwa Spika, tukirudi kwetu ningependa kusema kwamba, Jimbo letu la Mkinga limekuwa na maombi mengi sana ambayo bado napenda kuyarudia. Barabara ya Tanga-Horohoro, ni barabara muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. Kwa bahati mbaya sijaona popote katika bajeti hii au katika viambatisho vyake mahali inapozungumziwa juu ya ujenzi wa barabara ya Tanga-Horohoro. Vile vile barabara ya Pangani-Dar es Salaam ambayo tumezungumzia mara hii kuwa ni muhimu hajatajwa. Bandari ya Tanga kutengenezwa kama ndio mhimili muhimu hajatajwa. Wananchi wa Tanga walipata matumaini makubwa sana baada ya kuja Mheshimiwa Rais wa Rwanda hapa na kuamini kwamba bandari hiyo itatengenezwa, lakini haikutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumekuwa na maombi ya muda mrefu sana ya Wilaya ya Mkinga. Kwa bahati mbaya hayo nayo pia hayajajitokeza katika mwelekeo wa bajeti iliyopo na kidogo wananchi wetu wana masikitiko makubwa sana juu ya suala hilo. Vile vile kwetu pamoja na kuwa na milima ya kutosha na mito lakini tatizo la maji limekuwa ni tatizo kubwa sana. Tumelizungumzia sana tatizo hili kwa muda mrefu, lakini bado hatujapata maendeleo mazuri. Tunashukuru kwamba na sisi Wilaya yetu imetiwa katika mpango wa Benki ya Dunia, lakini maji tunayahitaji sana. umeme ni suala muhimu sana kwa maendeleo kama tulivyozungumza na Jimbo letu la Mkinga tumeomba maombi ya umeme muda mrefu, lakini hatujaweza kupata mafanikio hayo na bado natumia fursa hii kulieleza hapa nikiamini kwamba, mpango huu na bajeti hii ndio inaelekeza masuala hayo ambayo najua tutapata fursa ya kuzungumza katika wakati wa

sekta, lakini ni vizuri kuzungumzia sasa hivi katika kipindi hiki cha majumuisho ili kwamba yawekewe maanani na tuweze kupatiwa mahitaji hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nasema kwamba nashukuru bajeti hii imekuwa nzuri, tulivu, imeweka misingi mizuri, ina mwelekeo mzuri na inaleta matumaini mazuri kwa wananchi. Naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. Ahsante sana. (*Makofit*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge orodha ya wasemaji imewekwa kwenye ubao wa matangazo kule nje na ambao hawakuwepo jana walipoitwa waliwekwa mwanzo katika orodha ya leo. Lakini bado hawapo. Sasa ninawashauri Waheshimiwa waliopo kwenye chai wakaangalie orodha, tunawaita jinsi ilivyopangwa orodha iliyopo kwenye ubao wa matangazo.

Sasa namwita Mheshimiwa Remidius Kissassi, Profesa Mbilinyi ajiandae na Mheshimiwa Makinda ajiandae. Mheshimiwa Halimenshi Mayonga na Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga watafuatia.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nitoe mchango wangu kuhusu hizi hoja mbili zilizopo mbele yangu. Lakini awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote kwa kutupa nafasi ya kutufikisha hapa tulipofika leo kwa salama na amani.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kuungana na Wabunge wenzangu kuwapa pole za rambirambi ndugu na jamaa wa familia ya Mheshimiwa Abuu Kiwanga ambaye ametutoka katika kipindi cha hivi karibuni. Namwomba Mungu amlaze mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, tatu, napenda kuungana na wana CCM wenzangu na wananchi wote wanaopenda amani, kumpongeza ndugu yetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa kuchaguliwa na CCM kuwa mgombea wa kiti cha Urais. Vile vile, napenda kumpongeza mgombea mwenza Dr. Ali Mohamed Shein na mgombea wa Urais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume na *Inshallah* Mwenyezi Mungu atawajaalia wapate ushindi wa kishindo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nichukue nafasi hii kuwatakia kheri Wabunge wenzangu ambao tunakwenda kwenye kinyang'anyiro muda si mrefu, basi na wao wafanye kweli na tukutane humu Mungu akijaalia katika Bunge lijalo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Fedha kwa hotuba zao nzuri ambazo zinaleta matumaini na kwa kweli tunaona kila dalili ya kuwa huko tunakokwenda kuna mwanga. Kwa hiyo, nitoe mwito kwa wananchi kuzipokea hotuba hizi mbili na tuzifanyie kazi ili tuongeze ubora wa uchumi wetu na hivyo kuongeza ufanisi katika maendeleo ya mmoja mmoja na maendeleo ya wote kiuchumi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba niwapongeze wasaidizi wao Makatibu Wakuu pamoja na Makamishna kwa kazi nzuri na wafanyakazi mbalimbali wa Mipango na Ubinafsishaji na Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri wanazotufanyia Watanzania na hivi leo tunaona bajeti ambayo inatia matumaini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichangie machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niongeze katika jedwali hili la kwanza la *financial statement and revenue estimates* kwenye *table two, proposed changes in taxation*. Katika aya ya 1(3) ambapo kuna *third schedule of Value Added Tax to include mobile health clinics under item five*. Ningeomba tuongeze neno *plus fire rescue vehicles*.

Mheshimiwa Spika, nimesema tuongeze hili kwa sababu sasa hivi haya magari ya zimamoto tumeanza kuona umuhimu wake. Kwa hiyo, nafikiri kama tutayapa motisha wananchi wetu wenye uwezo wa kuleta magari ya zimamoto watasaidiana na Manispaa yetu ili kuleta kinga na usalama zaidi katika Miji yetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa kutoa pendekezo katika hotuba ya Waziri wa Fedha, ukurasa wa 36, *item (8)*, kuwa, Serikali imeamua kutenga moja ya nane ya ada ya ufundi stadi, *skills development levy*. Mimi nilitaka kupendekeza kuwa badala ya kuwa moja ya nane iwe ni moja ya nne kwa sababu sasa hivi tumeona umuhimu wa vijana wetu kupata elimu ya ufundi katika ngazi mbalimbali na nina hakika tukiweza kutunisha huu Mfuko vile vile maana yake ni vijana wengi zaidi watapata elimu hii ya msingi na hii itasaidia kupata ajira kwa kujitafutia ajira katika miradi mbalimbali ambayo sasa hivi Serikali inatekeleza katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, naomba nipendekeze kuwa, huu Mfuko wa Elimu Tanzania utenge fungu maalum la kuwasaidia ndugu zetu wenye ulemavu ili waweze kusaidiwa kupata elimu siyo ya ufundi tu lakini hata elimu ya juu kwa sababu tunajua mazingira magumu ambayo yanawakuta katika kupambana na hali ngumu ya maisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali hii kwa kazi kubwa iliyofanya mpaka ikastahili kusamehewa madeni yake mengi. Hii inatokana na kazi kubwa ya Serikali ya Rais Benjamin Mkapa. Lakini vile vile inatokana na jitihada nzuri ya wasaidizi wake Mawaziri na vile na sisi Wabunge tumechangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha suala hili. Naomba nitoe ombi na rai kuwa, fedha za msamaha ambao umepatikana zitumike zaidi kuimarisha miundombinu kama vile barabara, maji na umeme. Kwa sababu haya ni maeneo ambayo kwa kweli watu binafsi si rahisi kuchangia nguvu zao, lakini wananchi wetu wakihamasishwa vizuri wanaweza kuendelea kuchangia masuala ya elimu na afya. Kwa hiyo, mkazo utiliwe kwenye masuala ya barabara, maji na umeme.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna hii *concept* mpya ya *mini tiger* ambayo Serikali imeona umuhimu wa kuendeleza na kuanzisha hizi *Special Economic Zones*. Nilikuwa nataka kupendekeza kuwa, mpango huu ni mzuri kwa vile unatoa msukumo maalum kwa maeneo maalum ambayo yanaweza kutupatia maendeleo haraka. Tatizo langu ni kuwa, mpango huu wa *Special Economic Zones* usiishie huku bara isipokuwa vile vile ushirikishe maeneo ambayo tayari yalikuwa yameshatengwa kule Unguja kama vile sehemu ya Fumba katika Jimbo la Dimani, lakini vile vile Pemba katika maeneo ya Micheweni. Maeneo haya yametengwa muda mrefu sasa zaidi ya miaka kumi na tano lakini kwa kweli imeshindikana kutumika kuleta maendeleo tarajiwa kwa sababu hakuna miundombinu kama barabara, maji ya nguvu, wala umeme wa kutosha na hayajasafishwa, baadhi ya maeneo yalisafishwa lakini yameachwa vile vile. Sasa naomba Serikali ya Muungano ishirikiane na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha kuwa sasa *program* hii ya *Special Economic Zones* inashirikisha maeneo hayo muhimu kwa ajili ya kupata maendeleo katika visiwa vya Zanzibar na hivyo itasaidia kuleta maendeleo kwa Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nilitaka vile vile kusema kuwa kama Wabunge wenzangu kutoka Zanzibar walivyosema, Bandari ya Zanzibar imeshuka sana katika kutoa huduma kwa sababu ni mbovu. Lakini vile vile biashara yenewe imepungua sana. Sasa nataka kutoa pendekazo na rai kuwa, iundwe Kamati ya Wataalam, lakini vile vile na wanasiwa tuwemo ili tuangalie namna gani tutaweza kuhuishwa ile biashara iliyokuwa inafanyika katika bandari ya Zanzibar. Mimi nina hakika sio lengo la Serikali zetu hizi kuwa biashara iende upande mmoja tu wa muundo na upande mwininge ulale, lakini sasa kuna namna ya kucheza na masuala ya kodi ili kuhakikisha kuwa Bandari ya Zanzibar nayo inatoa huduma katika kiwango cha hali ya juu na biashara maalum ziwepo ambazo zinakwenda Zanzibar halifu tena zije katika Ukanda mwininge wa Afrika Mashariki. Lazima Zanzibar ipate biashara kwa vile haina maeneo makubwa ya kusema na sisi tuna katani, chai, kahawa na kadhalika, isipokuwa Zanzibar inategemea zaidi bandari, uvuvi, mazao ya karafuu pamoja na viungo. Sasa ni muhimu kwa Serikali zetu mbili za CCM ziangularie basi namna gani tutaweza kuharakisha maendeleo katika pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda vile vile kuipongeza sana Serikali yetu kwa kuwaona wafanyakazi wa zamani waliokuwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao kwa kweli walipunjwa na tumeona busara kuwarudishia na kuwapatia haki yao. Tatizo langu mimi ni kuwa Zanzibar nako kuna wafanyakazi wengi tu waliokuwa wanafanya kazi katika Jumuiya hii, lakini wanachanganyikiwa hawajui hasa waende kwa nani kupata haki zao. Hilo naomba nipayendekeze kuwa basi pale Unguja iteuliwe Ofisi kama itakuwa ni *TRA*, Wizara ya Fedha au Mipango wawe wana-coordinate suala la hawa wafanyakazi wastaaful. Lakini vile vile naomba niipongeze Serikali ya Muungano kwa kurudisha baadhi ya wafanyakazi ambao walikuwa wamestaafu katika kupata tena pensheni zao. Hivyo natoa mwito kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuiga hili jambo jema kwa sababu na Zanzibar nako kuna wafanyakazi ambao kwa kweli wapo taabani na ni vizuri kile kima chao cha pensheni kikaongezwa na wakawa wanapewa katika muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nirudie kusema kuwa kwa kweli mimi naunga mkono hoja zote mbili ambazo zimeletwa mbele yetu na tunaomba baada ya marekebisho haya machache basi tuitakie utekelezaji mwema. Ahsante sana. (*Makofit*)

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, nami natoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi ili niseme machache tu kuhusu hoja tulizonazo hapo mbele. Lakini kabla sijachangia, nami nataka kuunga mikono wale walionitangulia kwa kutoa rambirambi zangu za dhati kwa wale ndugu zetu Wabunge pamoja na Waheshimiwa wengine waliotutangulia mbele ya haki na nikiwatataja kwa majina ni Mheshimiwa Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo, Mheshimiwa Bomani ingawa alikuwa Mbunge wa zamani na Waziri wetu wa zamani. Mheshimiwa Abuu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero; Mheshimiwa Thadeus wa Ulanga Mashariki; Mbunge wa Mbeya Vijijini na Mbunge wa Kasulu. Hawa wote Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, rambirambi pia ziende kwa ndugu na jamaa wa Wabunge wa zamani hao ambaa nimeshawataja.

Mheshimiwa Spika, naungana pia na wenzangu walionitangulia kwa kuwapa pongezi nyingi sana wale waliofika fainali ya uteuzi wa CCM kule Chimwaga, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, mgombea wa Urais na Mheshimiwa Mohammed Shein, mgombea mwenza na Mheshimiwa Karume kwa kuwa mgombea wa Urais wa Serikali ya Zanzibar. Hao pia tunawapa hongera na pongezi kubwa sana. Nadhani pongezi za Chimwaga ziende pia kwa wale waliofika fainali, tunaishia walioshinda tu, lakini pia waliofika fainali wanahitaji kupewa pongezi zao na hao ni wawili; Profesa Mark Mwandosya na Mheshimiwa Salim Ahmed Salim. Katika kumi na nane wale watatu bora wamo, katika hilo nawapa pongezi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa michango yangu ya pongezi na rambirambi, naomba nitoe machache yahusuyo *budget speeches* mbili tulizonazo hapa. Kwanza kabisa niwapongeze Mawaziri kwa kusoma *speech* zao kwa murua kabisa na kutueleza kwa undani na kwa kinaganaga lakini kwa kifupi yale ambayo waliweza kuyafanya mwaka jana tangu walipotoa *speech* zao za mwaka uliopita. Ninawapa pongezi Mheshimiwa Mramba na Mheshimiwa Kigoda, Manaibu Mawaziri na Makatibu Wakuu na sisahau kuwapongeza pia watu wa *TRA* waliofanya kazi nzito ya kukusanya hela na kuvuka hata lengo kama tungeita na kufikia trilioni kutoka bilioni kwa mwaka huu unaoishia sasa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, tunasemaje juu ya mapato na matumizi. Kwa kweli mimi nasema natoa pongezi na sifa kubwa kwa *TRA* kwa kufanya vizuri. Kwa upande wa mapato, nadhani Serikali yetu miaka yote imeweza kufanikisha yale waliyokadiria, waliyafikia na mara nyingi walivuka malengo kwa ukusanyaji wake, lakini bado tatizo kubwa tunalo katika matumizi.

Mheshimiwa Spika, hii inatokana na sababu kwamba hatuna chombo kinachoweza kusimamia, kuamua na kudhibiti matumizi ya mapato yetu ya Serikali. Tumefika bilioni mwaka juzi, mwaka huu tupo kwenye trilioni nne, yaani inakwenda haraka sana na mwakani itakuwa trilioni tano au sita. Lakini shida ni tunatumiae, nani anaamua, mtu mmoja, Waziri peke yake, au yeye na Kamashna wa Bajeti au kikundi tu Hazina kinachoamua kuwa hizi fedha ingawa Bunge linatoa kwa jumla kuwa Wizara fulani ipate kadhaa, Wizara hii ipate kadhaa, lakini baada ya hapo nadhani zile *warrant of funds* zinatolewa na zikishatoka zitafika kwenye Wizara na Wizara itakasimu, inaendelea kukasimu mpaka inafika maofisa wale wa chini na fedha zinatumika. Hivyo ndio tunaona sasa mara nyingi fedha zinakwenda, huenda asilimia themanini zinatumika barabara na asilimia ishirini hazitumiki barabara, zinatembea au zinazagaa tu au zinakwama njiani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikuwa napendekeza kuwa, kama ikiwezekana Serikali yenyewe pamoja na Wabunge au watafute wataalam wa kutengeneza chombo cha kusimamia na kudhibiti matumizi ya Serikali kama chombo tulichonacho cha *TRA* kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato tuwe na chombo pia kingine cha kusimamia na kudhibiti matumizi ya *revenue* hizo zinazokusanywa na *TRA*.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka kulichangia ni kuhusu Sekta sitawenza kuchangia Sekta zote lakini zile chache ambazo nimeweza kuziweka akilini mara moja nichangie hizo kwa haraka mara moja nazo ni zile za Ujenzi na Uchukuzi.

La kwanza katika hilo ni kuwa ahadi na utendaji wa Serikali ulikuwa umeamua kuwa Mikoa yote iunganishwe kwa barabara za kudumu. Sasa nadhani Mikoa yote imeshaunganishwa na barabara za kudumu isipokuwa Mkoa wa Morogoro haujaunganishwa Kusini kwa Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Lindi. Kwa hiyo, pia tunaiomba Serikali kuwa itusaidie kuunganisha Morogoro na Ruvuma na Lindi. Hivi sasa ukitaka kutoka Songea ingekuwa ni mwendo wa saa sita kuja Dar es Salaam lakini inabidi upite Iringa uzunguke utokee Mikumi ndiyo uanzo safari ya kwenda Dar es Salaam ambapo ingekuwa kutoka Songea kuja Mikumi ni mwendo mfupi na ungefika Dar es Salaam mapema zaidi. Kwa hiyo, ni ombi maalum kabla hawajamaliza kipindi hicho cha Awamu ya Tatu angalau tusaidiwe barabara hiyo ya kuunganisha Morogoro na Songea. Wananchi wameanza kuunganisha Malinye na Kitanda upande wa mbili wa Songea Namtumbo, lakini wanahitaji *push* zaidi kwa upande wa Serikali ili tuweze kupata barabara ya heshima na tufanye iwe *shortcut*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jimbo la Peramiho nasikitika kusema kwamba kwa muda mrefu naongelea habari ya barabara ya Songea kwenda Mitumoni na daraja lake la kwenda Msumbiji. Tulipewa na Waingereza mwaka 1996 daraja na fedha za kuchonga barabara hiyo, lakini kwa bahati mbaya walikuwa bado hawajamaliza mazungumzo Tanzania na Msumbiji daraja liliazimwa au lilikopwa na Serikali na likapelekwa Maragalasi. Lakini kwa mimi niliyefuatilia daraja hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliniahidi kuwa itakapokuwa hali iko sawa tutaweka daraja lingine. Lakini mpaka leo mwaka huu kama unakwisha vile na ni mwaka wa 10 tangu mwaka 1996 mpaka leo siku zinakwisha na mimi naogopa kuwa walioniahidi wataondoka madarakani

wataniacha kwenye mataa kabla sijawapelekea wapiga kura wangu hilo daraja wala barabara. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba wafanye hima tupate daraja hilo mwaka huu, wapi watapata fedha nadhani zipo tu wanapoweza kukopa ni chache. Jitihada katika Mtwara *Development Corridor* wameiweka kama *Unit Bridge number two* kutokana na hiyo wanayoijenga sasa. Hiyo ni *Unit Bridge two* tufanye bidii watuunganishe barabara hiyo ili tuweze kwenda upande huo. Msumbiji wenzetu wameishajenga barabara yao na wameishajenga majengo ya Uhamiaji na *forodha* na kila kitu tumebakii sisi na biashara pale inazidi kukua kila siku kwa vile wao Msumbiji wanategemea hasa Tanzania kwa mazao yao mengi sana wanayotumia kule ya viwanda na hata ya chakula wanachukua upande wetu.

Kwa hiyo, tunaomba tutengenezewa hiyo barabara na tuwekewe daraja hilo ambalo walilazima watujengee jipyaa.

Mheshimiwa Spika, lingine kubwa nililotaka kuchangia ni Mtwara *Development Corridor*. Mtwara *Development Corridor* ni mradi mkubwa kabambe na kwa kweli tungeutilia nguvu Wizara zote au Serikali nzima na sisi Waheshimiwa Wabunge tuufanye uwe Mradi Mkuu *Mega Project* na wapo wengi wanaotaka kusaidia kwa kutoa fedha, lakini hawataki miradi midogo ya *Dollars* milioni 100, *Dollar* milioni 50 wanataka wanaita *Mega Project* bilioni kadhaa *Dollars*.

Kwa hiyo, pale nadhani tunaweza tukatengeneza Mtwara kwa kuweka Mchuchuma Mkaa pamoja na umeme wake, Liganga, Chuma pamoja madini mengine ya *Vaneleum tinedium*.

Mheshimiwa Spika, halafu tukaja Mtwara tukajenga Bandari ya kuchukua meli kubwa za tani 1,000 na kwenda mbele. Halafu ikajengwa reli ya umeme pia toka Mtwara mpaka Manda ikaunganika hapo na hivyo tukaweza kuwa na *Mega Project* ambayo hatutakuwa na shida kutafuta soko la umeme wa Mchuchuma ikawa soko linapatikana hapo tu tukiamua kulivalia njuga suala hilo.

Kwa hiyo, hilo naona tulifanyie kazi Serikali yote siyo Wizara chache au watu wachache na sisi Waheshimiwa Wabunge tuwe mstari wa mbele kuhimiza.

Mheshimiwa Spika, lingine nataka kuongelea ni Sekta ya Maji, tunashukuru sana kwa upande wa Serikali kwa Awamu zote moja, mbili na ya tatu kwa Ruvuma tuna maji karibu katika Wilaya zote bado tu sehemu ndogo na kwa upande wa Jimbo langu nina tatizo la vijiji vichache tu na hasa ni kijiji kimoja ambacho ni Kijiji Mji Peramiho yenye we tunahitaji maji ya uhakika. Fedha wanazohitaji kumalizia *Project* yao ni kama milioni 300. Sasa milioni 300 nina uhakika Wizara haitashindwa kupata hizo fedha ni kama *Dollar* 300,000. Kwa hiyo, tunaweza kupata hizo tukamaliza tatizo la maji Peramiho na tukaweka pia maji katika vijiji vitatu, vinne vilivyobaki vingine, Maweso, Lilondo na Matetereka. Kwa upande wa maji zaidi ni shukrani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa simu nayo pia ni tatizo, lakini tumepata tunaweza kusikilizana katika Jimbo nzima isipokuwa upande wa Kaskazini wa Jimbo hilo na Kijiji anachotoka Mbunge ambacho ni Kijiji Mji nacho pia hakijapata huduma ya simu bado. Kwa hiyo, naomba upande wa simu Mheshimiwa Prof. Mark Mwандосya aweze kutufikiria kabla hajarudisha funguo zake alizopewa anifungie angalau simu hizo na mimi niweze kuongea na Ulimwengu kutoka kijiji kwangu siyo lazima nije Dar es Salaam tu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ni hilo la wananchi waliofanya kazi kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mimi nadhani fedha ziliuju na Serikali yetu ilikubali kwamba ziliuju ila tu zilitumika kwa *priorities* nyingine. Suala rahisi nadhani ni kujua *dollar* ziliuju ngapi au *pounds* ngapi na tujaribu kutafuta hizo *pounds* au *dollars* tuwalipe wale watu wanaostahili kuliko kuanza kufanya mahesabu. Kwanza, kuchelewa kuwalipa, halafu pili, kuchelewa kufanya mahesabu kama tutumie *exchange rate* ya mwaka 1977 au ya mwaka 2007. Nafuu tuwachukulie zile *dollar* Serikali iziazime mahali sidhani kama ni milioni nyingi. Serikali iazime hizo *dollar* iwalipe wale watu kabla ya Serikali yetu ya Awamu ya Tatu haijaondoka madarakani. Hilo lingekuwa la maana kuliko kufanya vinginevyo na tukianza kubadilisha 1977 *dollars* yake ilikuwa shilingi chache sana. Lakini leo ukimlipa *dollar* zake yule bwana ataridhika na itakuwa *dollar* 1,000 kwa *dollar* yake akawa na *dollar* zake 20 anajua kwamba ana shilingi 20,000/=. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja na ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. (*Makofit*)

**SPIKA:** Sasa nitawaita wale ninaowaona humu Bungeni nao ni hawa wafuatao:- Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Frank Maghoba, Mheshimiwa Ali Machano Mussa na Leonard Shango. Nitawaita kwa mpangilio huo, kwa hiyo mjiandae hivyo. Namwita Mheshimiwa Anne Makinda.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha na ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na wenzangu kama walivyosema naomba nitoe salamu zangu za rambirambi kwa familia ya mwenzetu ambaye ametuacha hivi karibuni marehemu Abu Kiwanga, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba nitumie nafasi hii kwanza kabisa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Njombe Kusini ambao mwaka 1995 walinchagua kuwa Mbunge wao na mwaka 2000 pia wakanichagua kuwa Mbunge wao. Napenda kusema kwamba nina nia tena ya kugombea mwaka 2005. Katika kipindi hiki cha miaka 10 wananchi wa Jimbo la Njombe Kusini wameonyesha ujasiri mkubwa sana kwa kunichagua mimi Mbunge Mwanamke kuwa Mbunge wao kinyume na ambavyo watu wengi wanafikiria kwamba watu wa kule kwetu wanabagua wanawake lakini mimi walinchagua, wakanipa heshima na mpaka leo naendelea kuwatumikia kama Mbunge wao. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru kwa namna ya pekee tulipoanza mwaka 1995 shule za msingi zilikuwa hakuna na nyingine zilikuwa zimejengwa kwa matope au matofali ya udongo na ninavyozungumza hivi sasa shule zote za msingi wananchi wamezibomoa zile za zamani wamejenga nyingine mpya tena tuliwahi hata kabla ya MMEM, wao walianza hata kabla ya MMEM na wameendelea kujenga. Shule zote za msingi 62 katika Jimbo langu. Tunashukuru MMEM pia imekuja kutusaidia kukamilisha yale majengo ingawa bado tunaomba msaada zaidi ili itakapomalizika MMEM majengo hayo yote yawe yamekamilika na nyumba za walimu zimejengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia mwezi Aprili, tumefungua katika Jimbo letu Shule za Sekondari mpya tano katika Jimbo langu, wamejenga wananchi kwa nguvu zao na hivi sasa wanaendelea kujenga na ninawaomba tuendelee hivyo hivyo. Kwa sababu elimu ndiyo ufunguo wa maisha yetu bila elimu hatuwezi kufanya jambo lolote, hatuwezi kufanya biashara, hatuwezi kujihudumia kiafya, hatuwezi kuwasiliana na watu wengi. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa kutambua kwamba elimu ni msingi mkubwa sana kwa maendeleo ya mtu ye yote na moyo huo naomba uendelee wasikate tamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo tunaishukuru pia Serikali katika kipindi hiki tumeweza kupata maji asilimia kubwa sana pale Mjini Njombe. Hivi mwezi Juni, mwaka huu asilimia 75 ya wakazi wa Mji wa Njombe watakuwa na maji na maji safi. Tatizo letu pale sasa mkakati wa maji taka bado haujakuwa wazi. Kwa hiyo, nadhani hili suala Serikali itatusaidia kwa sababu jinsi tunavyozidi kupata maji safi ndivyo tunavyozidi kupata matatizo ya maji taka. Kwa hiyo, nadhani katika kipindi kijacho naomba tena Serikali iungane na sisi tuweze kushughulikia tatizo la maji taka pale Mjini Njombe.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo maji tumeanza kuyapeleka vijijini, maandiko mbalimbali ya maji na *survey* mbalimbali zimefanywa, lakini bado mchango katika maji vijijini siyo mzuri sana, lakini wananchi wameishatoa fedha zao kutengeneza maandiko ya maji katika vijiji. Kwa hiyo, naomba sana Serikali itakapoingiza utaratibu wake wa *Basket Fund* katika maeneo mbalimbali wakati naukubali utaratibu huo, lakini tusipoangalia utaratibu wa *Basket Fund* unaweza ukawa na matatizo hasa ikiwa utaratibu wake wa kugawana zile fedha kama siyo wazi unaweza pia ukaleta matatizo. Hii *Basket Fund* iko katika eneo la Afya, *Basket Fund* kwenye Maji na barabara sasa hivi wamesema ni *Basket Fund* na katika maeneo mengi mengine. Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema sisi wenyewe ndiyo tumewambia watuletee fedha halafu tugawane vipi. Mimi nakubaliana sana na mambo hayo, lakini tuwe na utaratibu ambao pengine Bunge hili lingekuwa linashiriki kwanza katika kutengeneza utaratibu wenyewe na pia katika kugawana zile fedha ama sivyo nchi itagawanyika katika walioendelea na wasiondelea kama ambavyo inafanana sasa hivi. Mimi ninaomba sana tuweze kuangalia.

Mheshimiwa Spika, nikiwa nasema hayo, nachukua pia nafasi ya kuwapongeza Mawaziri wetu hawa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Waziri Basil Mramba kwa kazi kubwa ambazo wamezifanya katika miaka hii mitano ama kumi kuanzia Mheshimiwa Rais alivyoshika madaraka. Kweli nchi yetu imekuwa ni nchi yenyе maendeleo makubwa ambapo watu wengi wanatuonea wivu. Wanatuonea wivu sana, Waheshimiwa Wabunge mlinichagua kuwa Mbunge wa *SADC* na juzi tumetoka huko mpaka wanasema nyinyi Tanzania imekuwaje mbona kila kitu chenu kinakwenda vizuri na wakati huo tulikuwa tunatengeneza mkakati wa kufanya maandamano rasmi ya kuomba nchi hizi *G 8* wanavyokutana mwezi ujao Scotland kuomba wawafutie nchi maskini madeni mia kwa mia. Sasa kabla hatujafanya hivyo tumeishafutiwa madeni mia kwa mia angalau yale ya *multilateral* kama Benki ya Dunia, *IMF* na ile ya *Africa Development Bank* ni heshima sana kwa nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu atakayeondoka madarakani atakumbukwa kwa mambo makubwa kama haya ni makubwa sana haya mambo. Mnajua watu wengi wanapenda kumbeza, kuna mtu mmoja alisema mtakumbuka Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa nini, wakasema watamkumbuka eti kwa mauaji yaliyotokea Pemba, hivi ni kitu cha kumkumbuka kwani yeze alikwenda kule. Lakini mambo aliyofanya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa dunia nzima inaona Tanzania ni nchi pekee. Kwa hiyo, kufutiwa madeni yeze peke yake asingeweza kufanya kama si hao wasaidizi wake. Kwa hiyo, lazima kwa kweli Tanzania tuseme ukweli uzalendo jamani lazima uwepo. Maana kama tunakosa uzalendo tunajinyonyoa wenyewe manyoya yetu hivi hivi uzalendo uwepo mambo makubwa yametendeka Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais na ameanzisha mikakati ambayo mingine imeanza vizuri kama huu wa *TASAF* ni wazo lake na ni mradi ambao uko chini ya usimamizi wake. Ameanzisha na mwingine huu watu wanasema MKURABITA ambapo mimi nipewa heshima ya kuwa Mwenyekiti wake. Mpango huo nao tunaendelea ku-*design* ni mkubwa sana na kama tutafanikiwa

tena itakuwa ni *mile stone* nyingine kubwa kabisa kwa Watanzania. Kwa sababu MKURABITA inavyozungumza kwa hii kinadharia. Hivi sasa tunahangaika na bilioni 4 Tanzania shilingi bajeti hii, lakini mali ambazo Watanzania wanazo katika Mikoa 10 tu ambayo tumeifanya utafiti wake ambayo haiko kwenye hesabu yoyote ni mali ambayo unayo tu, lakini haina faida kwako inasemekana ni sawa na bilioni 12 U\$ ambalo imelala tu wakati sisi tunahangaika huku, una nyumba kubwa huwezi kuitumia kukopea kitu chochote maana iko kwenye kiwanja kisichopimwa na una shamba lako ulirithi kwa baba yako na babu zako huko, lakini lipo tu pori halina kazi kwako wala kwa mtu yeoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo MKURABITA inajaribu kuangalia hivyo vitu vyote vipewe uhai viweze kutumika ili wananchi waweze kukopeshwa uwe na mali yako ambayo unaoweza kuitumia kuendeleza maisha yako na huku mali inabakia ya kwako. Kwa hiyo, ameanzisha hii haija-*take off*, lakini tutahakikisha kwamba lina *take off* kusudi Watanzania wote watambua nafasi yao katika nchi hii. Siyo kwamba fedha zinaletwa tu na Serikali, nyingi unazo wewe mwenyewe unazifungia umekaa. Kwa hiyo, mradi huu nao upo na tutaufanya kazi vizuri na tutaueleza taratibu kusudi mtu mmoja mmoja aelewae nafasi yake ni nini katika uchumi wa nchi hii na afanye nini. Ni nafasi ya kila mmoja wetu na kila mtu hapa ana nafasi ya kuleta maendeleo ya nchi hii, kila mtu ana nafasi isipokuwa hatujatambua nafasi zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna siku moja nilikuwa namtania Makamu Mwenyekiti wa CCM, nikamwambia wewe nyumba yako unayokaa pale uenda haina thamani sasa hivi, akasema kwa namna gani, nikamwambia hati yako uliipata miaka mingapi, akasema ni hati ya miaka 33 iliyopita, imepita haikubadilishwa ile hati kwa hiyo haina kazi ile hati na ni nyingi sana hizo. Kwa hiyo, ombi langu Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kwamba mradi ambao umeanzishwa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi wa kupima maeneo yasiyopimwa kama pale Manzese na katika maeneo mengine ya Mbozi na mahali pengine wangepewa fedha. Wapewe fedha waendeleze ila kazi ya kupima iendelee katika maeneo mbalimbali. Sasa hivi wamewafundisha wataalam katika Mkoo wa Mbeya, wamewafundisha wataalam katika Mkoo wa Iringa, lakini kwa sababu hawana fedha wamenyamaza hawafanyi kitu. Unajua elimu isipotumika inapwaya baadaye inakuwa haina maana inachunjuka. Kwa hiyo, naomba sana Waziri wa Fedha ile kazi ilioanzishwa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kupima maeneo ambayo ni *squatter*, tafadhali Mheshimiwa Waziri wa Fedha toa fedha kusudi wale waendelee hivyo tuone mfano wake halafu twende katika maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, moja ambalo siwezi kumaliza kuongea bila kulisemea nikushukuru utoaji wa mbolea kwa kupitia ruzuku kwa njia ya *transport* ambayo Serikali imeifanya huu utakuwa ni mwaka tatu. Zoezi hilo Wizara ya Kilimo na Chakula kaka yangu Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala na Waziri Charles Keenja wamesumbuka sana katika miaka hii miwili kujaribu kuweka utaratibu ambao unaeleweka. Mimi nawapongeza mwaka wa kwanza ulikuwa mbaya sana, mwaka jana ukawa mzuri kidogo nafikiri tunaweza kufanya vizuri zaidi. Mimi tatizo langu ni kwamba wakati Serikali inatoa ruzuku kwenye usafirishaji wa mbolea kiasi fulani lililotokea ni kwamba mbolea hizi zingine zimetoka kwenye maeneo ambapo zinahitajika zimekwenda mpaka Malawi.

Mheshimiwa Spika, halafu walifikia kipindi fulani wakatangaza wale ma-*agent* wao kwamba mbolea ya ruzuku imekwisha sasa tunaingia mbolea ya kawaida. Sasa hapa ndipo ninapofikiria Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji mbolea ukitoa nyingine inasafirishwa na Serikali na nyingine haisafirishwi na Serikali utajuaje mbolea iliyosafirishwa na Serikali ni ipi na ambayo haikusafirishwa na Serikali ni ipi? Hapa ndiyo kuna utata tukiweza kuondoa utata huu mimi nadhani utaratibu wetu wa kusambaza mbolea ni mzuri na utata huu tuuondoe kama tutaaumua mbolea zote ziwe zinapewa ruzuku kusafirishwa na Serikali basi tufanye hivyo ama sivyo tunasababisha mbolea isiende kwa wananchi ihamishwe kutoka kwa wananchi ipelekwe kama ilivyopelekwa Malawi kwa sababu wanasingizia kama ni mbolea yao ambayo haina ruzuku. Huwezi kutofautisha mbolea iliyopewa ruzuku na ambayo haikupewa ruzuku siyo rahisi kuitofautisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nafikiri ni suala ambalo tungelifanyia kazi kwa kweli utaratibu huu ni mzuri ila tatizo lake ni hilo tunasababisha rushwa, tunasababisha wizi, tunasababisha udanganyifu na tunasababisha wafanyabiashara baadhi wajitajirishe zaidi kuliko ambavyo walivyo. Maana wameficha mbolea hii hii halafu wanatangaza tarehe fulani kwamba mbolea ya ruzuku ilikwisha mwezi uliopita, sasa mnunue mbolea nyingine. Sasa wananchi wanashangaa.

Mheshimiwa Spika, ukichukua Wilaya kama ya kwangu tunalima mwaka mzima, sasa ukitupa mbolea kwa ajili ya mwezi Novemba, Desemba na Januari, halafu unasema imekwisha kwa kweli haujafanya kitu na hao wanaficha hiyo mbolea wanajua kipindi kingine wakulima watahitaji. Mbolea inatoka kwenye shilingi 14,000/= inafika mpaka shilingi 30,000 kwa mfuko kwa hiyo inakuwa tatizo kubwa. Hili nafikiri tulifanyie kazi vizuri nadhani nikisema hivyo mnanielewa. Hamwezi kutofautisha mbolea yenye ruzuku na isiyo na ruzuku kwa sababu hazina alama hilo ndiyo tatizo letu kama mkiweza kufanya hilo, utaratibu wa kusambaza mbolea kupitia ruzuku utakuwa mzuri sana siwezi kusemea maeneo ambayo siyafahamu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niwashukuru na niwapongeze Mawaziri wote wawili na niwatakie kila la kheri huko wanakokwenda wakachaguliwe warudi tena ili waweze kuendelea na ujenzi wa Taifa letu. Ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)



**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Na mimi kwanza nianze kwa kutoa rambirambi zangu za dhati na za wananchi wote wa Jimbo la Ukonga kwa wananchi na familia ya marehemu Abu Kiwanga, Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi ya pili, kwa kweli kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Benjamin William Mkapa kwa kazi kubwa anayoifanya katika kukuza na kuendesha nchi hii kiasi cha kufikia hatua ya kufutiwa madeni kama ambavyo imeshaelezwa. Kwa kweli yeye na Serikali yake wamefanya kazi kubwa sana na hata wanaobeza nadhani na wenyewe wanaelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nategemea kwamba fedha hizo ambazo zitatokana na unafuu utakaopatikana kutokana na kusamehewa madeni kama ambavyo Serikali imeeleza fedha hizi zitaelekezwa kwenye eneo kwa kweli la kukuza zaidi uchumi na kuondoa umaskini na ingekuwa basi kwa sababu zinajulikana kwamba fedha karibu bilioni 288 kama sijakosea tutakuwa tumeziokoa mwaka huu, basi maeneo hayo ambayo yataelekezwa kwa kutumia fedha hizi Bunge hili lipewe angalau taarifa tuweze kuona ni maeneo gani hayo.

Bado tunao muda kabla ya Mkutano huu wa Bajeti haujaisha basi tuletewe maeneo hayo tuyachambue na tuone kama ni sawasawa kama ambavyo tunagawa fedha zingine kwenye maeneo kadhaa na hizi fedha tuweze kuelewa zinakwenda wapi.

Mheshimiwa Spika, kwa mahesabu yangu mwaka huu tulitegemea tulipe madeni ya shilingi bilioni 528 sasa kama tumeamehewa bilioni 288 ina maana chini ya nusu tutalipa kama asilimia 45, yaani bilioni 240 ndiyo zitalipwa sasa kwa mpango ule ambao ulikuwa umewekwa, kwa maana hiyo zaidi ya nusu ya mikopo ya kulipa mwaka huu imesamehewa. Sasa ni vyema tukaelekeza hizo fedha kunakotakiwa.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kweli kwa bajeti nzuri na hii bajeti nasema ni nzuri kwa sababu kama ilivyoelezwa asilimia 50 imeelekezwa kwenye mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Sasa wapinzani wanabeza hii bajeti wakisema kwamba ni bajeti ya kisiasa si kweli hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kama kuna kitu cha kisiasa ni hayo maneno yao ya kubea bajeti ndiyo ya kisiasa, lakini bajeti siyo ya kisiasa, bajeti imelenga kwa kweli kukuza uchumi na kuondoa umaskini haikuongeza kodi za kero, imeacha kodi nyingi kama zilivyokuwa na kuongeza maeneo machache ambayo hayawezi kwa kweli kuathiri uchumi au vipato vya watu wa chini na huu ndio mpango ambao kwa kweli tumekuwa tukiusema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama nilivyosema nchi yetu imekuza uchumi wake. Uchumi wa jumla *Macro-Economics* kama ambavyo tunasema imekuwa kwa kiwango ambacho kinaridhisha sana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia takwimu zinaonyesha kwamba kwa wastani uchumi wa nchi za Afrika iwe ni Afrika nzima au Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, uchumi ulikua kwa mwaka jana 2004 ulikua kwa wastani wa asilimia 5.1.

Mheshimiwa Spika, sisi uchumi wetu ulikua kwa asilimia 6.7 sasa tuko juu ya wastani kwa kiwango kikubwa na hili lazima tulipongeze. Na imetokana na kuweza kuboresha mapato ya Serikali na mapato ya Serikali yameboreshwa kutokana na sera nzuri za kodi, sera nzuri za uwekezaji na kadhalika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, na vilevile Serikali imeendelea kupata misaada na hiyo misamaha ambayo tunaizungumza. Kwa hiyo, imetumia fedha hizi kuboresha uchumi wake na kuboresha huduma za jamii na kwa hiyo tuone kwamba huduma kama za afya, maji, barabara na elimu zimeboreshwa kutokana na uchumi kukua.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Ukonga ambao wao wanajua wako zaidi ya 700,000 wamekuwa mashahidi wa uboreshaji wa huduma za afya na huduma za maji ingawaje bado kuna matatizo ya maji, huduma za barabara na hasa huduma ya elimu au Sekta ya Elimu.

Nilipochaguliwa kuwa Mbunge pale kulikuwa na shule 26 za Serikali za msingi katika Jimbo la Ukonga, tumeongeza shule 48, sasa hivi tuna shule 74 katika Jimbo lile. Zaidi ya asilimia 150, sasa ni moja tu ya eneo kuonyesha kwamba Serikali hii imefanya kazi kubwa katika miaka mitano iliyopita. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa kisekta umekua na tunaelezwa na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji kwenye Sekta Kilimo, Utalii, uzalishaji, biashara na kadhalika kumekuwepo na kukua kwa sekta hizi.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na ukuaji huu bado tunahitaji kuendelea kuweka mkazo katika sekta hizi kwa sababu ukuaji wake bado ile *potential*, uwezo wa sekta hizi kukua zaidi upo. Utalii kwa mfano bado tunao uwezo wa kuboresha utalii zaidi na tukawa hatuwezi kulinganishwa na nchi yoyote hata katika Afrika kama tukiweka mikakati sawasawa kwenye sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na kukua huko kwa uchumi hii *Macro Economics* kweli kama ambavyo inasemwa zile faida hazijamfikia sawasawa mwananchi mmoja mmoja na hili ni jambo la kawaida na si la kushangaza kwamba mtu ushangae kwa nini uchumi umekua, lakini wananchi hawajafaidika, ni jambo ambalo ni lazima litokee hivyo.

Lazima kwanza uchumi ukue wa nchi kwa ujumla ile *Macro Economics* na baada ya hapo sasa ndipo uweze kupata manufaa ya kukua kwa uchumi na manufaa hayo sasa yaende kwa wananchi mmoja mmoja.

Kwa hiyo, ni mchakato, ni *process* ambayo ni lazima katika nchi yoyote, hakuna nchi inayoanza kwa kuwawezesha wananchi wao kuwa na kipato chao kama uchumi wa nchi yenyewe haujakua.

Mheshimiwa Spika, uchumi tumeuona umekua, sasa lazima tujielekeze katika kukuza kipato cha wananchi wa kawaida. Katika hili, wananchi hatuwezi kuilalamikia Serikali kwa sababu wadau ni Serikali na wananchi. Kwa kweli wananchi mimi nadhani wanayo nafasi kubwa zaidi hata kuliko Serikali katika nchi. Serikali kwa sasa kazi yake kubwa katika kuinua kipato cha wananchi ni kuweka mazingira mazuri na kutoa fursa za kuwawezesha wananchi kuinua vipato vyao. Lakini kwa upande mwingine ni wananchi ambao wana jukumu kubwa na kazi kubwa inayotakiwa kufanya. Ni kufanya kazi kwa bidii.

Watanzania katika hili hatujaweza kufika viwango vinavyotakiwa vyta kufanya kazi kwa bidii katika sekta yoyote ile, iwe ni ofisini au mashambani, viwandani, kwenye sekta ya kujiajiri bado wananchi kama sisi wenyewe lazima tujielekeze kufanya kazi kwa bidii. Sio kufanya kazi kwa bidii tu, kwanza uwe na elimu inayotakiwa, uwe mbunifu na ujifunze kuwekeza na hapa tunakuwa na upungufu mkubwa sana, kuwekeza kwenye sekta za uzalishaji lakini nyingine ni kuweka akiba suala ambalo limewashinda sana Watanzania. Tunashindwa kuweka akiba bila ya kujua kwamba kuweka akiba ndilo jambo ambalo linaweza likatukomboa.

Mheshimiwa Spika, haya mazingira ya kutoa fursa na kuwezesha kuinua kipato na kuondoa umaskini wa Mtanzania, mimi naweza nikasema kuna maeneo kama sita nitayaeleza ambayo naamini tukiweka bidii, Serikali na wananchi, huu mpango wa MKUKUTA tutaweza kuufanikisha na huko ndiko tunakotaka tujielekeze. Mpango wa MKUKUTA kwa kweli kwa kiasi kikubwa unalenga katika masuala ya umaskini na ukosefu wa ajira na vitu viwili hivi umaskini na ukosefu wa ajira ni pacha, unapotoa kimoja umeondoa kingine. Huwezi kuondoa umaskini kama hakuna ajira.

Ajira inapokuwepo, umaskini unaondoka, ndiyo maana yake. Ajira inabidi tuirolewe. Ajira sio ya kuajiriwa na kupata mshahara mwisho wa mwezi, ajira ni pamoja na wewe mwenyewe kujiajiri na kupata kipato chako. Uwe unajilipa wewe mshahara sio mwisho wa mwezi tu, lakini kila siku, kila wiki, kila mwezi na kila mwaka ndiyo ajira. Sasa ni mambo gani haya! Nadhani lazima tujielekeze katika kuondoa umaskini na kuleta ajira.

Ukiacha kuendeleza hiyo ambayo tumezungumza ya kuendelea kukuza uchumi katika sekta mbalimbali, lakini Elimu ya Ufundu na Elimu ya Juu ni muhimu sana. Kwa kweli nchi ambayo haina wataalamu, nchi ambayo haina watu wenye kujua ufundu, nchi ambayo haina watu waliobobe katika masuala mbalimbali ya kielimu, hatuwezi tukaondoa umaskini. Sasa tumeweza kufanya vizuri katika Sekta ya Elimu ya Msingi lakini Sekondari, *Vocational Training, Technical Education, Polytechnics* ilikuwa tuanzishe Vyuo kama hivi na *Universities* lazima tapanue elimu, hii, Watanzania walio wengi wawe na Elimu ya Ufundu na Elimu ya Juu wawe wataalamu. La sivyo, hii *labour mobility* ambayo tunaitela kutokana na kuingia katika Umoja wa Jumuiya ya Afrika

Mashariki utatuondo Watanzania. Ajira itakwenda kwa watu wa nje kwa sababu tutawaruhusu na wakimaliza watapeleka fedha kwao. Kwa hiyo ni lazima tuelekeze kwenye elimu.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni suala la pili. Kweli ukuaji wa kilimo umeonyesha hatua nzuri kutoka asilimia nne mpaka sita mwaka jana 2004. Lakini bado kilimo kinategemewa asilimia zaidi ya 80 ya Watanzania. Lakini kinachangia asilimia 46 ya pato la Taifa. Ina maana, bado uwiano si mzuri. Watu zaidi ya asilimia 80 wanategemea kilimo lakini kinachangia *GDP* kwa asilimia 46 tu. Sasa tuache kusingizia tu hali ya hewa, tujaribu kujielekeza kwenye mambo ambayo yatakuza uchumi wa kilimo. Teknolojia katika kilimo tuzungumzie umwagiliaji maji katika kilimo, zana na pembejeo za kilimo na uwekezaji mkubwa wa kilimo, lakini wakati huo huo, bila ya kusahau kilimo kidogo cha *peasant*.

Kwa hiyo, je, tunauvutiaje uwekezaji katika kilimo. Lakini kubwa ni *agro-processing*, lazima tuwe na viwanda na hivi vinu vya kusindika mazao na je, tumeweka kama sera ya kodi? Kwa mfano, tumewekaje vivutio? Mimi nadhani kwa mfano wawekezaji katika viwanda vya kusindika mazao wangeondolewa kodi karibu zote na hasa wanapokuwa ni wazalendo, ndio wanataka kuwekeza kwenye kilimo.

Sasa hivi wanasema kwamba tunazalisha tusichokula na tunakula tusichozalisha, inatokana na kutowekeza katika Sekta ya Viwanda vya Mazao ya Kilimo. Lakini kilimo vile vile cha umwagiliaji na kilimo kikubwa. Tunazungumzia mradi wa *Stigler's Gorge* tutaupanua lini? Tunaona kwamba huu mpango au mradi huu ni mkubwa sana una gharama kubwa, lakini ni karne gani gharama zitapungua za kuingia kwenye mradi huu? Mradi huu ni mkubwa, utakomboa nchi hii kwa kilimo kwa maji na kwa kweli katika uchumi wetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, lakini la tatu ukiacha kilimo, viwanda na uzalishaji ambayo inaendana na kuuza mazao nje ya nchi, kote huku ni muhimu tukaweka mkazo. Tumekuwa na mkazo sasa hivi ya maduka wala haya na Machinga pale kwangu Ukonga na Dar es Salaam kwa ujumla hatutafika mbali kwa vijana wetu kuuza bidhaa barabarani kama hatukuzingatia kwamba viwanda vianzishwe na uzalishaji ukue kwa nguvu.

Mheshimiwa Spika, lingine la nne ni huu mpango wa MKURABITA ambao Mheshimiwa amezungumzia hapa sasa hivi. Huu Mkakati wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge katika nchi hii, tuuvekee mkazo mkubwa. Lakini hii itasaidia kama tutawekeza zaidi, kama tutaangalia namna gani vyombo vya mikopo vinaboreshwaa, namna gani elimu ya kuwekeza na elimu ya mikopo inatolewa kwa wananchi wetu na kurasimisha hizo mali walizonazo. Ni muhimu sana kuliangalia hilo kwa kuwa litawezesha kuondoa umaskini kule kwenye Jimbo langu la Ukonga, Vingunguti, Kiwalani na Buguruni. Kama tukirasimisha nyumba za wale wananchi zaidi ya laki nne walioko kwenye Jimbo langu ambao wana nyumba ambazo hazina hati, tutakuwa tumeondoa umaskini kwa kiasi kikubwa sana kwenye Jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Spika, la tano, nataka kuzungumzia katika suala zima la kuhakikisha kwamba tunakuza uchumi ni hili la ushirikiano wa kibashara na nchi za Afrika na wale ambao tuko nao kwenye ukanda mmoja. Tunao mpango wa *East African Community* kupitia mpango wa *SADC* na mpango wa Afrika wa *NEPAD*. Sasa ni namna gani tunachukua hizo fursa? Sasa hivi tumeweka mikakati mikubwa tu na miradi mikubwa ambayo tumeiweka kule lakini tunaifuutiliae ili iweze kunufaisha wananchi wetu?

Mheshimiwa Spika, la mwisho la sita ambalo nadhani ni muhimu ni kuondoa upotevu ambao tunaupata katika matumizi ya Serikali na hasa katika suala zima la kutekeleza miradi. Tunayo *capacity* ndogo bado kwenye Serikali na hasa Serikali za Mitaa. Hapo ndiyo ilikuwa mwisho. Naunga mkono hoja hii. Ahsante. (*Makofî*)

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme ahsante sana kwa kuniona.

Kama jambo la kawaida, nami nitoe pole kwa wananchi wa Kilombero waliofiwa na Mbunge wao na Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, sitakuwa nimetenda haki bila ya kusema, huu ni mwaka wangu wa 10 ndani ya Bunge hili na sasa tunaingia katika kipindi kingine cha kwenda kuomba nafasi tena ya kurudi katika ukumbi wako na kuzungumza mambo ya bajeti kama haya. Naomba kabisa wananchi wa Bariadi niwatoe ile hofu waliyokuwa wameshaanza kutangaziwa na watu ambao wanajifikiria kwamba wao ndio wanawenza kuwa wawakilishi zaidi, kwamba Mbunge wa Bariadi Magharibi ambaye ni mimi hapa eti nakwenda kugombea sijui Temeke, sijui nakwenda kutafuta *Ph.D.* nakwenda wapi, mimi nipo na nitakuwa mgombea na nitakuwa Mbunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka kumi, tumeshuhudia bajeti hapa ndani ya Bunge. Nataka tu nifute jambo moja ambalo watu wengi wamekuwa wanazungumza humu kama Kambi ya Upinzani. Inasema, bajeti yote hii ni mufilisi, bajeti haina chochote! Hatujasema hivyo. Tunacho sema ni katika maeneo ambayo hata Wabunge wengine wameyaona kwamba yanahitaji kuwekewa *emphasis* na kuyaweka sawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengi tu ambayo tungependa tuyazungumze kwamba bajeti inapanda toka trilioni moja miaka ya nyuma tukaenda trilioni mbili, tatu na leo tuko trilioni nne. Lakini ukiangalia bajeti yenyewe, trilioni nne hiyo haiendani na kukua kwa pesa inayotengwa kwa ajili ya maendeleo. Nilitaka niseme la kwanza hilo.

Kwanza pamoja na bajeti nzuri ambayo tunaweza tukaisifu, tukaipamba, tukaiimbia nyimbo zote nzuri, lakini tuwe na wazo, tubadilishe mtazamo wetu, kwamba bajeti yote inayotokea *at least* asilimia kubwa zaidi iende kwa ajili ya maendeleo. Ukiangalia, chukua *figure* moja katika bajeti nzima mfano *salaries*. Ile mishahara uki-compare na posho ambazo zinatolewa kwa ajili ya kikundi fulani tu cha watumishi wa Serikali, posho zimekuwa ni kubwa zaidi kuliko mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nafikiria labda hapo tungekuwa na wazo la kufikiria namna gani tuongeze mishahara ya watumishi wa Serikali iwe mikubwa na wapate *incentive* ya kufanya kazi na mwisho kabisa ukiongeza mishahara hiyo kuwa mikubwa ili pensheni yao iweze kuwa kubwa kuliko kuwaongeza posho kikundi tu cha watu wachache. Hizo ndizo kasoro ambazo ziko kwenye bajeti ambazo wote tunatakiwa tuzione namna gani ziboreshe ili watu wengine waweze kufaidika kule mbele ya safari.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Msemaji wa Upinzani amezungumza kwamba hii bajeti labda ingeweza hata ikapunguza ule utegemezi kama sehemu nyine ambazo bado hazijaguswa na zenyewe zingeweza kuingizwa katika kuongeza pato. Moja, amezungumzia juu ya uvuvi kwamba kule baharini (*deep seas*) kuna meli ambazo zinavua samaki lakini zinatozwa leseni ya Dola 18,000 kwa mwaka. Akatoa *suggestion* tu kwamba katika nchi kama Somalia ambayo haina hata Serikali wanatoza Dola laki tatu kwa mwaka. Hiyo ingeweza *ku-brought back* katika *Revenue* ya Serikali, hivyo ingeweza kuongeza ikapunguza utegemezi ambao upo kwa sasa.

Kuna maeneo mengi tu, hata maeneo ya madini, labda kwa leo niwashukuru. Kwa mara ya kwanza nimezungumza muda mrefu sana! Ni nchi pekee ambayo katika machimbo yote tunawapa Wazungu (*Canadians*) Kahama Mines tumewapa dhahabu yote *hundred percent ownership* tukaanza kupunguza hata zile za Mwadui baada ya kutoza asilimia 25 tukaanza kuzipunguza zikabakia asilimia 12. Tunasema lazima katika machimbo yoyote yale *at least* asilimia 25 ibaki kwa ajili ya Watanzania. Hilo wamesema sasa wataweza kufikiria. Hicho ni kitu ambacho tunaweza kuwapongeza kwa mara ya kwanza kwamba *at least* wameanza kufikiria katika machimbo yote yale asilimia kubwa lazima ibaki ndani ya nchi iweze kusaidia maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kilimo ndio uti wa mgongo wa nchi hii. Mtu ambaye ni wa kuangaliwa zaidi katika kilimo ni mkulima mwenyewe ambaye *supervision* yake mwenyewe anajituma, haihitaji *supervisor* wa kumwambia wewe nenda ukalime. Hahitaji mtu yoyote isipokuwa ni kivutio cha kwamba ye ye akienda kulima pamba yake, bei ya pamba itakua na kwamba atakapouza pamba yake atalipwa kwa bei iliyopo siku hiyo hiyo na kwamba hatakopwa.

Mheshimiwa Spika, ni kitu cha kushangaza na kusikitisha sana kwamba mwaka jana kipindi kama hiki wanunuzi wa pamba walikaa pamoja wakaamu kushusha bei ya pamba kutoka Sh.300/= mpaka Sh.250/=. Waziri Mkuu amesimama ndani ya Bunge hili akatoa amri na takwimu akiagiza kwamba wale wakulima wote wa pamba waliopunjwa fedha zao warudishiwe Sh. 25/= au Sh.15/= zilizokuwa zimepunjwa.

Waheshimiwa Wabunge wameuliza maswali mengi ndani ya Bunge hili na wakapatata *assurance* kwamba zile fedha zote za wakulima wa pamba waliopunjwa watalipwa mara moja baada ya kufanya tathmini. Cha kushangaza, leo wakulima mpaka leo fedha yao waliopunjwa hawajalipwa. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, fedha iliyopatikana pale Bariadi, lazima nitoe mfano kwa Wilaya yangu. Wale wanunuzi wa pamba tumesema hawataweza kupewa leseni kama ile fedha ya mapunjo hawajalipwa wakulima. Walioweza kupeleka fedha kidogo pale kwa DC ndiyo amekuwa mlipaji wa ile fedha na yeye sasa ameanza kuangalia sura za watu, huyu ni *supporter* wa Chama cha Mapinduzi, huyu sijui ni nani, huyu ni rafiki yangu. Katika Kijiji ambacho kina watu 80, wamepunjwa, wanalipwa watu wanne tu. *This is quite unfair!* Nataka mkulima huyu alime na mwakani a-sustain kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa nchi hii. Sasa tumtendee haki.

Mimi nilikuwa nafikiria kwamba kama Serikali ilivyofanya kwa watumishi wa Afrika Mashariki ambayo pamoja na mimi ambayo sijalipwa, *intervention* inafaa pia itumike kwa wakulima wa pamba ambao mpaka leo hii hawajaweza kulipwa fedha zao za mapunjo.

Mheshimiwa Spika, ukitaka kukamua ng'ombe, lazima umbembeleze, umwekee majani yenyewe chumvi ili ajisikie aweze kutoa maziwa mengi, na mkulima ni hivyo hivyo! Kwa hiyo kama unataka kweli mkulima akulinde katika uchumi wako aendeleee kuwa ndio sekta kiongozi pia umjali katika bei yake ya pamba, bei yake ya kahawa na pia alipwe siku ile ile na hawa wanaopunja tuwachukulie hatua! Haya ni ya msingi ambayo Serikali inatakiwa kuyatilia maanani zaidi na kuhakikisha kwamba wakulima wetu ambao ndio wanatufanya tuwepo hapa wanatendewa haki wakati wote.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti tumeangalia maeneo ya kutoa umaskini, lakini labda nizungumzie tu juu ya elimu. Tulipoingia katika uchaguzi mwaka 2000 tulisema tungependa fedha yote inayopatikana kutoka kwenye *sources* zetu na sehemu nydingine na *savings* ziende kwenye elimu. Tukasema tunapenda Watanzania wasome Darasa la Kwanza mpaka Darasa la Saba bure. Hilo limeshatendeka. Lakini sasa katika hiyo imefanya Watanzania wengi zaidi wameingia Darasa la Kwanza. Watakapomaliza Darasa la Saba, hawana mahali pa kwenda.

Sasa *emphasis* na yenyewe tuielekeze katika Shule za Sekondari kwamba namba kubwa ya wanafunzi wanaomaliza Darasa la Saba, basi na wenyewe waende moja kwa moja Shule ya Sekondari na ikiwezekana na wenyewe wapewe hiyo fursa hiyo hiyo kwamba Darasa la Kwanza mpaka Darasa la XII wasome bure. Itakuwa ni kitu cha ajabu, unatengeneza watoto wengi wa Darasa la Saba halafu unawaacha tu Mitaani. Lakini hiyo iende moja kwa moja mpaka Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi kulikuwepo na swali hapa la umaskini wa Tanzania kwamba pato letu ni Sh.1,000/= japokuwa Waziri alisema sio hivyo. Lakini ukisoma katika vitabu, wanasema Mtanzania anaishi kwa Dola moja kwa siku ambayo ni sawa sawa na Sh.1,000/= hiyo hiyo, Sh.1,100/= au Sh.1,200/=. Sasa kama ndio pato lake na hali yake halisi, Mtanzania huyo, uwezo wake wa kusomesha mtoto wake mpaka Chuo Kikuu pia unapungua.

Kwa hiyo, Serikali ichukue *burden* ya namna hiyo, kwamba watoto wetu wanaomaliza Shule za Sekondari wasome Chuo Kikuu bure kama wengine ambavyo

tulivyoweza kusoma bure tutakuwa hatuwatendei haki kwamba sisi tumesoma bure wengine wasome kwa kulipa na huku tunajua kabisa kwamba baba zao ni maskini hawana fedha na hawana chochote cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kusema ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi, nami niweze kuchangia bajeti iliyoko mbele yetu.

Awali ya yote naomba nitoe pole kwa familia ya Mheshimiwa Marehemu Abu Towegale Kiwanga na Wapigakura wake kwa kifo chake.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niwapongeze viongozi waliochaguliwa kugombea nafasi za Urais katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Zanzibar kwa kupitia Chama cha Wananchi (*CUF*), Professa Lipumba. Lakini pia niwapongeze CCM kwa kumchagua Mheshimiwa Kikwete kugombea nafasi hiyo ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar. Vyama hivyo vimeonyesha nia nzuri kwa nchi yetu kwani kufanya hivyo mapema ni kuwafanya Watanzania wachague mbichi na mbivu za kuweza kuwasaidia maishani mwao. Nahimiza na wale ambao hawajafanya hivyo wafanye hivyo sasa ili Watanzania wajue cha kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mramba na Mheshimiwa Kigoda na hasa watalamu wao ambao wamewezesha bajeti hii kusomwa mbele yetu. Leo hii ningependa niwapigie debe wataalamu wa Wizara ya Fedha na Mipango kwamba waongezewe posho kwa kazi nzuri wanayoifanya kwani wamekuwa wakifanya kazi usiku na mchana wakati wengine tunasubiri kusomewa taarifa kama hizi. Kwa namna hiyo, hata Waziri wa Fedha na Manaibu wake wamekuwa hawapati kazi ya kusoma bajeti mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa mambo mengi tu, kwanza nikizingatia kwamba katika miaka mitano iliyopita Serikali imetoa kipaumbele katika kuboresha elimu hasa kwenye Shule ya Msingi. Naipongeza sana kwa kazi nzuri iliyofanyika kupitia Mradi wa *MMEM* ambao umeonyesha kweli kwamba tunakwenda mbele na sio kurudi nyuma.

Lakini pia naipongeza sana Serikali kwa sababu baada ya kugundua kwamba kuna majengo mengi ya Shule yamejengwa na kuna upungufu wa Walimu, hilo sasa naona linafanyiwa kazi kwa ajili ya Walimu wengine ili kuboresha elimu zaidi. Ila tu ni kwamba, katika suala la Sekondari, kama mnakumbuka matokeo ya mwaka uliopita kidogo, yameshuka kwa kulinganisha na kipindi cha nyuma na hii inaonyesha kwamba udhibiti sasa katika mitihani umekuwa mkubwa na kwamba mitihani sasa haivuji. Kwa waliofaulu mitihani mwaka huu wamefaulu kihalali na kupitia akili zao waliokuwa wamefundishwa na walimu zao.

Lakini cha msingi katika suala hilo ni kwamba naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza Walimu katika Shule za Sekondari, kwani sasa hivi watoto wengi wanafaulu lakini Shule zetu za Sekondari ni chache na Walimu pia ni wachache.

Kama tunadhani kwamba Watanzania hatufai au hatutoshi kufundisha Shule za Sekondari, basi tuajiri Walimu kutoka nchi za nje ili waje wafundishe watoto wetu na kuwawezesha kuingia Elimu ya Juu bila ubabaishaji.

Mheshimiwa Spika, mimi nachangia kidogo kidogo kwa sababu mengi wamechangia na wenzangu, lakini nitajaribu kuchangia vifungu vifungu. Pia, nije kwenye upande wa *TRA*. Nawapongeza sana *TRA* kwa kazi nzuri wanayoifanya kwani wameonyesha kwamba wakikaa vizuri na kufanya kazi kwa makini kama wanavyoifanya sasa, tunaweza kupata makusanyo makubwa zaidi kulingana na sasa hivi tunavyoifanya. Sasa hivi tunapata karibu Sh.145,000,000,000/= kwa mwezi kama sikosei. Kitu ambacho naomba ni kwamba waangalie, wageuze macho na masikio yao kwenye Bandari. Nina imani wakiboresha masuala ya pale Bandarini pato litakuwa kubwa zaidi. Kwa mfano pale gari likiingia ku-*clear* mizigo si chini ya siku 14 na zaidi. Sasa wakiondoa tatizo hilo, wateja watapatikana wengi pale kwenye Bandari ya Dar es Salaam. Sasa hivi wateja wengi wanakwenda Bandari ya Mombasa kwa sababu kule sana sana umechelewa ku-*clear* gari lako ni wiki moja na haizidi siku tatu na gharama zao ziko chini kidogo.

Sasa naamini kwamba kama kweli tutarekebisha suala hili mapato yetu yatakuwa makubwa zaidi kwa sababu tutapata wateja wengi zaidi. Wateja wengi wanakwenda Mombasa kwa sababu ya unafuu wa gharama za kule na pia wepesi wa kupata mizigo yao.

Kwa hiyo, nawaomba watu wa *TRA* waangalie suala hili na ikiwezekana waharakishe suala hili ili makusanyo yetu yaongezeke maradufu kama ambavyo tulitegemea katika Serikali yetu, kwa sababu usumbufu ambaao uko *long room* ni mkubwa sana. Tumepigia kelele sana kelele suala la *long room*, lakini bado naona linakuwa gumu. Sasa sielewi kuna tatizo gani. Haiwezekani wewe unaleta gari leo linakaa miezi miwili halafu wakati huo linakaa miezi miwili sio kosa lako wewe, bado zile gharama za kukaa Bandarini unatakiwa ulipe tena mwenyewe. Sasa hii ni tatizo.

Mimi nadhani hili suala lingeondoka na lingekuwa halipo kabisa na tungepata wateja wengi katika Bandari ya Dar es Salaam, lakini tunapoteza wateja kwa sababu suala hili hatujalipatia ufumbuzi wa msingi kabisa. Kwa hiyo, naomba wahusika, Mheshimiwa Mramba aangalie sana suala hili kwamba ikiwezekana, pale Bandarini na hasa *long room* wafanye marekebisho ili mambo haya yarekebishwe. Kwa sababu haiwezekani gari moja inakaa mwezi, siku 14 kitu ambacho kinatia aibu sana.

Bandari yetu ni kubwa. Leo watu wanakwenda Mombasa, kwa sababu gani waende Mombasa? Inafikia hata wageni wanapelekwa Mombasa ku-*clear* mizigo yao! Wageni kutoka nchi za nje ambaao wanakaa hapa Tanzania ambaao wana shughuli zao hapa Tanzania, wanasema kutokana na urasimu umekuwa mkubwa, Watanzania wanashauri ili mwondokane na usumbufu nendeni Mombasa kule mambo yenu mtafanikiwa. Kwa nini tufikie hatua hiyo? Mimi nadhani hakuna sababu ya kuonyesha kwenye sura ya nchi za nje kwamba Watanzania hawako makini katika suala hilo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa hilo, lakini pia niongeze katika suala la MKUKUTA. Naipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuanzisha suala la MKUKUTA.

Hili nadhani ni suala ambalo litakuwa ndilo la msingi katika kuondoa unyonge na umaskini ambao tunao kwa Watanzania hasa walioko Vijiji. MKUKUTA ni jambo ambalo sasa linaweza kutuwezesha wakulima na wananchi wa kawaida kufanikisha katika mambo yao hasa kilimo na biashara zao. Naamini kama MKUKUTA huu utasimamiwa vizuri, kwa kweli nina imani Watanzania wataondokana na suala la umaskini. Suala la MKUKUTA ni la muhimu, lakini katika suala hili pamoja na kwamba fedha zinapelekwa kule moja kwa moja, kuangaliwe wataalamu watakaoweza kusimamia suala hili bila kupoteza fedha ambazo tunatazamia kuzipeleka kule.

Mfano mzuri ni ule wa *TASAF*. *TASAF* walivyokuwa wanaleta fedha zao, zilikuwa zinasimamiwa na wanavijiji hao hao na kwe kweli kuna mafanikio makubwa sana ambayo nimyeaona na hasa kwenye Wilaya yangu ya Temeke na hususan Jimbo la Kigamboni. Tumepata mafanikio makubwa sana kupitia mradi wa *TASAF*. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Mkapa kwa sababu lile wazo la kusema tupeleke Temeke, nadhani limefika sehemu yake na sisi tumefanya vile ambavyo amekusudia. Kwa hiyo, naomba sana, hata suala la MKUKUTA liige mfano wa *TASAF* ambao sasa kuna mafanikio makubwa na sasa hivi kuna awamu ya pili nadhani kutokana na hali hiyo hiyo, hali itakuwa nzuri zaidi.

Pia niishukuru Serikali kwa kufuta ushuru wa mafuta ya ndege kwani hilo linaonyesha kwa kiasi gani Serikali inataka kuboresha maisha ya Watanzania na pia kuwafanya waweze kufanya shughuli zao bila matatizo. Lakini wasiwasi wangu ni kwamba, pamoja na kwamba ushuru huu umefutwa:- Je, Serikali itakuwa tayari kupunguza gharama za nauli za ndege hizo? Kwa sababu sasa hivi nauli ya kwenda Mwanza ni Sh. 165,000/= kama sikosei. Kwenda Kigoma ni Sh.190,000/= kama sikosei. Sasa kama ndivyo ndugu zangu wa Mikoa ya Magharibi naona wanapata taabu sana, Kigoma, Mwanza, Shinyanga, Zanzibar na Pemba.

Mimi naamini kwa kufuta ushuru wa mafuta ya ndege, sasa Serikali itaangalia uwezekano wa kupunguza zile gharama za nauli ili Watanzania ambao walikuwa hawana uwezo wa kupanda ndege wapande ndege, sasa wafaidi matunda ya nchi yao. Nina imani kabisa kwamba suala hili Mheshimiwa Mramba ataliangalia kwa undani kabisa. Nashukuru Serikali imefanya hivyo, lakini pia iangalie na jinsi ya kuendesha shughuli hizo baada ya kupunguziwa gharama za mafuta au kuondolewa gharama za mafuta ya ndege kwani kwa kufanya hivyo utakuwa umeboresha maisha ya Watanzania, nao wajidai kwa kupanda ndege angalau kidogo.

Mheshimiwa Spika, sasa nakuja kwenye shughuli zangu hasa kule Kigamboni, naanza na daraja. Katika mpango wa Waziri wa Mipango sijaona akizungumzia daraja na kama amezungumzia, basi mimi sikuangalia, labda macho yangu hayawezi kusoma vizuri. Lakini naamini kwamba sijaona akizungumzia daraja la Kigamboni ambalo kila mwaka najaribu kupigia kelele. Ni hivi karibuni Serikali imetua kifaa ambacho kinawenza kikaokoa watu wanapotaka kuzama na pantoni. Sasa inaonyesha ni kiasi gani tunahitaji kuwa na daraja badala ya kuwa na pantoni. Pantoni zile zilizoko pale zimechoka na *service* yake inahitaji gharama kubwa mno.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nimeshauri muda mrefu kwamba, kama daraja la Kigamboni litajengwa, nina imani Watanzania watakuwa tayari kulipia gharama ambazo hata kwenye pantoni wanalipa. Kwa maana hiyo, hata hela za kulipia hilo daraja zitafidiwa mapema sana. Leo hii kila kukicha pantoni imekwama, mara imepotea njia, mara imepoteza mwelekeo. Hii ni ku-*risk* maisha ya wananchi wangu wa Kigamboni.

Kwa hiyo, naomba sana suala hili Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha waliangalie kwa undani. Daraja la Kigamboni kwanza ni daraja ambalo linaweza kutuinulia uchumi katika Jiji la Dar es Salaam na Taifa kwa ujumla. Suala la daraja lisiwekwe kama suala la kisiasa, liwe ni suala ambalo linatakiwa tulitekeleze kwa nia ya kuwakomboa Watanzania na kuwaongezea kipato chao. Kwa kufanya hivyo, utakuwa umewakoa Watanzania ambao wanaishi Kigamboni na wanachi wengine wanaotaka kujenga ndani ya Jimbo la Kigamboni. Naomba sana Waziri Mramba aangalie suala hili na pia aliwekee umuhimu.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye suala la barabara ya Kilwa, naomba Mheshimiwa Mramba nimkaribishe kwangu akae siku moja tu, halafu kesho yake tuamke wote kwenda kazini, aone adha ambayo ipo kwenye barabara hiyo ya Kilwa kutoka Mbagala kuja mpaka Uhasibu. Kuna adha kubwa! Leo hii barabara hiyo ambayo tulikuwa tunaitegemea imebomoka, pale karibu na daraja la Wachina, limebomoka kabisa. Kwa hiyo ina maana kuna kanafasi kadogo kakupitisha magari ya kwenda huku na huku, kwa hiyo kunakuwa na msongamano, yaani ukiamka saa kumi na moja Ofisini unafika saa tatu. Sasa hiyo ni tatizo. Hii barabara ni kiungo kikubwa kwenda kwenye daraja la Mheshimiwa Mkapa kule, sasa kama barabara hii itakuwa haipitiki hata daraja hilo halina maana kwa sababu magari yatakuwa hayaendi kule. Kwa hiyo, naomba hili suala liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye suala la viwanda. Suala la viwanda nadhani juzi Serikali imefutiwa madeni na katika Bajeti ya Mheshimiwa Mramba, viwanda havikupewa kipaumbele sana katika kuimarisha viwanda. Mimi naomba sana, kwa kuwa sasa tumefutiwa madeni, japo sijui kama itachukua muda gani kupewa hizo pesa au kama tulikuwa tunazo kwa ajili ya kulipa madeni sasa kwa sababu zipo, naomba sasa nguvu kidogo zielekezwe kwenye viwanda, kwa sababu viwanda vinavyokuwepo vinasaidia kupatikana ajira kwa wingi kwa Watanzania na pia vinasaidia kuinua uchumi kwa haraka haraka sana. Kwa hiyo, naomba kwamba pesa hiyo inayofutiwa madeni iingie kwenye viwanda.

Juzi Mwenyekiti wa Shirikisho la Viwanda, Mheshimiwa Mengi, alizungumzia suala hili kwamba ameona Bajeti lakini suala halikutiliwa mkazo katika viwanda. Kwa hiyo, naunga mkono kwa hii hoja ya Mheshimiwa Leonard Mengi kwamba, kweli viwanda vinatakiwa viangaliwe kwa sababu zinaleta pato kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika viwanda hivyo hivyo nawashauri na nawaomba viongozi ambao wanasmamia viwanda vyao waache kunyanyasa wafanyakazi ambao wanazalisha kwenye viwanda vyao hivyo. Juzi juzi hapa kulikuwa na mtifaruku mkubwa *KTM*. Lakini namshukuru Mkurugenzi wa Kiwanda alikubali

kwamba alifanya makosa hayo kwa sababu alikuwa anashauriwa vibaya na viongozi wake wa chini na amekiri hilo na ndio maana baada ya kufunga kiwanda akafungua baada ya kufanya mazungumzo mimi na Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na Viongozi wengine kwamba amekubali makosa hayo na kwamba sasa atarekebisha na kwamba hata madai yote ya wafanyakazi yatakuwa tayari kuyafanya marekebisho. Kwa sababu alikuwa anashauriwa vibaya na viongozi wake.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tulimwomba kwamba katika kiwanda kile kuundwe Chama cha Wafanyakazi ambacho kinaweza kupeleka malalamiko yake Serikalini na kwingineko ili wale wananchi wanaofanya kazi mle wasizulumiwe haki zao au mambo kadhaa. Ilifikia mfanyakazi anaomba likizo ananyimwa au mtu amefiwa akienda kwenye msiba akirudi anakatwa mshahara wa siku mbili kwa sababu tu amekwenda kwenye msiba ambao ni wa ndugu yake. Sasa hiyo ni unyanyasaji mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi sikutegemea kama mtu anapata mabilioni ya pesa kwenye viwanda pamoja kwamba Serikali inafanikiwa katika hilo, lakini sasa kwa nini wafanyakazi wanyanyaswe? Nina imani kwamba wafanyakazi wale wanaozalisha walitakiwa kuenziwa na kupewa hata posho. Imefikia sasa mwenye kiwanda anampa *uniform* mfanyakazi pamoja kwamba alijitetea, *uniform* hiyo anamkata mshahara mfanyakazi. Hivyo, mimi naamini kwamba mwenye kiwanda kutokana na mazingira ya kiwanda, pale kuna *chemical* nyingi inatakiwa upate *gloves*, upate *boots*, upate na *uniform* kwa ajili ya kufanya kazi mle ndani. Mle kiwandani kuna *chemical* ambazo ni kali. Ukishika yale maji bila *gloves* unachunika ngozi. Sasa leo unampa vifaa mfanyakazi halafu unamkata mshahara wake anaondoka na Sh.400/= mwisho wa mwezi au Sh.1,500/=, unategemea umemsaidia nini huyo mfanyakazi?! (*Makofi*)

Mimi nawaomba wenyе viwanda, namwomba Mheshimiwa Mengi kwamba, suala la wenyе viwanda aliangalie na ahakikishe kwamba anakaa nao kuhakikisha wafanyakazi wanapata haki zao inavyotakiwa wapate haki zao. Haiwezekani tukazalisha kwa wingi halafu wafanyakazi wananyanyaswa kwa sababu tu hawana pa kusemea. Tupo, wa kutuambia na wametuambia na nikayafanya kazi. Mimi nilikwenda pale Dar es Salaam nikahakikisha kwamba hilo suala linafanyiwa kazi na kiwanda kinafunguliwa na kinafanya kazi.

Mimi nakubali, naunga mkono Bajeti hii kwa sababu ni nzuri na inafaa kusimamiwa kwa uangalifu sana. Asante sana. (*Makofi*)

**MHE. ALI MACHANO MUSSA:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia hotuba iliyokuwepo mbele yetu. Kwanza kabla sijaanza kuchangia hotuba hii, kama kawaida, pamoja na kwamba pole zilizotolewa zimekuwa nyingi na mimi niungane na wenzangu kutoa pole kutokana na kifo cha Wabunge wenzetu Mheshimiwa Abu Kiwanga wa Jimbo la Kilombero na Mheshimiwa Hassan Diria wa Jimbo la Rahaleo, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pia kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tumbatu Zanzibar ningelipenda kuwapongeza Waheshimiwa wetu ambao wameteuliwa na Chama

chetu kugombea nyadhifa za juu katika Serikali yetu ambao ni Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Amani Abeid Karume. Nawapongeza sana na pia nahakikisha kwamba tumaini la vijana sasa limetimia na pia nina uhakika kwamba Chama chetu kwa utaratibu huu kitaendelea kushinda. Pia nisikosee kusema kwamba vijana matakwa yenu yametekelezwa kwa kuchaguliwa viongozi wanaofaa. Kwa hiyo na nyie m jitayarische kutupa kura ili tuhakikishe Chama chetu kimeshinda na mambo yenu mhakikishe yanatengenezwa vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia sina budi kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wawili ambao wametuletea hotuba zao hizi kwa umahiri kabisa nao ni Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Waziri Mramba Waziri wa Fedha, Manaibu wake wawili na Makatibu Wakuu na Maofisa wengine ambao wameshirikiana katika kutekeleza wajibu wao. Wakati nimesimama hapa nafikiri nia na madhumuni ni kuchangia hotuba hizi.

Kabla sijakwenda mbali, nisije nikasahau, niseme kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia na naunga mkono kwa maana nina uhakika inakidhi mahitaji ya wananchi. Kwa hiyo, hali hii hatuna budi niseme kwamba pamoja na kwamba kuna watu wanabeza hali hii, huo ni mchezo wa kawaida. Nasema, wao wamepotea njia, lakini sisi tunasema kwamba hotuba hizi ni nzuri na zitatufikisha mahali ambapo kuna mahitaji. Mimi kwa upande wangu nataka nichangie mambo mawili tu katika haya, lakini yatakuwa na sehemu nyingi nyingi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na kwamba nitakuwa ninayarejea kidogo yale ambayo Wabunge wenzangu wameyazungumzia, basi naomba uniwie radhi. Ni kwamba maneno unayajua ndio yale yale yaliyokuwepo duniani, isipokuwa mpangilio kidogo unakuwa unatofautiana. Mimi kwanza nataka niungane na Mheshimiwa Kissassi wa Jimbo la Dimani, kuizungumzia Bandari ya Zanzibar. Maana ya kusema hivi ni kwamba Waziri wa Fedha katika sehemu ambazo anategemea zitaiingizia pato Serikali ya Tanzania ni pamoja na ukusanyanyaji wa mapato yanayotokana na biashara zinazotokea Zanzibar.

Ukweli ulivyo ni kwamba, Bandari ya Zanzibar imeachwa katika hali ya kuwa inazidi kuperomoka ambayo kukosekana kwake mapato ya Tanzania yatakuwa nayo yana dosari. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliangalie hili kwa upande wake. Lakini hilo dogo, kubwa zaidi ni kwamba Bandari ile ina watu ambao walikuwa wanapata riziki na sasa hawapati tena. Kuna wananchi Mikoa mitatu ya Zanzibar kazi wanazozitegemea zipo, lakini pamoja na hayo wanategemea wengine kazi za kubeba mizigo, mizigo yenye ya Bandarini Zanzibar. Kama Bandari ile haifanyi kazi, tunategemea wananchi wale waendee wapi?

Hivi ninavyozungumza, wananchi wale ambao miaka mingi wamekaa pale kufanya kazi kabla mimi sijazaliwa wako pale kutwa wanahesabu magari ambayo yanapita njia. Watakaporudi Mitaani kwao jioni wakawaambie nini watoto wao? Sasa ukiachana na kwamba mapato hayapatikani, lakini pia wananchi ambao wanaishi katika

maeneo yale hususani wanaotoka Kaskazini Unguja, kama wale wa Tumbatu, Mkwajuni, Nungwi, Chaani ni watu ambao wanahitaji kuchukua mizigo Bandarini au kufanya kazi za Bandarini. Kukosa kwao kwa mapato, basi tuseme kwamba wananchi na watoto wao maisha yao yamo hatarini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuipa nguvu Bandari ya Zanzibar sio tu kukusanya mapato ya Tanzania, lakini pia kuondoa ukali wa maisha kwa wananchi baadhi ya wanaoishi katika Visiwa vya Zanzaibar. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri akalitazame hilo kwa jicho la huruma kabisa.

Meshimiwa Spika nikitoka sehemu hiyo, nafikiri nimezungumza kwa ufupi, inaoanekana itakuwa imeeleweka. Nafikiri sasa nielekee katika hali ya madeni, jambo la kujivunia kuwa Serikali yetu tayari imefutiwa madeni au inaendelea kufutiwa madeni. Lakini kama Serikali imeendelea kufutiwa madeni na sisi wenyewe Viongozi wa nchi hii tuna watu wanatutizama kwa macho mawili ambao ni wananchi wetu, haitakuwa jambo la busara kusikia kwamba wewe unadaiwa, umefutiwa madeni lakini unayodaiwa mengine ya humu ndani hutaki kuyalipa. Kiungwana kabisa ni kwamba ukidaiwa mdeni wako usimbabaishé kwamba kesho, kesho kutwa. Hebu tuone kwamba wananchi wetu wanaotudai tufanye busara za kuwalipa, tena wanadai pesa kidogo sana hawa.

Kwa bahati nzuri, maswali yanayoulizwa Bungeni yanajibiwa kwamba wanaodai pesa za Afrika Mashariki wanategemea kulipwa, kila mwaka maneno ndiyo hayo hayo. Watalipwa, watalipwa! Nashukuru kwa hili kwamba uamuzi ni kwamba watalipwa.

Lakini kilio kingine kipo kwa wananchi wengine ambao wanafanya kazi Serikalini, bado nao wanaendelea kudai. Hebu tujaribu kupunguza mambo mengine na tuone kwamba kuna umuhimu wa wadai hawa wanaotudai tuwalipe na tukate mara moja suala hili tufanye mambo mengine. Kwa masikitiko makubwa ni kwamba nina masuala kama matano ambayo nimeuliza Wizara ya Mambo ya Ndani na nimepata majibu kwamba askari Polisi, Magereza na Uhamiaji wanategemea kulipwa. Hili naliacha mpaka wakati wa Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani. Lakini nimwombe Waziri wa Fedha, vijana wetu ambao tunawategemea watulinde, wana mshahara mdogo, lakini mshahara mdogo huo huo bado nao wanadai, mtu ana kitu kidogo naye anadai, kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, wanajeshi kwa ujumla, lakini hasa hasa madeni ambayo wanadai Askari Polisi, ni mengi sana ambayo ni madogo lakini katika vifungu mbalimbali. Kuna Maaskari wanadai pesa ambazo Wizara ya Mambo ya Ndani haiwezi kuzipata isipokuwa zitoke Wizara ya Fedha. Wastaifu waliofanya kazi miaka kadhaa wanadai, Askari wanadai posho zao ambazo juzi pia tarehe 21 niliuliza nikaambiwa tayari wanalipwa, wanadai posho za vyeo, wanadai posho za mavazi kwa wale Maaskari wa *CID*. Sasa posho kama hizi au madeni kama haya madogo madogo, kwanini Mheshimiwa Waziri, hii Wizara ya Mambo ya Ndani asiifanyie maarifa akalipa mara moja tukabakiwa na mambo mengine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimeuliza swali moja ambalo kwa bahati mbaya halikupata muda wa kuulizwa. Ni kwamba, tulikuwa tunahitaji Maaskari wapige kura siku yao moja na siku nyingine waingie katika hali ya Uchaguzi wakiwa katika hali nzuri na tunawategemea Maaskari kutulinda sisi na mali zetu, lakini hali zao za maisha ni mbaya. Sasa kama hali zao za maisha ni mbaya na bado wanaendelea kudai, watatulinda vi? Kwa hiyo, mimi naomba tuwaangalie kwa jicho la huruma, walipwe posho hizi wasiwe na sababu ili watulinde kwa hali nzuri. Mheshimiwa Waziri kuhusu suala la deni nafikiri niishie hapo, inaonekana kidogo nitakuwa nimeeleweka.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, kabla ya muda haujanipita nizungumzie suala la mchango wa afya. Utaratibu wa mchango wa afya hata mimi nauafiki na ni mzuri, ukweli unatekelezeka. Lakini kuna wananchi ambao wako Zanzibar wanafanya Serikali ya Muungano, jambo la kusikitisha, mwaka mzima mtu hajakwenda hospitali, anapokwenda anaandikiwa dawa za Sh. 1,500/= bado zinakuwa ni matatizo kuweza kutibiwa. Hili tatizo nafikiri lioneokane. Hebu tufanye maarifa mazuri wasiwe na masikitiko madogo madogo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu wana nia safi, lakini mambo madogo madogo tuyaoondoe. Nafikiri *massage* hii imefika. Lakini pia nizunguzie kuhusu habari ya mapato ambayo wanakusanya baadhi ya Mashirika ya Serikali, kwa mfano kama hawa watu wa Shirika la Maji au Umeme wana matatizo ya kutuletea *bill* na wanakwambia kwamba Komputa tayari imekuandikia wewe kwamba unadaiwa Sh.50,000/= kwa mwezi, nyumba yenye we umekuja Bungeni wiki moja na nusu. (*Makofii*)

Kama wiki moja na nusu unadaiwa Sh.58,000/= au Sh.40,000/=? Umetumia maji kiasi gani? Lakini *bill* kama ikija unaambiwa wewe ulipe tu komputa imeandika. Sasa haya makusanyo mengine yanayopatikana, Serikali iangalie wananchi wetu, tunawaumiza. Kwa sababu kama unahitaji maji utakwenda wapi? Kama unahitaji umeme umeletewa *bill* utakwenda wapi? Hebu niambieni! Sasa ni vizuri tuangalie, tusione tu kwamba tunakusanya makusanyo mengi, mapato Serikalini yanapatikana lakini mengine yanatokana katika hali ambazo si halali.

Mheshimiwa Spika kwa hilo naomba tuliangalie, lakini pia sikupenda kengele inililie. Kwa hiyo, niseme tu kwamba hotuba hii ni nzuri, inafaa kuungwa mkono na vizuri tuone kwamba wanachi wetu hatuna budi kwamba mkae na m jitayarische kwa mafanikio mema. Naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niongee katika hoja hizi mbili ambazo ziko mbele yetu.

Kwanza, kabla sijaongea lolote, nami naungana na wenzangu kutoa rambirambi kwa familia na wananchi wa Kilombero kwa kufiwa na mpendwa wao Mheshimiwa Abu Kiwanga.

Pili, naungana na wenzangu pia kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuteuliwa kuwa mgombea Urais kupitia CCM. Pia, nawapongeza

Mheshimiwa Amani Abeid Karume na Dr. Shein kwa nafasi zao walizoteuliwa na CCM katika uchaguzi wa mwaka huu. Labda siyo vibaya pia nikiwapongeza wale wenzetu walio teuliwa upande wa Upinzani kuwasindikiza wenzetu wa CCM. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuwapongeza Mawaziri wetu walio tuletea hoja hizi mbili, Mheshimiwa Waziri Basil Mramba kwa hoja ya Wizara ya Fedha na Mheshimiwa Dr. Kigoda kwa Mipango na Ubinafsishaji.

Labda kabla sijaanza, naomba tu kusema hapa au kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kutambua sifa zangu na uzoefu wangu, uzoefu pekee mwaka 2000 na kunipa ridhaa yao ya kuwawakilisha Bungeni.

Mimi hapa nilikuja na ajenda zangu na niwakumbushe tu kuwa, kwa miaka 25 mimi nilitumikia Benki ya Afrika. Siyo kama Karani, lakini kama *professional staff*. Katika utumishi wangu, nikawa na uhusiano wa kikazi na nchi zote za Afrika. Kwa hiyo, nchi za Afrika ndiyo zili kuwa kama Tarafa zangu. Nina uhakika ni wachache waliopo hapa Bungeni ambao wana uzoefu kama huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuitia kwako nawaomba Waheshimiwa Mawaziri hawa wawili wasinielewe vibaya nitakapoziongelea hoja hizi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hotuba za Bajeti ni hotuba muhimu katika uhai mzima wa Bunge, kwa hiyo unapoleta Bajeti mbele ya Bunge, maana yake unaleta miongozo na maelekezo. Sasa ukweli uko hapo hapo kuwa unaweza ukaleta takwimu ambazo zinaonyesha uchumi umekua, sekta mbali mbali zimekua, zinaendelea kukua, lakini mimi ningeomba tukubaliane vizuri kuwa, kukua kwa uchumi, kigezo ambacho kinachonyesha uchumi unakua, iwe kukua kwa ubora wa maisha kwa wananchi hasa walio wa kawaida.

Nianze na hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ameongelea kuwa mwaka huu matumizi yamekadiriwa kuwa trilioni nne na katika hizo, kuna trilioni moja itakuwa kwa miradi ya maendeleo. Mimi nilitaka kujua kuwa tangu nilipoingia hapa, ni agenda yangu kuwa kilimo cha sasa au uchumi wa sasa katika sekta mbali mbali hasa kilimo, unahitaji mageuzi au Mapinduzi. Lakini ningemwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuwa katika hizo fedha ambazo zitakwenda kwa miradi ya maendeleo. Je, kilimo kimetengewa kiasi gani?

Pili, Mheshimiwa ametueleza jinsi Tanzania ilivyomepata sifa kwa kujua kuongea na Wahisani. Hii kama kwa kweli ni sifa ya Taifa letu, ningemwomba basi, kama ikiwezekana Mheshimiwa Waziri awapigie magoti Wahisani, awaombe fedha za kutosha kusudi tuanzishe katika Bajeti hii jinsi ya kuleta mapinduzi kwenye kilimo. Naongelea hivyo kwa sababu suala zima la kilimo tunaendelea kuongelea kilimo kinachotegemea mvua. (*Makofî*)

Tatu, katika jamii zetu, umaskini unaendelea kuongezeka, katika hali halisi na tunaona unaendelea kuongezeka kwa kasi sana. Kwa hiyo, suala hili la kupunguza

umaskini, itategemea sana kwa sababu asilimia 70 au 80 ya watu wetu ni wakulima kama hali zao hazitaboreshwa.

Kuhusu hoja ya pili ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, mimi nilitegemea, kwa sababu ya kuona umuhimu wa kilimo na lazima sasa tuone umuhimu wa kuleta mapinduzi katika Sekta ya Kilimo. Yeye angeongelea zaidi jinsi ya kuhakikisha kuwa kuna hatua kwa hatua sasa kilimo cha kumwagilia kianze na kuvuna maji ya mvua. Huwezi kumwagilia kilimo kama huna maji. Kilimo ni shughuli ambayo ni lazima ifanywe kwa wakati wote. Kama mwenye duka anakuwa na kazi yake kwa mwaka mzima, miezi 12, kwa nini kilimo chetu kitegemee miezi mitatu ya msimu wa mvua na baada ya hapo wakulima wetu waweke majembe uvunguni?

Ufumbuzi wa hilo ni suala la kuvuna maji. Hii *concept* kwa nini ina kigugumizi? Dunia yote sasa haitegemei suala la mvua. Njaa imetutinga kwa miaka mitatu mfululizo, karibu nchi nzima imaguswa na njaa au upungufu wa chakula. Ukweli ni kuwa, suala hili ufumbuzi wake upo katika uwezo wetu.

Siku moja mwaka jana nikakutana na rafiki yangu ambaye sasa ni Naibu Waziri wa Kilimo wa Morocco, nikakutana naye Amstardam. Nikamwambia Bwana, Mheshimiwa, sisi kwetu tuna njaa sana kwa sababu hatukuvuna mazao ya kutosha kwa sababu ya ukame. Yeye akasema, "Sikuelewi." Nikamwambia hunielewi namna gani? Nimekueleza hivyo. Akasema, "Sikuelewi!" Nikajaribu kumweleza kwa kifaransa, nikasema (*Mon frere, dans mon pays de Tanzanie cette annee nous avion le problem des secheresse*). Lakini akasema ndiyo nilikuelewa, lakini sasa hivi unategemea nini? Morocco ikuelewe katika tatizo hilo?!

Akasema sisi Morocco tungepata mvua hata ndogo kama ya kwenu, mbona sisi tungefika mbali zaidi kuliko hapa? Sisi nchini Morocco hatuna mvua, lakini kilimo chetu ni cha miezi 12. Sisi tunatumia maji yatokayo chini ya ardhi, maji yatokayo milimani, barafu ikiyeyuka tunaivuna. Ninyi mnashindwa kuvuna maji ya mvua na nani atawahurumia kwamba mna njaa au mna ukame? Tatizo lenu Tanzania ni la kujitakia. Ufumbuzi wa tatizo hili upo ndani ya uwezo wenu. Sasa Mwaziri wetu hawaelewi hivyo? Hivi tutaendelea lini? Hivi njaa imetuttinga mwaka huu, mimi juzi nimepita kwenye Kata zangu kama nne hivi. Kidaru, Tuliya, Ntwike na Shelui, wananchi hawatavuna hata debe moja la mazao. Mwaka jana labda walivuna madebe mawili au matatu kila kaya. (*Makofî*)

Sasa nini tumejikita kuhakikisha mwaka ujao suala hili la njaa lisitukute? Tunaendelea kuona kama mambo yanakwenda sawa, hata hizi takwimu zinatolewa kuwa tani kiasi fulani, yaani tani 13,000 mwaka jana zilivunwa. Hii ni msimu mmoja:-, Je, ingekuwa misimu mitatu, tani ngapi zingevunwa?  $13,000 \times 3$ , ingekuwa mavuno kuzidi tani 39,000. Lakini suala hili tunaendelea nalo. Kilimo kinachotegemea mvua hakitatutafikisha popote. Umaskini wa wananchi wetu utapunguza tu kama Serikali itawajengea mazingira ya kundesha kilimo kwa mwaka mzima.

Katika Bajeti hii, wangeweka mambo sawa, kuwa tuna mipango ya kila Wilaya na kila Mkoa jinsi ya kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya kilimo. Suala la upatikanaji wa mvua ya kutosha halitabiriki, hali ya hewa sasa imevurugika na mvua hazitabiriki. Mvua zitaendelea kuwa ndogo mwaka hadi mwaka, lakini sisi hatujafanya lolote. Lakini mbona wenzetu kwenye nchi za majangwa hawana hata mvua ndogo na kama inatokea ni wiki moja au mwezi mmoja tu, lakini wanaendelea kulima kwa sababu ya kuzamia katika matumizi ya teknolojia ya kuvuna maji yatokayo chini ya ardhi.

Hivi teknolojia ya kuvuna maji haipo ndani ya uwezo wetu? Tunaongelea tu, lakini suala la kilimo cha kumwagilia kitaanza na kuvuna maji ya mvua *systematically*. Hapa Tanzania tuna maji mengi hivi, tuna mkataba gani na Bahari ya Hindi tunapoachia maji yanamwagika baharini?

Huko Zimbabwe Mito yao inapofika mipakani, kwa mfano Mto Limpopo unafika mpakani karibu na Afrika Kusini yanabaki matone tu. Maji yote yatakuwa yamevunwa. Sasa sisi tunaachia iwe Mito mikubwa, midogo, maji yanakwenda baharini. Halafu tunaawambia wananchi, jamani, mnaokaa kwenye mabonde mhame. Kwa nini mnayaogopa maji? Kwa nini msiyavune maji haya kabla hayajawatishia wananchi mabondeni? Hili suala la kuvuna maji, kitu gani ambacho mnakuwa na kigugumizi? Maji yale yakivunwa yatatumika kwa mambo mengi na yatabadilisha mazingira. Mimi nasema huu ni upungufu katika Bajeti hii kwa sababu tunataka tuwe na *systematic approach* ya kuvuna maji kusudi tutumie kwenye kubadilisha kilimo ambacho wananchi wanaweza kuwa kwenye shughuli za kuzalisha mazao wakati wote kwa miezi 12 ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nitoe pongezi kwa Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri inayoendelea nchi nzima ya kujenga barabara. Lakini ningeomba pia suala la barabara kuu ambazo zinazojengwa ni vizuri, lakini barabara pia zielekezwe kwenye maeneo ya uzalishaji, yaani *feeder roads* au *link roads*. Barabara hizi zimeachiwa Halmashauri ambazo hazina uwezo. Nashauri barabara za Vijijini zingechukuliwa na Serikali Kuu, yaani izijenge na baadaye Halmashauri izimiliki. Lakini sasa hivi unakuwa na barabara kuu inapita pale, lakini kufikisha mazao kwenye barabara hizi kupeleka sokoni hakuna barabara (*feeder roads*), mpaka yafikishwe na punda. Sasa hii ni kasoro kubwa pia. Hizi nguvu zetu sasa tuelekeze kwenye barabara zinazokwenda kwenye maeneo ya uizalishaji. Kwa hiyo, ningeomba kasoro hizi zirekebishwe katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, mimi ningeomba suala la umeme Vijijini litazamwe upya na wenzetu hawa wa *Net Group Solution*. Kwa kweli wapunguziwe (*they over lived their usefulness*). Sasa hivi umeme kupelekwa Vijijini, kasi imepungua sana, haipo tena, kwa sababu mbalimbali. Jukumu la kupeleka umeme Vijijini ni jukumu la Serikali na ningeomba sasa Serikali ione umuhimu. Hiyo ni nishati ambayo itasaidia sana katika maendeleo ya wananchi wetu Vijijini. Siyo tu suala la burudani, ni suala la nishati ya kutumia katika kazi za maendeleo.

Pia, ningeomba suala la wenzetu wa Afrika Mashariki ambao walistaafu, Serikali imesema itawalipa. Je, wale waliochukuliwa mbele ya haki, yaani waliokufa, familia zao zitalipwa? Wastaafu wengi wamengojea mpaka Mungu akawachukua. Sasa

ningeomba Serikali ihakikishe kuwa itafute familia za Marehemu zikalipwe, zimeachwa katika hali ngumu na mbaya sana. (*Makofi*)

Pia ningeomba kama ingewezekana Serikali ihakikishe kuwa suala la elimu liendane na hali halisi ya sasa. Sekondari nyingi Vijijini hazina umeme, hazifundishwi masomo ya kompyuta na hali halisi ya leo katika Ulimwengu, mwanafunzi lazima ajue kutumia kompyuta kusudi aendane na hali halisi ya dunia ya leo.

Mimi ningeomba Wizara ya Elimu ihakikishe kuwa mashule yote Vijijini ambayo umeme uko karibu, wapewe au wawanunuliwe jenereta za kuzalisha umeme kusudi vijana wetu walioko Vijijini pia wapewe vifaa hivi vya kompyuta wafundishwe, usiwe ubaguzi wa kufundisha masomo ya kompyuta kwa mashule ya Mijini tu.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, mimi ningeomba kusema tu kuwa nitaunga mkono kwa dhati kabisa hoja hizi mbili, lakini naomba watazame suala zima la mageuzi kwene kilimo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hizi mbili ambazo ni muhimu katika maandalizi yetu ya mwaka ujao. Kabla ya yote naomba nitoe salaam za rambirambi kwa familia za wenzetu waliotutangulia mbele ya haki Mheshimiwa Abu Kiwanga aliyekuwa Mbunge wa Kilombero na Mheshimiwa Ahmed Hassan Diria aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo na ambaye nimekaa naye miaka yote katika Kamati ya Mambo ya Nje. Tunaomba Mungu awape subira familia zao na aweke roho zao mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda niwapongeze ndugu zetu ambao wamechaguliwa kushika Bendera ya CCM katika kutafuta ugombea wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kule Zanzibar na vile vile Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein ambaye ni Mgombea Mwenza wa Mheshimiwa Kikwete. Tuna imani kwamba kwa kushika bendera hiyo tutapata kura za Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuwapongeza Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafishaji kwa kutuletea bajeti hii nzuri ambayo nafikiri kwamba ikitekelezwa tutasogea hatua moja mbele katika kutafuta maendeleo ya nchi yetu. Nawapongeza sana na ninaunga mkono hoja hizi mbili. Bajeti hii ni nzuri kwa sababu naona wameainisha miaka, bajeti imeonesha kwamba uchumi wa nchi yetu unakua mwaka baada ya mwaka. Hii ndiyo inatuonyesha kwamba utendaji wa kazi wa Wizara zilizokabidhiwa dhamana na watumishi wote walio katika Wizara hiyowanafanyakazi vizuri. Ombi langu kwao ni kwamba usimamizi vile vile uwe mzuri kwa sababu mara nydingine tunakata tamaa tunaposikia Wizara fulani watu wawili/watatu wamejichukulia bilioni kadhaa au milioni kadhaa ambayo ni mamilioni ya fedha.

Tunasikia matangazo lakini mara nyingi hatusikii hatua gani zimechukuliwa kwa watu wale waliojigawia vipande nya fedha bila bajeti ya Bunge hili. Fedha zilikotaka kwenda hazikwenda lakini hatusikii wamechukuliwa hatua gani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi naomba kwa jinsi walivyokazana kutafuta vyombo nya kuzuia wakwepaji wa kulipa kodi basi waweke vyombo vikali nya kuwachukulia hatua hawa wanaonyofoa bajeti ya wananchi na kutumia kwa manufaa yao wenyewe. Naomba wawe imara kabisa katika kazi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuomba Wizara hizo mbili, Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji, wameweke utaratibu wa mikopo kwa wananchi ili kuondoa MKUKUTA. Wanasema waweka vyombo ambavyo mimi naviafiki kabisa. Lakini mara nyingi vyombo hivi vinahudumia watu wale wale, wengine amba wanataka wahudumiwe amba mara nyingine ni maskini lakini wana utaalam ni maskini kwa mapato, lakini si maskini kwa utaalam wanavikosa kwa sababu hawana labda rehani au wengine hawakupita kwenye elimu ya kutengeneza miradi, wana elimu nyingine labda kama mwalimu wa shule kama mimi. (*Makofi*)

Sisi tunafundisha kufundisha mtoto hatufundishwi kuandika miradi. Sasa mimi mwalimu nataka kujitumbukiza nikapate mkopo ambavyo wameviweka kwa kuondoa umaskini unakuta kwamba makaratasu yale wanayopeleka hayaendani na vyombo nya ukopeshaji wa hizo benki. Sasa mimi ombi langu kwao naomba kwa heshima na taadhima kwenye vitengo nya kukopesha kuwe na vitengo nya kuelimisha wakopaji wasiozoea. (*Makofi*)

Mpaka sasa hivi mimi huwa nashangaa wakisema wananchi wamekopa, wananchi wako wapi, nani? Kama wananchi wale wale watano/kumi ndiyo mnaendelea kusifu kwa kweli inabidi iangaliwe. Mwanamke mpishi mzuri ni yule anayepika vitu vingi anajua kuvipika vyote vizuri. Anapika tu mlenda wa kwao, anajua kupika, anajua kupika. Sasa mlenda Wanyakyusa hawali mlenda, unajua kupika ukiweza kuchanganya vitu mbalimbali nya mlenda nya samaki, ngisi na mambo kama hayo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango na Ubinafsishaji, wanapojisifu uwekezaji umekwenda vizuri, wawekezaji wangapi Wamachinga mmewekeza katika mashamba? Wale vijana mngegeweke katika mashamba ambayo yalikuwa ya *NAFCO* mkawafundisha, mkawapa kazi tungepata uzalishaji na mapato ya ndani yanaongezeka na wewe ungeongeza pia bajeti yako kwa kuona vijana wengi wameongezeka. Hizi hesabu tunazozifanya kwa watu wachache naomba ziendane sana na uzalendo zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *VETA* wapo wanafundisha mambo mengi ya useremara wa vitu mbalimbali ni viyi hawa vijana tuisiwakusanye tuwaweke katika vikundi vyetu na wafundishwe pale pale kwenye *VETA*? Nafikiri tutaweza kuondoa umaskini (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kijana hapa jirani alikuwa amesifu kwamba vijana sasa wataangaliwa mimi nasema wanaweza kuangaliwa kwa maneno nilikuwa namwambia hapa chini, lakini inawezekana kwa matendo wasiangaliwe. Sasa mimi naomba sana

vijana hawa waangaliwe wafundishwe kwa sababu hata vijana wenyewe hawajui, kijana anayebba godoro hakupita pale kwenye masomo atawezaje kwenda kukopa kwenye vyombo hivi mnavyotuwekea, *SACCOS* anakopesha Sh.50,000/=, Sh.60,000/=?

Tunaomba wafundishwe waweze kutumia hata fedha nyingi. Juhudi tunaiona lakini iongezeke zaidi. Jinsi *TRA* inavyojitahidi kuziba mianya ya wakwepaji kodi basi na Wizara zetu hizi ya Uwekezaji ijitahidi kuvua wale ambao hawajaingizwa kwenye uwekezaji. Wanasema wana nini, sasa mtu kama hana nini wewe uliyenacho si umpe? Serikali ndiyo inacho ina kila kitu kwa nini wasiwawekee utaratibu wa kuweza kukopa ili waondoe huo umaskini wa MKUKUTA, vinginevyo tutakuwa na maneno tu, MKUKUTA, maneno magumu magumu, lakini yasitooe umaskini kwa sababu Watanzania tumesifika sana kwa kuunda Kiswahili si wanasema Kiswahili kilizaliwa Tanzania kikakulia Kenya, kikafia Uganda. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, bajeti ya kuondoa umaskini wanapokwenda sasa tukiipitisha maana tunajua kwa vyovyote vile tutaitipisha hatuna ugomvi na Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, tuna ugomvi na utendaji tupitishe hapa na zikafanye kazi kwa watu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie kidogo suala la Kiwanja cha Ndege Bukoba, Bukoba tuna kiwanja cha ndege kidogo hatuna kiwanja kikubwa, Kiwanja cha Ndege Bukoba, ndege hazitui wakati wa mvua. Mwezi uliopita watu wengi walikuwa wanashinda Mwanza na kulala Mwanza kwa sababu tope limejaa kwenye kiwanja kwa hiyo, ndege haziwezi kutua. Ninajua hata Waziri mmoja alinaswa na mimi nilfurahi sana tena alikuwa jirani, sikwenda kumsalimu niliogopa kwamba nitamwambia bwana umeona, alikwama kwa sababu tope lilikuwa haliruhusu ndege zitue.

Kwa hiyo, usafirishaji wa anga uende sambamba na usafirishaji wa magari na meli na mambo ya treni. Tuangalia kwamba vitu hivi vinakwenda sambamba ili watu wetu wapate amani, kwa sababu kama ndugu yako amekaa Mwanza ndege haitui na wewe uko Bukoba au Karagwe n.k ni jambo ambalo linaleta mtafaruku wa moyo hata pengine usiweze kuzalisha mali na kuongeza uchumi katika Wizara ya Fedha. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba kiwanja hicho kiangaliwe kabisa. Hata pamoja na kwamba kuna mawazo ya kujenga kiwanja kingine cha ndege kikubwa Mkajunguti lakini hicho tutachukua muda mrefu, sasa hiki kitengenezwe kwa wakati ambao mawazo ya kujenga kiwanja kingine, Mkajunguti unatayarishwa hiki kiwe kama cha *first aid*, kiweze kufanya kazi ambayo baadaye kitatumika hata kama tukiwa na *international airport* kule Mkajunguti na mimi nafikiri *international airport*, Uganda iko *international airport* pale jirani Mwanza itachukua mizigo gani, basi kitengenezwa hiki kiwanja ambacho ndiyo kitakuwa kinasafirisha wafanyabiashara kwenda kushughulika na shughuli nyingine. Hili ni ombi langu ambalo ninaliweka mbele ya Wizara hii kwa nia yote ya moyo wangu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia juu ya ukopaji. Waswahili wanasema kukopa harusi kulipa matanga. Wakati Serikali yetu ilipokuwa na matatizo ilikopa fedha za wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, katika *sterling pound* miaka yote hiyo tumeshindwa kuwalipa na ni Serikali yetu ambayo tuna imani nayo. Mheshimiwa Rais, mwezi Mei alizungumza kwamba hataki kuondoka na madeni. Lakini katika bajeti hii tunaona kwamba kuna shilingi bilioni 50 nadhani ndizo ambazo zinatakiwa kuwalipa lakini ilikuwa bilioni 400 sasa hapa kama tumechukua sijui ni miaka mingapi tangu Afrika Afrika Mashariki waache kazi, fedha ziletwе kutoka Serikali ya Uingereza, mpaka leo hii tunapitisha bajeti hii walipwe hizo bilioni 50, itatuchukua miaka mingapi kulipa bilioni 350? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba tuwe na amani tuangalie kama mambo haya yangekuhusu wewe ungesema namna gani? Basi mimi naomba utaalam ule ule ambao mmetumia katika kukusanya kodi basi mtumie utaalam ule ule na dawa ile ile, ili muweze kupata fedha muwalipe watu hawa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, mtuondolee aibu kwa sababu aibu hii ni ya Serikali. Tunaumiza familia za watu wengine hata wanapigwa kupandishwe kwenye magari. Kwa bahati mbaya wale waliokuwa wanawapiga mmoja wao kapata laana kagongwa gari, hatujui Mungu alikasirika au alifurahi kwa sababu ametoka kuwapiga watu leo, kesho akagongwa na gari. Mambo haya si madogo katika nchi kama yetu yenye heshima kubwa duniani pote. Naomba wawalipe hawa wafanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mambo ya nishati tunaomba umeme vijiji. Lakini Wizara ya Nishati na Madini imeshindwa hata kupeleka umeme pale Bunju “A” na Bunju “B” kwa sababu eti hawana fedha. Mheshimiwa Basil Mramba, tunaomba uwaokoe watu hawa wapeleke umeme Bunju hapo na vijiji jirani na Dar es Salaam. Jimbo letu la Kawe tunaomba lipone, tafadhalii Mheshimiwa Mramba, peleka umeme kwa watu ambao walihidiwa. Kama wangkuwa hawakuahidiwa nisingesisitiza wala kujali kitu lakini wameahidiwa na Jimbo lile ni letu la CCM, tunaomba upeleke umeme pale, Jimbo tuzidi kulichukua. (*Makofi*)

Mwisho napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Mawaziri, katika uwekezaji. Kuna mashamba ambayo wananchi wanayahitaji. Ninaposema wananchi ni wale wananchi wa MKUKUTA mashamba yale ya *NARCO* wapeni wale wa MKUKUTA mliowaandalia MKUKUTA. Maana MKUKUTA hamkuandalia watu wengine kwa sababu MKUKUTA ndiyo wapiga kura wale, maana mimi sielewi huo MKUKUTA wenu, MKUKUTA mnaoita kuondoa umaskini, umaskini kwa MKUKUTA ndiyo wapiga kura, wengine wako pale pale katikati, wakati wa ukoloni pale pale, wakati wa uhuru pale pale, katikati. Tumegeuka wako pale pale katikati na ndiyo wanaopata mikopo mingi sana. Wako pale pale katikati na kupiga kura hatuwaoni sana wanakuwa pembeni.

Kwa hiyo, hawa wenzetu mnaopanga mipango tuone waziwazi kwamba MKUKUTA hawa mnawakukutua kweli au ni maneno kwenye vitabu ili dunia isome. Usimfurahishe wa nje kabla wa ndani hajafurahi.

Akina baba, kama mama hajasema karibu pole na kazi amani huna. Mpiga kura kama atachukia tupate wapi amani na sisi CCM tunataka tutawale mpaka mwisho wa

dunia? Tunataka tutawale Chama cha Mapinduzi, chama cha heshima kitawale mpaka mwisho wa dunia basi tunawaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji angalia MKUKUTA. (*MakofîKicheko*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki hautoshi kwa kumwita mchangiaji mwingine. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(*Saa 06.49 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia*)

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nitawataja watakaochangia jioni hii. Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, simwoni; Mheshimiwa Faki, simwoni; Mheshimiwa Bernard Membe, haonekani; Mheshimiwa Juma Kidunda, hayupo; Mheshimiwa Mayonga, hayupo; Mheshimiwa N'hunga, hayupo; Mheshimiwa Mwamoto, hayupo; Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi yupo. Mheshimiwa George Mlawa atafuatiwa na Mheshimiwa Mutungirehi halafu Mheshimiwa Dr. Zainab Gama.

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja hizi mbili ambazo zote naziunga mkono. (*Makofî*)

Kwanza kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kalenga ninaloliwakilisha, ningependa kutoa rambirambi zangu kwa familia ya Marehemu Abu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kilombero. Vile vile, naipongeza Serikali kwa kufutiwa madeni na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa wakati huu tunapojadili bajeti ya mwaka huu. Hii ni ishara ya wazi kwamba hali ya uchumi wetu inazidi kuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kwanza nichangie juu ya mambo mbalimbali ambayo tumeweza kufanikiwa kwa mipango mizuri ambayo imepitishwa hapa Bungeni na mpango ambao umezungumziwa katika hotuba zote za Mawaziri wawili ni Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kwamba kupata elimu bora ya msingi, halafu na Elimu ya Sekondari, inafanya vijana waweze kuwa waelewa katika enzi mpya inayoingia sasa ya utandawazi ambapo maisha yatazidi kuwa magumu sana kwa vijana wetu. Kwa hiyo, huko mbele watakaofanikiwa ni wale ambao ni wajanja na wenye nguvu, wanaita *survival of the fittest*.

Kwa hiyo, kwa sasa kama tunavyoendelea kupanga mambo yetu, tunaonyesha wazi kabisa kwamba elimu ndiyo zana ya msingi kwa ajili ya vijana wetu kujitetea na mazingira magumu, kujilinda, kujiendeza na hatimaye kuweza kuishi maisha yaliyo

bora na kwa kweli kwa sasa hivi ni kwamba wale vijana ambao watakuwa wamesoma vizuri Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari, hao ndiyo watakaofanikisha mpango wetu wa MKUKUTA. Mpango huu utafanikiwa ikiwa sehemu kubwa ya vijana wana elimu bora ya msingi na ya sekondari. Bila hivyo, hatuwezi kufanikiwa katika uchumi wetu       na       vile       vile       hatuwezi       kupunguza       umaskini.

Kwa hiyo, sasa hivi jinsi tunavyoendeleza elimu kwa nguvu hii, basi hali ya uchumi inakuwa nzuri. Ni kama alivyosema Mwandishi mmoja, yaani mkiwa kwenye mwendo au mchakato wa namna hii, anasema *moving from survival to stability, from stability to success, from success to significance*. Kwa hiyo, uchumi unazidi kuwa mkubwa, tunakuwa *significant* katika duru za kimataifa na ndiyo maana tumeweza hata kusamehewa madeni yote na Mashirika haya ya kifedha kupitia G8. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine ningependa nieleze jinsi sisi kwa upande wa Jimbo la Kalenga jinsi tulivyotafsiri MMES na kuitekeleza. Mwaka 2000 wakati naingia Bungeni kama Mbunge wa Jimbo la Kalenga, Jimbo letu lilikuwa na Shule mbili za Sekondari zilizojengwa na wananchi, Shule ya Sekondari ya Kalenga na Shule ya Sekondari ya Isimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya hapo tumeweza kuunganisha nguvu za wananchi, Serikali na wafadhili inapowezekana ambapo sasa tunaweza tukatumia mpango huu wa MMES na wananchi wameweza kufyatua matofali ya kujenga kwa mamilioni, kukusanya mawe, mchanga na kadhalika na kuchanga fedha nyingi sana.

Kwa hiyo, tuliweza kutoka zile Shule mbili tulizokwanazo kwa sasa hivi na kuongeza Shule tisa na kufanya jumla ya Shule za Sekondari kufikia 11. Kwanza tulianza na Shule inayoitwa Shule ya Sekondari ya Kiponzelo ambayo ilikuwa ya Tarafa na ikapata fedha toka *TASAF* pamoja na nguvu za wananchi na sasa hivi imeendelea imeshafika mpaka Kidato cha Nne safari hii. Ikafuata Shule ya Sekondari ya Wasa nayo imefika Kidato cha Pili na tumepata fedha za MMES hata hii Kiponzelo imepata fedha za MMES. Shule ya Kata ya Lumuli, inaitwa Lumuli Sekondari, nayo imepata fedha za MMES pamoja na nguvu za wananchi. Tumeshafungua *Form One* mwaka huu.

Shule ya Kata ya Kiwere nayo wananchi wamejitolea, wamejenga pamoja na fedha za MMES tumefanikiwa kufungua Kidato cha Kwanza mwaka huu. Shule ya Sekondari ya Nzihi, nayo tumepata fedha za MMES pamoja na nguvu za wananchi, tumefungua *Form One*. Shule tatu tunaendelea nazo, Shule ya Sekondari ya Mseke ambayo tumeshapata fedha za MMES tunategemea Januari 2006 Kidato cha Kwanza kitaanza.

Kuna Shule ya Sekondari ya Luhota, Kata ya Magulilwa nayo mwezi Januari tutafungua *Form One*. Nayo imepata fedha za MMES pamoja na Shule ya Sekondari ya Mgama, itakuwa nayo imepata fedha za MMES, kwa hiyo tutafungua *Form One*. Lakini vile vile tumeweza kusaidiana na wananchi ambao wamefungua Shule za binafsi (*private owned secondary schools*), kuna Shule ya Sagamiko Sekondari, iko katika Kijiji cha

Wenda, Kata ya Mseke, tayari wanafunzi wanasoma pale na kwa upande wangu mimi mwenyewe nimeweza kuwasaidia vitabu vingi sana vya Shule ya Sekondari. (*Makofii*)

Halafu kuna Shule ya Magulilwa nayo inajengwa na mtu binafsi akisaidiwa na Shirika moja la kidini la Kilutheri huko Marekani. Nayo tunasaidiana, tunategemea mwezi Januari itakuwa imefunguliwa. Kwa hiyo, zitakuwa ni Shule tisa tulizojenga za wananchi, halafu mbili ambazo wamejenga watu binafsi. Kwa hiyo, tutakuwa na Shule 11 mpya pamoja na zile mbili za zamani, kumi na tatu katika Jimbo la Kalenga. (*Makofii*)

Kwa vile hizi Shule kwa mfano hii ya Sagamiko na Magulilwa, hizi ambazo ni *private owned* wanaosoma ni watoto wetu, ningependekeza kwa nguvu zote kwamba mpango huu wa MMES nao kwa namna moja au nyingine wanufaikie maana wanaosoma ni watoto wetu. Inaweza kuwa siyo kwa kiwango kile ambacho Shule zile za wananchi zinapewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa vile vile kuonyesha wazi kwamba mipango tunayopanga na kupidisha humu Bungeni inatekelezwa kikweli na kwamba kweli uwezo tunao. Tumeweza kuwa na uwezo wa kujenga miundombinu, yaani kujenga huduma za uchumi na huduma za jamii. Kwa Jimbo la Kalenga tumekuwa na barabara nyingi za Mkoa, Wilaya ambazo zimejengwa na barabara ambayo. Ni ya zamani, sasa tunaanza kujenga kuwa ya lami kutoka Mjini Iringa kwenda Kalenga, Nzihi, Ipwasi, halafu inaingia Tarafa ya Idodi mpaka *Ruaha National Park*.

Kwa hiyo, kwa mara ya kwanza sasa kufika Kalenga kwenye Makao Makuu ya Mtwa Mkwawa ambapo pia ndipo alipozikwa sasa Hayati Chifu Adam Sapi Mkwawa, aliyekuwa Spika wa Bunge hili patakuwa panafikika kwa lami. Kwa hiyo, itaweka heshima ya mahala pale ambapo ni pa kihistoria kwa Wahehe na Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha tunazopitisha humu ndani vile vile zimeweza kuleta matunda mengi tu. Kwa mfano katika Jimbo la Kalenga, kwa kutumia mpango wetu wa *TASAF* kabla ya hii awamu ya pili ambayo imepitishwa sasa tumeweza kujenga Zahanati nyingi. Tumejenga Zahanati nzuri katika Kijiji cha Ng'enza, Kijiji cha Lupembelwasenga, Kijiji cha Mibikimitali, Kijiji cha Makombe na Kijiji cha Weru.

Tumefanikiwa kujenga mabwawa ya kilimo cha umwagiliaji maji katika Kijiji cha Kibebe, Kaning'ombe na kadhalika. Barabara vile vile kutoka Wenda-Kikombwe na kadhalika. Katika Shule, *TASAF* imechangia katika Shule ya Kiponzelo ambayo sasa hivi imefikia Kidato cha Nne na Shule za Msingi nazo imechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza vile vile kwa fedha tunazopitisha humu ndani za Bajeti ambazo zinaonyesha mafanikio katika hotuba ya Mawaziri wote wawili. Tumeweza kuwa na *irrigation schemes* Kalenga, Mgera, Magubike na sehemu nyingine mbalimbali. Ningombaa na kupendekeza kwamba hili jambo, limekuwa linapendekezwa na hata Waheshimiwa Wabunge wengi tu kwamba huko tunakokwenda katika suala la kilimo, twende zaidi kwenye *irrigation farming*. (*Makofii*)

Kwa hiyo, maji tunayoyatumia tuyatumie zaidi kwa ajili ya kilimo na upande wa umeme sasa tuondokane hatua kwa hatua kutumia maji *hydro electricity* na kutumia makaa ya mawe pamoja na gesi ili maji haya tuliyonayo tuongeze uwezo wetu wa kilimo cha umwagiliaji maji. Hili jambo ni muhimu sana kwetu sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa niendelee zaidi, lakini ningependa nieleze kwamba mambo tunayoyafanya mwanzo yanaonekana kama ni madogo. Lakini ni mambo makubwa katika historia ya nchi hii. Kuna Mwandishi mmoja anaitwa Dr. Myles Moonroe anasema: *"In every seed, there is a tree, in every tree there is a fruit and in every fruit there are more seeds in which you will find more trees, that will bear more fruits. The truth is that, in every seed there is a forest. Plant your seed." And that is what we are doing. (Makofî)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofî)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniruhusu niweze kuchangia. Tunachangia katika mawasilisho ya Wizara mbili, kwanza Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji na Wizara ya Fedha. Waingereza wanasema, *a plan is what you intend to do and the budget is the reason as to why you can achieve what you intend to do or you can fail.* Sasa kwa sababu wanapopanga mipango yao, ili iweze kutekelezeka, lazima kuwe na pesa.

Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji kwa jitihada ambazo wanazifanya. Halafu pili, nitoe mawazo kwa kadri ninavyoona. Nimepitia hotuba yake, mambo mengine ni yale ya kawaida ambayo huwa tunayazungumza hapa na kama si yale ambayo tunayazungumza hapa basi iwe tunabadili hii lugha kufuatana na wakati. Ila kitu kimoja, aliposema wanakusudia kupanda miti, ni kitu ambacho mimi nakiona ni kizuri kwa sababu raslimali nyingine kama dhahabu, samaki, almasi, *tanzanite* zinaweza kwisha ardhini.

Lakini mkiamua kwa nchi kubwa kama Tanzania, ambapo kuna ardhi kubwa na watu hawataki kuilima isipokuwa wanafuga mbung'o na nyoka tu, mkipanda miti kwa ajili ya mashamba ya kuzalisha karatasi na vingine inawasaidia na itawapa uhai kwa sababu ushahidi upo. Mwaka jana nilikuwa Afrika ya Kusini na Mheshimiwa Profesa Maghembe nadhani na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, tuliangalia nchi ya Swaziland ambako wanapanda miti na ile nchi haina madini.

Kwa kweli wanaishi vizuri na wana bajeti kubwa kufuatana na miti waliyoipanda. Ni suala tu la mahesabu kwamba mti mmoja mkubwa ni shilingi ngapi? Kama una miti milioni 200, basi huna wasiwas, una uhakika kwamba hapa kuna uendelevu na watu unaogaiwa *plot* na mashamba wanafanya kazi mle. Sina uhakika kama ninayoyasema yanafikiriwa au wengine wanadhani miti ni kitu cha hovyo. Lakini kwa dunia ya sasa, hata kama kuna kompyuta, hakuna utakachokifanya bila kubonyeza ikaenda kwenye karatasi. Kwa hiyo, hicho ni kitu ambacho ninawashukuru kwamba hilo wameliona. Lakini lisiishie pale, lazima kuwe na programu hiyo ya kupanda miti.

Miti inapandwa kwa sababu kama tatu hivi. Siyo kama ile ya Dar es Salaam, inapandwa miti inakaa hivi, mara inalalia nyaya, mara nyaya zitaunguza umeme, mara yanazikata leo, mara asubuhi. *At least you should have so many, uses of this*, kama ni *economic importance* tuone kwamba *this is for economic importance*. *For medical importance* tujue kwamba unatoa dawa pale. *For food importance and nutritional importance* kwamba mnapanda pale, kwa hiyo, siyo kupanda miti imekaa hovyo, halafu inaharibu nyaya halafu mnapata taabu. Siyo kupanda halafu mnacheka mnahesabu idadi, halafu inaungua kwa moto. Kwa hiyo, hilo mlione. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mtaniwia radhi watu wa Chama cha Mapinduzi. Lazima tufike mahali tukubaliane kwamba ubinafsishaji na tunavyoendesha uchumi, kwa kweli tunajiweka katika mtego mkubwa sana. Hasa pale Serikali inaposema Serikali haifanyi biashara, Serikali haiwezi kuwekeza, itawekeza kwenye barabara.

Leo hii tunachekelea tunapouza *Breweries*, tunapouza *Tanga Cement* yale majengo, tunapouza kiwanda cha Mgololo, tunacheka tu tunapata hela tunaweka mfukoni. Visingekuwepo mngeuza nini? Aliuliza hapa Mheshimiwa Moi kwamba mimi ninawashangaa, mnachekelea tu mmeambiwa muuze na Wazungu mnacheka tu, mnacheka tu. Sasa mkiuza vyote vikaisha halafu baada ya miaka 30 viwanda ni vya wawekezaji wengine, mtauza nini kama mtafilisika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi hapa ni kwamba, kuna vitu tunawenza kutaka kufanya Watanzania na wawekezaji tuliwaruhusu hawataki kwa sababu vinashindana na vya kwao. Unataka kujenga *heavy industry and primary industries*, viwanda vya msingi, viwanda vizito vya kutoa magreda, vya kutoa mashine kubwa ili tuweze kupeleka mashine hiyo kwenye kuchimba madini.

Hakuna mtu atakuja kukuwekea hapa. Ukimwambia unabinafsisha Kiwanda cha Bia, anajua watu wanakunywa bia wengi. Ukizunguka Dar es Salaam nzima bila kuona bia, wala hamna hata maktaba, lakini bia zipo. Ukiuliza wapi wanauza vitabu? Havipo. Ukizunguka hapa Bar, *Bar, Grocery, Grocery*.

Kwa hiyo, hapo watakimbia watakuja na matokeo yake hata ninyi mnaposema mmewekeza kule kwenye mtambo, mnapata *import duty*, kwenye mtambo wa kuchimba almasi na dhahabu. Hamwezi kupata kwa sababu bidhaa zote mzito zinatoka nje na mmewapa kwamba hawa tunawaondolea ushuru kwa sababu wanakuja kuwekeza. Hamna mtu atakaa kule kutoka Uchina, kutoka Japan, kutoka Urusi aje kuwawekea viwanda vikubwa hapa kwenye migodi ya chuma ile ya Liganga. Mtakaa hapo tu miaka 30, mnajenga hoja ambazo hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulikuwa kwenye Serikali wakati fulani, Warusi walikuwa marafiki wa Tanzania miaka fulani, walipoambiwa watathmini dhahabu iliyoko chini ya ardhi, walileta takwimu za uongo. Hata kama wakati ule tulikuwa marafiki zao. Kwa hiyo, usije ukadhani kuna Mzungu kule nje anakuonea huruma. Anataka akusaidie

akupe samaki, siyo nyavu, halafu hata kama wewe unaona anakuvekea maji kwenye kisima chako, anaweka kwa mrija halafu anayaondoa kwa bomba la Idara ya Maji. Si mnajua ile ukubwa wake ule.

Sasa mimi sisemi kuwachekesha, mwulize Mheshimiwa Waziri kwamba Geita wakichimba madini kwa mwaka kwa *royalty* wanalipa Shilingi ngapi. Hivi zinazidi bilioni tatu!. Zijumlishe zote kwa miaka 16 watakayochimba, hawawezi kulipa zaidi ya bilioni 300.

Ukisema Mbunge lazima ulete ushahidi, kama wakati *ana-wind up* hapa aseme kwamba kwa *royalty* ya asilimia tatu, madini yote watakayochimba kwa miaka 15 watalipa zaidi ya bilioni 300. Mimi nitajiu zulu na watakuwa wamepeleka nje zaidi ya madini ya trilioni nne.

Meshimiwa Mwenyekiti, mimi ninajenga hoja, maana haya mambo tunaposema tunapanga, lazima tunafikiri na tunatafakuri. *You have to think and reason and these are two different things. In reasoning there are five stages. In thinking, there are only three stages*, sasa sitaki kwenda kwenye *philosophy*. Kwa hiyo, mimi sisemi hapa kuchekesha chekesha tu. Sasa watu wanapanga, pale mimi nimekwenda Ikulu, pananuka. Ikulu ya Dar es Salaam, shombo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, univumilie, maana yake kuna watu wanataka kunikamata kwa Kanuni. Pananuka shombo la samaki pale Ikulu. Nimekwenda nimemwuliza Mheshimiwa Rose Migiro juzi nilikuwa pale Ofisi ya Waziri Mkuu, upepo ukija, tumbo mimi likauma, nikauliza, nini hii? Kuweka samaki pale Ikulu mna maana gani? Hii ndiyo utata tunaoupanga. Inanuka! Sasa kama kuna mtu anabisha hapa, anataka kunikamata kwa Kanuni, twende na pua, tuteuane, twende pale. Tuone kama hapanuki! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda Washington, wamesema hakuna kujenga majengo marefu kuzidi ya *White House*, hakuna! Kajengeni huko sijui wapi New York huko. Sasa wewe unachukua samaki unaweka pale Ikulu, wageni wanakuja shombo linanuka. Hivi hamkuwa na mahali pengine pa kujenga? Hiki ni kielelezo cha kwamba tunavyopanga hatuwi makini, hata watu hawaoni aibu. Ikulu mnapanga vitu vinanuka tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaelewa hata asali ambayo ni tamu, nyuki wanakwenda kwenye mikojo wanakwenda kwenye kinyesi na nini, ni tamu. Hata samaki ni watamu, wakishapikwa ni watamu, lakini wa hivi hivi mnavyofanya pale ovyo tu, pananuka. Hicho ni kielelezo cha kwamba tunapanga tu hivi hivi, yule aliyepanga pale anastahili kuadhibiwa. Mnajua wale wanaouza pale watakasirika, *I don't care* lakini mlifanya vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Yeye binafsi najua, *in every system there are sub systems* kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha anafanya kazi kwenye mfumo wa kiserikali. Yeye binafsi namshukuru kwamba ni mtu ambaye anasikiliza, unamfikia, hana kiburi wala hana ukorofi wala hana ujeuri. Yale

yatakayoshindikana ni kwa sababu sasa hawezi kuji-*knob*. Kwa hiyo, kwa hilo namshukuru.

La pili, sasa madeni nadhani Watanzania *they are very much euphoric* kwamba tumefutiwa madeni, wanakimbia wanaimba, wanataka waandamane, wajipongeze wamefutiwa madeni. Maana yake nini? Wewe unakwenda kule unakopa, unakuja kwa mke wako ulinunua vijiko umeweka hapa na sahani na uma halafu mzigo unakuwa mzito unatoa uma unauba halafu unakopa ili ununue glasi. Maana hatujui Watanzania wangapi waelezwe trilioni tisa tunazodaiwa sisi zilikwenda wapi. Mwingine atasema tulijenga viwanda, mbona mnaviuza sasa. Si ndiyo ulikopa ukununua kijiko halafu unakuza unataka kununua uma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna haja ya kujipongeza hapa umefutiwa madeni, Kenya kwa nini wasijipongeze? Maana yake inaonekana kama Kenya watu wa ovyo, hivyo wamenyimwa msaada. Wao bajeti yao asilimia tisini, mia moja. Kwa trilioni zaidi ya tano za kwao wanakusanya. Sasa Wazungu kwa sababu wanataka watupe masharti, wakija wakikukopesha hivi, wewe unafurahi, wananipenda wamenikopesha.

Lazima wakupe masharti. Sasa Kenya hawawezi kuyapeleka. Korea ya Kaskazini hawawezi kuyapeleka. Iran hawawezi kuyapeleka. Ndiyo maana yake. Kwa hiyo, tunashangilia tunesamehewa madeni, tunesamehewa madeni halafu tunakaa na hii inaendana na kwamba yale madeni tunayosamehewa tumeyafanyia nini na tunayokopa tunayafanyia nini? Nimezungumza tulikuwa kwenye semina Dar es Salaam kwamba hivi Serikali inapokopa, Wabunge inawaambia? Au inawapa taarifa? Maana yake kuna mtu kumwambia unamshirikisha, kuna mtu kumpa taarifa kama anapinga kheri na kama anataka kujinyonga aende ajinyonge.

Kwa sababu kama umekopa wewe umemwambia tunakwenda kukopa hela za kujenga hapa, watakuja wasimamie waone. Sasa wapi unachukua hela hizi? Sisi tunafanya hivi mambo ya mzaha mzaha hivi, tujifunze kutoka kwa Wachina, watu wanajenga hapo jengo, kila mmoja ameliona hapo wala halitamaliza mwaka limekwisha. Lakini mtu anapewa kazi pale anafanya mwaka, mwaka, mwaka, miaka 10. Lete taarifa, unajua hela ziliongezeka, unajua, macho anayatoa tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la deni la Taifa nadhani tuna matatizo kidogo. Naomba Wizara ya Fedha nilikutana na Walimu jana pale, wanasema mmetuma cheki, mmeandika kwenye magazeti. Lakini wengine hazijawafikia, wamekwenda pale kwa Mkurugenzi wanamwuliza, mbona tuko wengi hapa 200? Anasema zimefika cheki hapa za watu 20 Mkoa wa hapa Dodoma na wengine wanalamika kule nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua, Serikali hivi huwa ina *circular* ya kujua magari yanayopashwa kununuliwa na Serikali, yako mabenzi ya Ikulu, yako magari ya Mawaziri, mimi ningeyapanga hivyo, yako ya Wakuu wa Mikoa, yako ya Wabunge na watu wengine. Sasa nataka kujua Serikali ina utaratibu wa kujua Serikali inanunuaje magari yake kwenye Wizara zote. Maana watu huku na Waandishi wa Habari na watu nje, Wabunge wamenunua mashangingi, oh! Wamenunua. Kama kuna Mbunge hapa ana gari la milioni 30 asimame hapa, mimi nitajiuzulu. (*Kicheko/Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuzulu kabis! Au kama mna maandishi au Hazina inasema Wabunge, wana magari ya milioni 30, *I will resign.* Sitagombea tena! Nitakuwa mwehu! Mwende muwaambie kwenye Jimbo langu. Lakini unakwenda kwenye Wizara wanunu gari, sijui la Mhasibu, mimi sijui la nani, milioni 70, mna maana gani? Nina ushahidi. (*Makofit*)

Kama mnataka, muulete hapa. Kama upo najiuzulu. Sasa milioni 70 kuna mwongozo gani? Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba uandike hapo, halafu unijibu. Kuna mwongozo gani kununu magari ya Serikali ya watu wa kawaida milioni 70. Tumezungumza hapa, tumeanzisha kile Chuo cha Mwalimu Nyerere, *Nyerere Foundation*, kwamba hiki Chuo bwana kawapeni fedha za kutosha, mnapeleka pale milioni 100. Unakwenda kwenye Wizara wamejipangia magari matano zaidi ya milioni 400, watu wanne tu nyinyi mnachukua hela hapa tunataka kujenga Vyuo kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijiuzulu, mnataka kwenda kwenye Jimbo langu? Sitajiuzulu, sasa haya mambo yanatucheleshwa, tunapopanga hatuvezi kutekeleza tunaahirisha, tunaahirisha tunakuwa kama nyani. Unajua nyani wanakaa kwenye msitu. Kuna miti mingi, sasa wakaambiwa wajenge nyumba, huyu anasema unajua mimi nakwenda kwenye Mahakama. Niliokota mtoto wa mwanamke na ye ye akaokota mkia wangu. Huyu nyani mwingine anaambiwa nenda kwenye Mkutano mjenge nyumba. Anasema unajua niliiba mahindi ya fulani. Nyani mpaka sasa hivi hawana nyumba, wanakaa tu kwenye msitu ambayo ina miti wanarukaruka, wanakimbiakimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii wengine wanasema inawasaidia wanyonge na hii lugha ya wanyonge mimi sijui inatoka wapi. Tunakomboa wanyonge, mwaka 1961. Tunatetea wanyonge, miaka 50 wanyonge. Hivi hawa wanyonge mna mkataba gani nao kwamba waendelee kuwa wanyonge muwatetee wawape kura, mna mkataba gani nao? Wanyonge!

Sasa kama nyinyi mnataka kuishi kama Wafalme isiwe kama Mungu, Mungu ni Mfalme amewapa dhahabu, amewapa maji, amewapa miti, amewapa mafuta ambako kuna jangwa chimbeni wote mkaishi. Nyinyi mnapanga bajeti hapa ya kusaidia wanakijiji, maji tuko tu. Punguza mafuta, ushuru wa mafuta, mnapunguzana nyinyi

kwenye ndege. Hivi *World Bank* hawana hela za kulipa kwenye ndege hata mkawawekea trilioni za punguzo la ushuru?

Punguza wale ambao wanakwenda pale kwenye mafuta ya taa na ndiyo wanalipa *VAT* mwisho kule. Hamtaki mnasema tunawasaidia wanyonge. Kawajengee viwanda, kawapeni mikopo wabangue korosho zao, kawapeni mikopo wajenge viwanda vy a kusindika kahawa, kusindika iwe unga siyo mnapeleka tu pale kahawa. Kikombe kimoja tu pale London ni dola tatu, kilo ya kahawa Mbeya sijui wapi kilo Sh.200/. Ukiwaambia mnapanga nini, tunachecha tu, unajua tunapanga. Unapanga nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani sasa unapojuizulu ni pale ulipokosea na kwamba hufai, lakini kama unatoa hoja, hupashwi kukimbia, unakaa pale unatoa hoja, kama kuna wa kukupiga anakupiga. Nakushukuru sana. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Najiuzulu tarehe 30 Julai, 2005.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi naungana na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi kwa Mheshimiwa Abu Kiwanga na Wabunge wengi ambao wametutoka katika kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani kwa wanawake wa Mkoa wa Pwani katika vipindi viwili wameweza kunichagua kuwa mwanamke na nilikuwa wa kwanza na ninawawakilisha naomba niwashukuru na ninawaambia sikuwaangusha, nilifanya kazi kwa uhakika na nilisikika kwa uhakika. Kwa hiyo, ninawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Pwani, lakini naishukuru UWT kutoa nafasi hizi za wanawake na kunipa mimi *confidence* ya kufanya kazi ndani ya Bunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naishukuru CCM kwa kupanga sera zake za kuwasaidia wanawake na ndio maana wanawake tuko hapa, naomba niwaambie CCM, UWT na wanawake sisi tuliokuweko huku ndani ya Bunge hatuwaangushi, tunajitahidi kwa uwezo na kwa faida yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niwashukuru watu wa Mkoa wa Pwani wanawake kwa wanaume angalau mimi nilikuwa Mbunge Viti Malaam Wanawake lakini walinikubali kwa uhakika hata wakanipa Uwenyekiti wa Wazazi Mkoa wa Pwani. Bado naomba niishukuru Serikali, tukiwa ndani ya Bunge inawezekana nilikuwa mkorofi sana lakini waliweza kunivumilia na waliweza kunisaidia na wakweza kunitangaza na nikawa najulikana, naomba niishukuru Serikali kwa uhakika kabisa. (*Makofî*)

Naomba nimshukuru Spika, Naibu wa Spika, wewe Mwenyekiti na Mwenyekiti Mheshimiwa Eliachim Simpasa, kwa kweli mliweza kunipa nafasi mpaka nikawa nasikika kwa kweli naitwa mwanamke shupavu nashukuru sana. Mngekosa kunipa nafasi nisingeweza, lakini bado nawashukuru Wabunge wenzangu, tuliveza kukaa pamoja tukashirikiana, tukapanga kwa faida ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi wananchi kwa

jumla na nashukuru walionichagua kuwa Mwenyekiti wa *APNAC* niliweza kufanya kazi na Serikali katika suala zima la kusaidia kupambana na rushwa na Serikali imejitahidi kwa kweli, na sisi *APNAC* tumekuwa mfano katika Afrika na katika *GOPAC* kwamba *APNAC Tanzania Chapter* kwa kweli ni *mode* na watu walikuwa wanatuita, walikuwa wananiita mimi kutoa semina na kuwaelimisha, naomba niwashukuru wajumbe wa *APNAC*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo naomba na mimi niwaambie watu wa Mkoa wa Pwani, Wilaya ya Kibaha, kwamba wasitetemeke na wasisikie usanii wa watu ambao wao wenyewe wanaogopa wenzi wao kwa hiyo, wanaweka usanii, mimi sijafungwa, sijatiwa, mimi sijalazwa, mimi sijakimbia Arabuni, sijakimbia Ujerumanii wala Marekani niko buheri wa afya na nina waambia nitagombea Jimbo tena bila ya woga na huo usanii wanaotumia wakuuwa ni shauri ya woga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo naomba nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kaka yangu kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa Chama cha Mapinduzi, naomba nimwambie Mheshimiwa Jakaya Kikwete, watu wameshakuwa na imani na ye ye sana na imezidi wakati alipokuwa anazunguka kushukuru na kuwaambia wananchi, zile *speech* zake watu wote wameshakuwa na imani na watu wamesema wengi wanajiuzuru kutoka kwenye vyama vingine kuingia CCM.

Naomba nimpongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Amani Abeid Karume na wao pia kuteuliwa Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kuwa mgombea mwenza na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kuwa mgombea urais Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli napongeza Serikali kwa dhati, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imetekeleza kwa asilimia kubwa ilani ya uchaguzi kwa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kwa asilimia kubwa hata uchumi umepanda, kutokea asilimia 4 sasa tuna asilimia 6.7, mimi naomba niwapongeza na hasa nawapongeza lile suala la uwazi na uwajibikaji, mnajikuta katika magazeti tunaambiwa taarifa za uchumi, tunaambiwa mambo mbalimbali, *PSRC* wanapotoa matangazo yao tunaambiwa, Rais mwenyewe kila mwezi, hii naomba niwaambie wenzetu wanataka kuiga nchi za nje kwa moyo yaani nikisema *East Africa* wanatupongeza sana.

Kwa hiyo, mimi nasema Serikali ya Chama cha Mapinduzi mmejitahidi isipokuwa tu tunapongeza mawili, matatu, kukusaidieni tu. Baada ya kusema hayo naomba nishauri, nashauri tumezungumza na watu wanategemeo kubwa kwa Serikali ya awamu ya nne na hasa vijana kwa ajira, sasa naomba nishauri ajira hasa kwa vijana.

La kwanza, naomba utaratibu uwekwe kiwango ambacho watu wetu, vijana wetu wakimaliza wata-*compete* ndani ya nchi na nje ya nchi. Ili waweze kupata kazi ndani ya nchi, waweze kupata kazi nje ya nchi, isifike hatua mtu anamaliza Chuo Kikuu hata ku-*apply* kazi anashindwa. Kwa hiyo, naomba cha kwanza elimu yetu tuiwekee mipango kuhakikisha watu wetu wata-*compete* kama wenzetu wa *West Africa* wanavyo *compete* ndani na nje ya nchi.

Lingine wafanyabiashara wadogo wadogo mimi nawaomba tuwawekee utaratibu, nimekwsenda China nimekuta wamachinga sijui ndio mnawaita wamachinga au mnawaita juakali wamepangwiwa kitu kinaitwa *moro* yaani wapo pale wamepewa uwezo wanatengeneza vitu ambavyo vina *compete* hata sisi ukija mtu kutoka nje unapelekwa pale na unavinunua vilivyokuwa vimepandishwa thamani.

Kwa hiyo, mimi naomba hawa vijana wetu wamachinga hawa machingazi wanaonunua mitumba tuweke utaratibu, mitumba iletwe yenyenye thamani kwamba hata ukienda Kenya, Uganda watakuja Tanzania kununua mitumba, tusione biashara ya wasiwasi. Tunazungumzia mama ntilie, mama ntilie waendeleze kiwango kuanzia kupika barabarani waende kwenye maharusi ikiwezekana hata watoke katika *East Africa* wa *compete* na *East Africa*.

Tunazungumzia wafanyabiashara wadogo wadogo wale wenzetu wanaotengeneza labda wanatumia mbao kutengeneza vitu, watengeneze vitu kama vile vinavyofanywa hapa Chang'ombe, basi tuwasaidie waendelee hawa vijana wakipata ndio ajira, ajira sio ya kwenda kuajiriwa tu, lakini ajira ya kilimo, mimi naona hatujakuwa *serious* kwenye kilimo, utanisamehe kaka yangu Mheshimiwa Charles Keenja lakini nasema hatujakuwa *serious*.

La kwanza, tuna maafisa ugani, kuna maeneo mengine kila kijiji kuna maeneo mengine kila Kata, maafisa ugani hawa *percent* kubwa ukiwaambia wananchi kule vijijini mnawafahamu, hawafahamu hawajawaona kazi yao na pikipiki, hawana mpango wa kazi hawana taratibu za kazi na kwa kuthibitisha hawafanyi kazi mpaka leo bado tunalima kilimo cha asili. Siku moja nimekaa mahali nawaeleza wananchi kuhusu kilimo, akatetewa Afisa Kilimo anaambiwa huyu anakuja kila saa, nikauliza hapa nipo kwenye mkorosho, mkorosho huu wa nani? Akasema huu wa kijiji tena Shungubweni, mbona mkorosho huu una ma-branches mpaka chini si ndio ungekuwa mfano?

Sasa mimi nasema tuwawekee taratibu maafisa kilimo hawa tuwapangie kazi waoneshe *plan of action* zao na zile Serikali za vijiji ziwawekee Sheria ndogo ndogo ili wafanye kazi. Maana yake wakilima vizuri badala ya eka moja ya mahindi kutoa nusu debe inaweza kutoa hata magunia ishirini kwa maana ya kama Kibaha, hilo la kwanza.

Lakini la pili, umwagiliaji, naomba tutenge maeneo sio kila eneo linawenza kufanya umwagiliaji tutafute mikoa ile ambayo tunaweza kufanya umwagiliaji tutenge maeneo tulime kwa hakika tuhakikishe mavuno tunauza ndani na nje ya nchi. Tukifanya tu umwagiliaji kila sehemu tutashindwa, tunakwenda kwenye suala zima kuwatafutia masoko sio tushindane, nakumbuka wakati wa korosho kipindi hiki hiki kati ya 2002/2004 tulikuwa tuna Wabunge na Mawaziri tunagombana, naomba tuyatafute masoko ya biashara zote ndani na nje na tuweke *finishing good* sio unapeleka korosho ihakikishwe imepakiwa vizuri, wasaidiwe hao wabanguaji, kaka yangu Mheshimiwa Charles Keenja tumelumbana hapa miaka mitano ananiambia nitakusaidia, nitakuletea mashine mpaka leo Bunge linakwisha watu wa Kibaha waliokuwa wanabitaka, watu wa Mkoa wa Pwani hawana mashine, hawana nini, wananiuliza mama mbona umetudanganya, nasema kawadanganya Keenja. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi kwene suala zima la uwekezaji, hawa wawekezaji tuwasaidie, tuwakaribishe bila ya woga, watu waseme lakini tuwakaribishe, kwa sababu ukimkaribisha mwekezaji ataongeza ajira kwa vijana na wata compete kwa sababu watakuwa na elimu nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa kwa mfano mwekezaji wa hoteli, atataka aletewe mayai, mfugaji akipata soko kubwa atalazimika kuwaajiri vijana, kumsaidia mayai. Kwa hiyo, katika mtindo huu vijana wetu watapata ajira na mikopo. Naomba nimshauri kaka yangu Mheshimiwa Basil Mramba alisema mikopo ya Serikali hasa hii ya Halmashauri tutaitafutia utaratibu, mimi naomba nikushauri, tatuwa *agents* wakuchukua hii mikopo kukopesha mkiwa mnawasimamia. Kwa sababu mikopo ya sasa hivi hii ya Halmashauri *ten percent* ni mikopo sasa hivi ya kisiasa, Dr. Gama anataka Ubunge, karibu ya Ubunge nawatafuta watu wanakopeshwa ikifika wakati Dr. vipi mbona watu wako hawarudishi nashindwa kwenda kuwaambia, naomba weka *agents*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini inasikitisha, tunazidi kushuka tu hii ya mwaka 2003 tulikuwa kwenye asilimia *eighteen* katika Pato la Taifa, sasa hivi tuko *fifteen point six*, naomba madini jamani ndio tukiyavuna tumeyavuna, tukiyachimba hayarudi tena nayo tuyawekee utaratibu mzuri. Narudi Mkoa wa Pwani, jamani ninamwomba Waziri wa Ujenzi atusaidie ukiacha barabara kubwa inayotoka Dar es Salaam kwenda Mbeya, Tunduma au kwenda Arusha na barabara kubwa inayokwenda Lindi, Mtwara na hii inayotoka Dar es Salaam mpaka Bagamoyo hapo tu ni za lami, lakini mkoa wa Pwani ni mkoa wenye hadhi ya kijiji, hauna barabara ya lami ukiacha hizo.

Mimi nilikuwa naomba tusaidiwe jamani sasa inasikitisha zile barabara nafikiri hii Bajeti ya *TANROAD* sasa hivi imekwisha, barabara tunayokwambia yanatisha mkoa wa Pwani. Wengine tunaambiwa tumewekeea barabara za changarawe, lakini za vifusi samahani sana kusema hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafia, Mafia tusipoangalia Serikali ya Chama cha Mapinduzi tutakuwa ni sababu ya Kisiwa kuchukuliwa na Upinzani, sasa hivi Kiwanja cha Ndege kinatisha, tiketi sasa hivi ni elfu sitini, ilikuwa arobaini imepanda na wale watu wa ndege wenye makampuni ya ndege wengi wameacha kwenda Mafia. Kwa hiyo, anayesafiri Mafia ni mwenye uwezo wale wanaosafiri kwa maboti, wengine wanapata shida na nashukuru *Tsunami* ilikuwa haikukuta watu kwenye bahari wangekuwa. Naomba tusaidiwe pia kupewa gati Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani mnafanya watu wa Mafia wawe Kisiwa, Wakojani waje kutunyanyasa, Wakojani wanatunyanyasa sasa hivi na wanaletwa makusudi ili *CUF* ichukue, samahani kwa kusema hilo, naomba kweli Serikali ya Chama cha Mapinduzi isaidieni Mafia.

Naomba nzungumzie wastaifu, nazungumzia wastaifu wa Mashirika ya Umma, haya Mashirika yalikuwa Mashirika ya Umma ya Serikali kama mlivyofanyia wastaifu wa Serikali haya Mashirika yalikuwa ya Serikali, wastaifu hawa wamepewa tu *take home*

wameachwa wanakufa, hali zao mbaya hii kwa sababu yalikuwa Mashirika ya Umma Serikali igharamie, iwave, iendelee kama ilivyofanya kwa wastaa fu hawa wengine. Kwa kweli wanasikitisha, hali zao zimekuwa mbaya naomba tufikirie tena, tufikirie kama tulivyofikiria wastaa fu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PSRC* nafikiri nina dakika kidogo, *PSRC* mimi naishukuru sana, imejitahidi kwa uwezo wake lakini kweli nazungumza kwa uchungu na najua ni Bunge la mwisho hili, naomba tuambiwe *IPTL* inafanya nini *IPTL* naomba tuambiwe, mimi niliuza swali hapa naona Mheshimiwa Spika, aliamua kuwalinda tu Serikali kwa sababu lile swali ndani yake lilikuwa *IPTL* iliwekwa katika ile saini inavyotumia pesa nyingi bilioni 4 kila mwezi, umeme kila siku unakatika, *IPTL* mkataba ule kwa nini tunashindwa kuitizama vizuri Wamalaysia, Wamalaysia wanafaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono mia kwa mia Bajeti hii.  
(*Makofî*)

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa kikao, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi nipaye nafasi ya kujadili hoja zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kukupongeza sana kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti, wa MKURABITA utanisamehe maana sijui kama MKURABITA au MKUKUTA haya maneno mapya kidogo.

#### **MWENYEKITI: MKURABITA.**

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** MKURABITA, lakini nichukue nafasi hii pia kumwomba Mwenyezi Mungu kwako wewe mwenyewe binafsi, lakini na kwa Wabunge wote ambao wamo ndani ya Bunge najua wana mambo mengi ndani ya nyoyo zao, basi Mwenyezi Mungu awajalie hayo wanayoyaomba wayapate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba Bunge hili pamoja na wewe mwenyewe katika kipindi hiki yamefanywa mambo makubwa sana na nina imani sana na wananchi wa Tanzania watarudisha wote katika Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili tukageuka kama mchimba kaburi, maana mchimba kaburi akishamaliza kuchimba hilo kaburi akiambiwa aingie ndani ya kaburi abakie mle hakubali. Sasa Bunge hili limeleta maendeleo makubwa sana, Bajeti nzuri mpaka tulipofikia hivi sasa. Lakini sio hiyo tu, kuna mageuzi makubwa katika Bunge. Bunge linalokuja la mwaka 2005 kuna ukumbi mpya wa kisasa na bahati nzuri kwa kushirikia na Mheshimiwa Spika, Wabunge hawa wamepewa mafunzo maalum ya kuingia katika karne hiyo. Nadhani wanaweza wakasaidia kuwa nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia na mie niungane na wenzangu kumpongeza mgombea au mgombea mteule wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, nimpongeze Mheshimiwa Aman Abeid Karume na mgombea

mwenza wa Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein. Naamini kabisa kwamba watakapokabidhiwa kijiti hiki cha kutekeleza sera za Chama cha Mapinduzi watatekeleza vizuri sana na naamini ndani ya miaka mitano ijayo kutakuwa na mabadiliko makubwa kabisa ambayo hayajawahi kutokea Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kutoa rambirambi zangu kwa msiba wa Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahala pema peponi. *Amin.*

Niungane na wenzangu wengi wamezungumzia na mimi nilikuwa nahangaika sana kuangalia vitabu vyote, cha Mipango na kile cha Bajeti. Nilikuwa naangalia vizuri sana suala la ajira. Tanzania hivi sasa suala la ajira ni ajenda, ni vizuri wenzetu ambao wako Serikalini wakalizungumza vizuri maana hivi sasa hasa kundi la vijana lina matumaini makubwa sana na Serikali hii na ijayo, kwamba mkakati utaandaliwa vizuri na vijana wetu watapata ajira, bila ya kuwa na ajira katika nchi vijana watakuwa tafulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu hilo la kwanza na nadhani wenzangu wengi wamelizungumzia. Jambo lingine ambalo nalizungumzia ni suala la mshahara wa kima cha chini. Waziri amesema kwamba, mshahara wa kima cha chini hivi sasa utakuwa shilingi 60,000, lakini ukiangalia 60,000 hivi sasa hazikidhi haja, shilingi 60,000 maaana yake nini?

Shilingi 60,000 kwa mtu ambaye anamiliki watoto watatu nyumbani kwake mtumishi wa chini anahitaji apate sembe kidogo, alipe umeme, alipe maji hawezi kuishi, maana maji katika nyumba moja ya mchango haipungui kwenye shilingi 5,000 lakini umeme hawezi kupungua kwenye shilingi 12,000, sasa kinabakia nini? Bado atahitaji ye ye kama yuko Dar es Salaam nauli ya kutoka nyumbani kwake kwenda kufanya kazi. Sasa ndani hapo fungu lililobakia haliwezi likazidi shlingi 25,000, ataishi namna gani? Nilitaka kusema kwamba Serikali ni vyema iangalie na inapoweka kiwango cha chini isiangalie tu kwamba kiwango cha chini ndiyo hicho kinatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi kutumia neno walalahoi lakini kwa kweli wenzetu wanaopata mshahara kiwango cha chini hali zao si nzuri, ni vyema Serikali naiomba iangalie upya. Jambo lingine ambalo nitalizungumzia na nataka niipongeze sana Serikali hasa Mheshimiwa Basil Mramba kwa sababu ameliweka, amaeliweka kwamba safari hii Serikali imetenga na imeweka ndani ya Bajeti asilimia 4.5 ya misaada kwamba itagaiwa katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, jambo zuri sana na si la leo, wale waliokuwemo humu tumekuwa tunalizungumza hili jambo zaidi ya miaka kumi halipati ufumbuzi wake. Sasa Mheshimiwa Basil Mramba kama umefikia kuliweka katika Bajeti nakupongeza sana na nakutakia heri na fanaka na *Inshallah* katika mwaka 2005 tukutane hapa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini inapopitishwa kwamba sasa ipewe asilimia 4.5 Zanzibar imepitwa na wakati, jambo hili lilipendekezwa na Mheshimiwa William Shelukindo, akiwa Katibu Mkuu, leo Mheshimiwa William Shelukindo ni Mbunge, toka mwaka 1991, kwenye Kamati ya Shelukindo, asilimia 4.5 toka yule bwana aliyeju hapa

sitaki kumtaja jina lake yuko kijana mpaka kaja hapa mzee, bado tunasema aslimia 4.5 ya misaada yote, haiwezekani. ni vizuri kiwango cha misaada angalau kifike asilimia 10 (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba katika kuungana lazima mambo mengine tuvumiliante, tukubaliane kwamba hali ya uchumi wa Zanzibar sio nzuri hivi sasa. Tukubaliane kwamba kiwango hiki hakiridhishi hata kidogo na hali ya umaskini imeongezeka na nasikitika tu hapa nasikia Mawaziri wanasema umaskini, umaskini, kwa nini hamzungumzii kabla ya umaskini, maskini anakawa na uwezo wa kula, anajua atalala wapi, anajua atafanya nini, lakini wapo Watanzania hivi sasa mafukara, fukara hajui atalala wapi, ataamka wapi, atafanya nini? Hao wanahitaji kuzungumzwa na tukajua mikakati ya Serikali ikoje. Kwa nini tunaanza na hao maskini, mafukara tunawaacha? Na dalili zipo tu ukitoka nje na sehemu nyingine utawaona watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme na niombe sana kwamba naiomba Serikali ya Jamhuri wa Muungano iki kiwango cha aslimia 4.5 kiangaliwe upya, ili Zanzibar katika suala la misaada kutoka nje manung'uniko yaondoke. Nataka leo niseme haraka haraka lingine ambalo nataka nilizungumzie na limenifuarahisha Serikali katika Bajeti yake imetenga fedha za madhumuni ya kununua dawa za kurefusha maisha, nawapongeza sana. Lakini ninachosikitika sikuona katika Bajeti hii Serikali imetenga kiasi gani cha kuhudumia yatima, Tanzania hivi sasa kuna yatima zaidi 10,000 na wapo tu wengi kwenye *NGO's* wengine wanaranda tu mitaani, wengine hawaeleweki, watoto wa mitaani wameongezeka, Serikali iko kimya na Bajeti hii haikuwazungumzia hawa, watazungumziwa na nani katika janga hili la UKIMWI, wako watu wamekosa baba, wamekosa mama, wamekosa shangazi na baadhi ya nyumba zimefungwa hata kurithiwa hazirithiwi.

Sasa Serikali imezungumzia hawa kuwahuisha, lakini hawakujuwa watasoma vipi, wataishi vipi, watakula nini, watakwenda namna gani hajiazungumzwa, mimi nadhani sasa hivi Serikali ndio ingeanzisha makambi maalum ya watoto yatima mbali ya zile *NGO's* zinazosaidia, lakini yawekwe makambi maalum ya watoto yatima ya kuwasaidia hawa vijana ili tuhakikisha kwamba maisha yao wanapata elimu nzuri, wanaishi vizuri hili ndio Taifa la baadaye la kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia nizungumzie na niipongeze Serikali sana suala la kuweka msamaha wa *VAT* katika vifaa vyta treni napongeza sana, lakini treni ukiitizama treni sijui tufananishe na nani, nikisema na jongoo si sawa. Treni mara nyingi haiwezi kufanya kazi yenyewe lazima ina vyombo vingine inavyovitegemea. Treni ya Dar es Salaam imeanzia bandarini, maana mzigizo unapofika pale unatoka nje unaletwa na meli na ziko meli za Watanzania zinatoka nje na ziko meli zinafanya kazi ndani na inakoishia reli ya kati ziko meli katika Ziwa Victoria.

Sasa nilikuwa naomba tu kwamba huu msamaha wa vifaa mbalimbali, huu msamaha wa *spare* za treni nilikuwa naomba msamaha huu uhuishe *spare* za meli, itasaidia sana Watanzania wanaotumia meli kwa kupakia mizigo yao na kwa usafiri. Leo hii Watanzania hasa Mtwara wanatatizo la usafiri, mmezungumza kuna upungufu wa

meli. Tukisaidia vifaa vya meli vikapungua *VAT* bila shaka na nauli ya kwenda Mtwara itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa niseme hilo tu kwa ufupi, lingine ambalo ningeliomba na lenyewe niliseme ni suala la vinywaji baridi, soda, *juice*, hivi Mheshimiwa Basil Mramba, wewe ukatia vyote kodi hata *juice*, hata soda, waachie watu wanakunywa soda, soda lazima ipatikana kwa bei nafuu zaidi. Sasa leo imeongezwa *VAT* nilikuwa naiomba Serikali iachane na hii *VAT* kwenye soda, kwenye vinywaji baridi hivi wanakunywa Watanzania wote pamoja na vijana na watoto wa Taifa, nani mtu hapendi watoto wake na wagonjwa hospitali naambiba hapa nilikuwa naomba sana na nasema kwa ufupi ili Mheshimiwa Basil Mramba, usije ukasahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba jambo hili la usawa wa kodi baina ya SMT na SMZ usawa wa kodi bidhaa inashuka Zanzibar, kodi yake sawa na Dar es Salaam na Dar es Salaam sawa na Zanzibar, imeifanya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iwe lofa, imeifanya hali ya uchumi wa Zanzibar uwe mgumu na hili tumelisema na tukalisema, wenzetu mmeziba masikio, hamsikii, hamuoni, labda wenzetu kwa sababu katika ofisi zetu mna *air conditions* sasa sisi uwezo wetu wa kusema na hii Mwenyezi Mungu atatupa thawabu zetu na ninyi wenzetu mnaokuwa tunawaambia hamsikilizi atawahukumu kwa yenu. (*Makofit*)

Tumesema na kusema, leo Zanzibar kuna watu milioni moja, huwezi kumlinganisha mfanyabiashara wa Zanzibar awe sawa sawa na mfanyabiashara wa Tanzania Bara, Zanzibar kama utaleta *television* milioni moja ina maana kila Mzanzibar mpaka mtoto atanunua ya kwakwe, zile zitakazobakia atauza wapi? Lazima muandae mkakati wa kibiashara unaoeleweka kuipa nafuu Zanzibar. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, akinamama hawa, akinamama zamani wa Dar es Salaam wanakwenda Zanzibar na ndio wanaopenda Muungano wa namna hiyo, wanakwenda Zanzibar wanarudi. Wananyanyasika akinamama, tumeshasema hapa si mara ya kwanza, si mara ya pili, si mara ya tatu, akinamama hawa wanaokwenda Zanzibar kwanza siku hizi hawaendi tena, kwa sababu wananyanyasika, mzigo wa mkononi unalipa kodi, kisha ukalipa na *weight* kilo mbili, tena kuna mtu ana *machine gun* pale ukifika na mzigo wako wa kilo tano, kilo ishirini ulipe kodi ya kawaida uongeze uishe ukalipe na *weight* na Zanzibar ilishalipwa, hivi nyie wazee mliowekwa huko Wizara ya Fedha na Mipango, mipango hii inafanywaje. (*Makofit*)

Sasa bidhaa za kutoka Zanzibar hakuna za kushikwa siku hizi wameanza kuzishika za Dar es Salaam zikienda kule Zanzibar, wakikuona na kilo tano, kumi unafuatwa mbio na watu sita, saba, nane, tisa, mzigo huu ulete hapa uje ufanye makisio ya *weight* na *custom*. Toka lini nchi moja, Rais mmoja na kila kitu kimoja akinamama wananyanyaswa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, rafiki yangu sana Waziri wa Mipango na sasa hivi wewe Mheshimiwa Waziri bahati nzuri uliyokuwa nayo wewe ni mfupi, lakini mpevu na hili Bunge tunamaliza, Dar es Salaam mimi na wewe ni vizuri Watanzania waweke hekima yako ambayo waliipata. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofit*)

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ili nami nichangie hoja hizi zote mbili. Kwanza kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kilolo nitoe pole nyingi sana kwa mwenzetu Mheshimiwa Abu Kiwanga, ambaye ametangulia mbele ya haki. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi. *Amin.*

Pili natoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Amani Abeid Karume na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuteuliwa kwao kuwa wagombea wa katika uchaguzi mkuu ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kuchangia hoja ya Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda ambayo ni Ubanafsishaji. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana, kwa kweli kazi imefanyika vizuri kama kawaida na yale ambayo tumekuwa tukimshauri ameyafanya kazi vizuri. Lakini ushauri wangu ambao ningeomba kuutoa ni kwamba ye ye ndiyo tunamtegemea sana katika mipango ya nchi yetu. Kwa hiyo, aimarishe vizuri Chuo cha Takwimu na Chuo cha Mipango, kwa sababu kama hatutakuwa na takwimu za uhakika sio rahisi tukafanya mipango mizuri.

Kwa hiyo, naomba sana, mwaka jana tulikubaliana kuwatengea Chuo cha Mipango fedha za kujengea mabweni lakini sina hakika kama mabweni yale kwa kweli yamejengwa, kwa hiyo, kama halijafanyika hilo basi naomba lifanyike haraka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niende sasa kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba kwa kweli Bajeti ya mwaka huu kama ulivyosema mwenyewe ilikuwa tulivu, nzuri na kwa wale wenzenetu ambao hawana macho pia wameweza kuona ni kwa sababu tu inabidi waseme, lakini ni Bajeti nzuri na nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri.

Pia nikupongeze kwa Serikali yetu kufutiwa madeni, Mheshimiwa hii ya kufutiwa madeni inaendana sambamba kabisa, maana yake waliotufutia madeni ni wenzenetu wageni wa nje na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje ndiye ameteuliwa kugombea. Kwa hiyo, wale wameonyesha imani kwamba yule ambaye ameteuliwa haswa ndiyo waliye mkusudia. Hivyo nawashauri Watanzania wenzangu wote wa vyama vyote kwamba, sasa hivi ni kutoa kura nyingi kwa Mheshimiwa Jakaya Kikwete wa Chama cha Mapinduzi ili yale madeni yaliyobakia tuweze kusamehewa yote.

Nianze moja kwa moja kuchangia kuhusu suala la elimu. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kilolo ambao haswa ndio walionileta hapa niweze kuwatetea. Nilipoingia kwenye Jimbo la Kilolo lilikuwa ni Jimbo lakini baada ya muda mfupi *Inshallah* tulipata kuwa Wilaya, kwa hiyo, nawashukuru wao na Serikali yetu.

Baada ya kupata Wilaya tuligundua kwamba shule ya Sekondari tulikuwa nayo moja tu. Sasa hivi ninaposimama hapa mbele yenu ni kwamba kila Kata ina Shule ya Sekondari, kwa hiyo, tuna Shule za Sekondari zaidi ya 16. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa ushirikiano wao ambao wameonyesha kuona kwamba suala hili la elimu linapewa kipaumbele katika Wilaya ya Kilolo.

Lakini ushauri wangu kwa Wizara ya Elimu ni kwamba fedha si nyingi sana, hazitoshii lakini zile ambazo zipo zifike kwa wakati unaotakiwa, kwa sababu fedha zile kufika mashulenii kwenye huu mpango mpya wa MMES, zinacheleweshwa sana. Kwa hiyo, zinawakatisha sana tamaa wananchi ambaa wamekusudia kutumia nguvu zao kushirikiaana na Serikali kujenga sekondari.

Pia ningeomba awamu hii basi tujikite zaidi katika ujenzi wa mabweni kwa sababu jiografia za vijiji vyetu ni mbaya, ili mtu afike shulenii inabidi mara nyingine atembee saa tatu mpaka nne. Sasa kwa watoto wa kike wanaweza wakapata vishawishi ambavyo havifai wakashindwa kumaliza shule. Kwa hiyo, ningefikiria kwamba tuanze na mabweni basi ya watoto wa kike ili tuweze kuokoa kizazi hicho.

Pia ningeweza kuchukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwenye suala la kilimo cha umwagiliaji, kwa sababu kilimo cha umwagiliaji ndicho kilimo ambacho chenye uhakika. Nichukue nafasi hii pia nimpongeze sana Mheshimiwa Leonard Shango, kwa sababu yeeye amekuwa kwa kweli mtetezi sana wa malambo na uvunaji wa maji ya mvua. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru sana Wizara ya Kilimo kwa jinsi ambavyo wamefanya kazi nzuri kwenye Jimbo la Kilolo. Wameweza kujenga *intake* za maji nzuri kwenye sehemu za Nyazwa, Ilindi, Magana na Ruaha Mbuyuni na sasa hivi wananchi wanamsubiri Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aende akafunguwe kabla Bunge hili halijaisha, kwa sababu miradi ile imekwisha na *zimetumika* fedha nyingi. Lakini nichukue nafasi hii pia niwashauri wananchi ambaa wanakaa kwenye vyazo vya maji kwamba kwa kweli wanatakiwa waondoke mara moja ili wananchi waone umuhimu wa kutumia maji yale bila matatizo.

Pia nichukee nafasi hii nimshukuru sana Waziri wa Maji na Mifugo kwa jinsi ambavyo amekuwa akihamasisha utunzaji bora wa mifugo pamoja na uchimbaji wa malambo. Kwa sababu bila hivyo kwa kweli baada ya miaka kumi au kumi na tano ijayo, duniani tutakabiliwa na upungufu mkubwa sana wa maji na tusiache kuona kwamba maji yote yanakwenda baharini hayana kazi, tujifunze jinsi ya kuyavuna, tuyatunze. Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo aliwahi kuwapeleka baadhi ya Wabunge kule Misri, walijiona wenye jinsi wananchi wa Misri wanavyowezza kuyatunza maji, pamoja na kuwa na jangwa lakini wanalima mwaka mzima bila ya kuwa na wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafsi hii pia niweze kuzungumzia habari ya mikopo kwa wakulima. Kama hatutawawezesha wananchi, kwa kweli umaskini utaendelea kuwepo. Sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri Benki ya *TIB* ibadilishwe mara moja iwe Benki ya Wakulima ili wananchi wa kawaida waweze kukopa kwa ajili ya kilimo. Kwa sababu kwa Benki za kawaida mwananchi wa kawaida akiende kukopa sio rahisi kwa mwaka mmoja akarudisha. Sasa mimi nafikiri hilo kwako uonddoke ukiwa umeliacha vizuri ili sisi tuendelee kukuombea na mambo yako yandelee kukunyooke. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TASAF*, nichukue nafasi hii pia niwapongeze sana wenzetu wa *VTTP*, wamefanya kazi kubwa sana kwenye Jimbo la Kilolo lilikuwa *pilot area*. Barabara nyingi kwa kweli hazina matatizo zinapitika bila matatizo, ujenzi wa madaraja na bahati nzuri sana mradi ule kwenye Wilaya za Iringa msimamizi ni mama, anaitwa mama Maleko ameweza kusimamia vizuri. Kama unavyojuwa wanawake wakipewa kazi kusimamia walio wengi wanafanya vizuri na mradi wa *TASAF* pia. Lakini kitu ambacho ningeomba nitoe ushauri ni kwamba kuna wenzetu wa *TASAF* wametujengea, tumesaidiana tumejenga Zahanati, madarasa na baadhi ya barabara. Lakini sasa Mheshimiwa Waziri wa Afya yuko hapa kwamba Zahanati zilizojengwa zimejengwa lakini hamna wauguzi wala hamna dawa. Sasa wananchi wanashindwa kuelewa kwamba nguvu zetu zote tulizotoa zinakuwa hazina maana. Kwa hiyo, ningekuomba Mheshimiwa mama yetu uagize mara moja wapelekwe waganga kule Isagwa na Udekwa haraka ili wananchi kwa kweli waone kwamba Mheshimiwa upo unawajali, wanaokufa wengi ni akinamama wenzio. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu inabidi wabebi wagonjwa, machela kwa ajili ya kwenda kujifungua mbali sana. Kwa hiyo, ningefikiri Mheshimiwa Waziri wa Afya, sio mbaya ukapiga simu kesho uongee na Mganga Mkuu pale Iringa ili akinamama wale wasiendelee kufa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia nichukue nafasi hii nizungumze habari ya mawasiliano kule kwenye Wilaya ya Kilolo. Mawasiliano mambo siyo mabaya sana, pale Ilula ambapo walikuwa wanapiga kelele sasa hivi mawasiliano ni mazuri ya *Celtel*, lakini Makao Makuu ya Wilaya hakuna mtandao. Inabidi upande juu ya mti ndipo uweze kupata mawasiliano, sasa itakuwa si vizuri na ahadi ya Serikali yetu ni kwamba kila kwenye Makao Makuu ya Wilaya mawasiliano yatapelekwa na miundombinu itapelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kwamba si vibaya kama Mheshimiwa Profesa Mark Mwандосya, ukatufikiria fikiria kwa sababu ndio njia ya kwenda nyumbani hiyo. (*Makofi/Kicheko*)

Kuhusu miundombinu, nichukue nafasi hii kwa kweli nimpongeze Mheshimiwa John Magufuli kwa kazi nzuri ambayo ilikuwa ikifanyika. Lakini ahadi yako na wewe kwamba Makao Makuu barabara itakwenda kutoka Ilula kwenda Mlafu, Wotaisoli, Isagwa, Ipalamwa, Mkaranga, Kising'a, Lulanzi mpaka Kilolo hiyo ndio njia yenye. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa kama utaweza uhakikishe hiyo barabara unatoka ikiwa imeanza. Mwenzetu Mheshimiwa Hamza Mwenegoha siyo mbaya hata ukapita tu kule na wewe tutakupa mambo mazuri ya kule, tutakupa eneo na wewe. Wakikuona tu watapata matumaini na tutakuombea mambo yako yakunyooke. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la umeme, tunakuja na kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya. Sasa ili vijana wale wajiajiri tuhakikishe umeme vijijini unafika. Kwa sababu kule Kilolo ni kwamba mazao sasa hivi tunavyozungumza yanaharibika kwa sababu ya kukosa usafiri, kukosa kusindikwa. Sasa tungefikira kwamba ni vizuri sasa tukapeleka umeme, tukatengeneza miundombinu mizuri na masoko ili nyanya ile ya Ilula isiharibike, matunda yale ya Kilolo yasiharibike.

Mwisho kwa kweli kwa kuwa imeonyesha dalili kwamba tutasamehewa madeni yetu hawa wazee wa Afrika Mashariki, mimi nafikiri siyo vibaya Mheshimiwa Basil Mramba ukaongeza kidogo kiwango. Kwa sababu ukifanya hesabu vizuri kwa kweli ni vizuri mmewasaidia, lakini bado pesa watakayopata ni ndogo sana. Wanadai kwa muda wa miaka 28, hebu fikiria miaka 28 ni muda mrefu. Mimi nafikiri hata mara nyingine hizi mvua zimekuwa hazinyeshi vizuri kwa sababu ya masikitiko ya hawa wazee. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, ni vizuri tukawasaidia kwa sababu ukiwalipa kwa kupiga hesabu ya dola 8 kwa wakati ule kwa kweli kabisa utafanya hawa watu wazidi kuumia zaidi.

Kwa hiyo, mimi nafikiri tuwasaidie, kwa sababu sisi timesamehewa na sisi tuongeze pale kidogo na tuwalinde kwa sababu wale wenzetu walifanya kazi hapa tulipo ndio walipotuleta. Kuna methali moja ya kule kwetu Iringa inasema kwamba, siwezi kusema kwa kihehe nitasema Kiswahili, kwamba kule Iringa tunatega wanyama kwa kutumia mitego sasa mnyama akishakamatwa na mtego usikimbilie kwenda kufurahia, kubusu yule mnyama, busu mtego. Sasa hawa wazee wa *East Africa* ndio mtego wenyewe kwa hiyo, tunawasahau, tunabusu nyama. Nashukuru naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami kuchangia hoja hizi zote mbili. Kabla ya hapo ningependa kutoa pongezi kwa wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa MKURABITA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kupata nafasi hii ya kuchangia hoja ya Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na ile ya Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil Mramba. Naunga mkono hoja zote mbili mia kwa mia na pia nawapongeza wataalam wahusika na maandalizi ya hotuba hizi zote nzuri.

Awali ya yote pia ningependa kwa niaba ya wananchi wa Liwale kutoa pole kwa ndugu zetu wananchi wa Kilombero kwa kufiwa na Mbunge wao Marehemu Abu Kiwanga. Kwa kweli wananchi wa Kilombero tuna udugu mkubwa sana na wananchi wa Liwale kwa hiyo, msiba huo umetufika sisi pia.

Nachukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kugombea nafasi ya Urais katika uchaguzi utakaokuja. Vile vile naipongeza awamu hii, awamu ya tatu ambayo iko chini ya Rais Benjamin William Mkapa, kwa kazi kubwa iliyofanya ya kimaendeleo nchini kwetu. (*Makofi*)

Hata hivyo nachukua nafasi hii kupongeza awamu ya kwanza na awamu ya pili kwa kuwa hizo ndizo chimbuko la maendeleo haya ya awamu ya tatu. (*Makofi*)

Vile vile natanguliza pongezi kwa awamu ya nne kwa vile itaanza na nguvu mpya na ari mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Bajeti ya mwaka huu ina malengo mazuri endapo tu kama itatekelezeka. Hivyo basi ningetaka nichangie katika maeneo machache yafuatayo, mojawapo ikiwa afya, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kununulia dawa kwa ajili ya waathirika wa UKIMWI. Ninachokiomba katika suala hili au katika maandalizi haya ni kwamba dawa hizi zisirudie mijini au zisiwe zoezi la watu walioko mijini, ziende mpaka vijijini.

Matangazo ya UKIMWI yamewekwa mpaka vijijini hivyo ningeomba dawa hizi ziwafikie walengwa walioko vijijini pia. Maeneo mengine sasa hivi wanasema dawa hizi zitapatikana tu Mikoani, hospitali za Mikoa kwa mfano Mkao wa Lindi ina maana itapatikana Lindi. Ni kilometra 250 kwenda, kwenda na kurudi ni kilometra 500, wananchi wa kawaida na ugonjwa wa UKIMWI na safari ndefu kama hiyo inazidi kumdhoothifsha. Kwanza hana uwezo, pili atagharamia kulala hotelini au kwenye *guest* hivyo vyote hana uwezo.

Ningeshukuru sana kama Serikali ingeandaa mipango mizuri ya kufanya angalau *clinic, mobile clinic* ya kwenda kuwashudumia wananchi walioko vijijini. Kuhusu malaria nashukuru kama kuna mikakati ya kupiga vita ugonjwa wa malaria, Tanzania tusitegemee sana ngao kwa kuwa ngao ina muda wake wa kutumika mpaka uende ukalale ndani ya chandarua, na wananchi wa Tanzania siyo jeshi kwamba utawalazimisha wakalale saa mbili ili wasiumwe na mbu, watakuwa na kazi nyingine za kufanya kiasi cha kwamba wataumwa na mbu huko nje.

Pia ningependekeza mbali ya kufikiria tiba peke yake na ngao pia pangekuwa na utaratibu sasa wa kuharibu mazalia ya mbu kitu ambacho kilikuwa kinafanyika wakati wa ukoloni na baada ya Uhuru. Sielewi kwa nini tumeacha mtindo huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika takwimu ambazo tumeonyeshwa katika Bajeti hii inaonyesha kwamba mazao asilia Tanzania yameongezeka kwa mauzo ya nje. Kwa mfano korosho 62.9, tumbaku 44.3, pamba 60.2 kwa bahati mmeefikiria pia kutoa ruzuku kwa ajili ya pembejeo ya mazao hayo, tunashukuru sana kwa hilo. Lakini kwa upande wa korosho naomba mtoe ruzuku kwa pembejeo aina zote linalofanyika sasa hivi ni kwamba wametoa ruzuku kwa pembejeo ambazo zinahusiana na maji maji au dawa za maji maji na sio *sulphur*, kwa nini mnaagiza *sulphur* kama haina ruzuku? Hata kwa kigezo kwamba *sulphur* ina madhara, sawa hata asprini ina madhara kwenye ardhi. Hakuna dawa yoyote au hakuna *chemical* yoyote ambayo itakuwa haina madhara.

Kwa hiyo, mimi ningeomba kabisa *sulphur* ambayo wananchi wengi au wakulima wengi wanaitumia pia ipewe ruzuku ili waweze kuinunua kiurahisi zaidi na waweze kutumia kiurahisi zaidi. Hiyo itakuwa ni *challenge* kubwa pia kwa wataalam wa kilimo kama inaleta madhara kwenye ardhi basi watafute mbinu ya kuona kwamba madhara hayo yasitokee kama inavyofanywa na ndio maana kuna sehemu za utafiti. Sasa hizo tafiti kama hamwezi kuziendeleza kwa kulingana na hali halisi basi itakuwa ni vigumu. Upande wa kilimo naona hili sasa hivi limeshakuwa tatizo, kusema kweli kuwa na mvua nyangi kwa Tanzania ni tatizo na kuwa na mvua chache Tanzania ni tatizo.

Sasa sijui kama tuna uwezo wa kum-*convince* Mwenyezi Mungu atueletee mahitaji ya mvua yale tunayotaka na kama hatuna basi inatakiwa sisi wenyewe kiutalam tuone ni jinsi gani tunaweza kuwashauri wakulima wetu watumie mvua nyingi kwa kupanda nini? Na mvua chache kwa kupanda nini? Mapema iwezekanavyo. Kama utafiti kweli unafanyika Tanzania basi tujiveke tayari kupambana na hali kama hiyo na siyo kungojea tu mvua ambazo hatuna uwezo nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuwalipa watendaji wa vijiji. Lakini inanisikitisha sana kuona tumewasahau Madiwani hawa. Madiwani wengine wapo katika Halmashauri ambazo kusema kweli hazina uwezo naangalia Waziri wa Fedha anavyozungumzia Halmashauri labda anazungumzia Halmashauri za Temeke, Kinondoni ambazo zina Bandari na viwanda, lakini Halmashauri zingine hazina miundombinu aina yoyote ya uchumi. Kwa hiyo, ziko katika hali ngumu sana, basi angalau katika Bajeti hii tungetenga hata fedha kwa kuwa baada ya miaka mitano Madiwani hawa wanaingia tena uchaguzi. Basi angalau tuwapangie fedha ambazo wangepewa kiasi fulani kutokana na utumishi wao wa miaka hii mitano tutafute *formular* ya kuweza kuwapa hizo, endapo kama Halmashauri zao wanawenza kuongezea chochote basi wawaongezee kile kidogo kitakachopatikana.

Nashukuru sana kwa upande wa Liwale pia elimu tumeweza kuboreka kwa kipindi hiki na hii yote kutokana juhudhi iliyofanywa vizuri na Serikali hii ya awamu ya tatu. Zamani ilikuwa Mbunge mmoja wa Liwale Jimbo moja Sekondari moja, lakini sasa ninavyosema tunafungua Sekondari tano. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hayo yote yasingepatikana bila kupata ushirikiano mzuri na Wizara husika katika Awamu hii ya tatu nashukuru sana, pia Sekondari za Kata ziko mbioni kujengwa. Serikali pia imetenga fedha kwa ajili ya mafao ya watumishi wa waliokuwa wanafanyakazi Afrika Mashariki, kama nakumbuka vizuri wanasema bilioni 50, sijui kama naweza kukumbuka tena vizuri madai waliyokuwa wanayazungumzia wao ilikuwa ni bilioni 400 sasa hii *10 percent* ambayo wanapewa sijui itakuwa inatumika vipi na sijui patakuwa na utaratibu gani, Mheshimiwa Waziri itabidi hapo utupe maelezo mazuri kwa kuwa mimi hata kwenye Jimbo langu wapo Watumishi wa Afrika Mashiriki ambao wamestaafu hawajapata chochote.

Kwa hiyo, ningombo uelezee utakapo-*wind up* namna gani niende nikaelimishe jinsi ya kugawanya hizo bilioni 50 ambapo mategemo hayo yalikuwa bilioni 400. Kutokana na msamaha tunaopata kusema kweli na maisha yaliyokuwa magumu kwa nini tusifumbe macho na kuamua sasa kima cha chini kiwe 100,000. Kuna tatizo gani? Maana yake sasa hivi 60,000 hizi kusema kweli hazimsaidii mtu yoyote, tunajidanganya na hakuna sababu ya kusema kwamba tunafanya lolote kwa wananchi hawa. Naomba kima cha chini uone njia ya kuongeza mpaka ufikie 100,000 angalau.

Kwa upande wa mawasiliano kipindi hiki nashukuru sana awamu ya tatu imenisaidia kilio cha wana Liwale na pia nampongeza Waziri wa Mawasiliano Profesa Mark Mwandosya, ambaye ametusaidi sana kwa karibu akishirikiana nami hakuchoka

wakati wote ambao nilikuwa nafuutilia simu kwake hakuwa na hasira hatimaye tumeweza kupata *Buzz*.

Sasa hivi tunaitwa Liwale ni wajanja, na hata hivyo *Celtel* iko mbioni nadhani kufika mwezi ujao itakuwa nayo imeshaanza kufanya kazi. Naomba Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, usiketi chini tumalizie ngwe kwa kufungua *Celtel* mapema iwezekanavyo. Kwa upande wa barabara pamoja kwamba barabara Nangurukuru -Lindi inatengenezwa, lakini sisi kilio kikubwa kutoka Nangurukuru kwenda Liwale kilometra kama 200 na kitu hivi na kutoka Liwale kwenda Nachingwea kuna eneo la mchanga, matengenezo yanayofanywa kusema kweli yanasaidia tu kwa muda fulani kwa zile sehemu korofi na kwa bahati nzuri sisi tunapata mvua na kwa vile Mwenyezi Mungu hatuwezi kumtengea sehemu za kunyesha mvua na kuacha barabara isinyeshewe ili wananchi waweze kutumia. Naomba Serikali iongeze juhudhi ya kuboresha barabara hiyo ili tuweze kuitumia wakati wote na itakuwa nafuu kwa wananchi wa Liwale. Kutoka Liwale kwenda Nachingwea kuna *portion* ya kilometra kama 30 ambazo ni mchanga hiyo inatuongeza gharama kwa kuwa hata magari yanayokwenda kule wanapandisha nauli na pia hata wale wanaokwenda kununua mazao yetu wanunuua kwa bei nafuu kwa kujali eneo lile kwa kusema barabara ni mbaya.

Kwa hiyo, naomba ili wakulima wa Liwale waweze kunufaika basi maeneo hayo yatengewe fedha za kutosha ili barabara zake ziweze kuboreka vizuri. Kuhusu maji, namshukuru sana Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa juhudhi zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja hii ya hotuba za Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, katika hoja hizi ambazo kwa hakika ni funga dimba la kipindi kirefu ambacho tulikianza katika matayarisho ya kuboresha uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vile vile nichukue nafasi hii nami nitoe rambirambi kwa familia, ndugu na jamaa wa Waheshimiwa Wabunge waliotangulia mbele ya haki. Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Kilichofanyika ni kuwa wao wametangulia lakini sote sisi tuko katika safari moja tunaelekeea huko huko.

Pili, niwapongeze viongozi wa vyama mbalimbali ambao wameshateua wagombea wao wa urais. Lakini kwa wale waliokuwa wanasubiri eti Chama cha Mapinduzi kitamteua nani ili baadaye wao wateue mtu wao ashindane na yule atakayeteuliwa na Chama cha Mapinduzi wao walie tu, kwani ni dhahiri ya kuwa hawana mtu, hawana kitu wala hawana mpango wowote. Huo ni mchezo wa danadana ambao hauna magoli na wananchi kwa hakika wameshautambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii, nimpongeze ndugu yetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume na

Makamu wa Rais kwa kuteuliwa kushika bendera za CCM kugombea viti hivi muhimu vya Taifa letu. Nina hakika kabisa viti hivi ni vyetu na tutavichukua kwa ulaini. (*Makofî*)

Kwa namna ya pekee, napenda nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa ushindi maarufu na wa kutakasa pale Chimwaga. Ni dhahiri hata kwa Wapinzani wetu hapa kuwa uchaguzi wa Oktoba utakuwa kama ni *formality* tu, ni kama mchezo wa kufumba na kufumbua. Nawashukuru Wapinzani kwa kutambua hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, ushindi huu wa Mheshimiwa Jakaya Kikwete, utakuwa ni *forgone conclusion*. Lakini tayari tumeshaona dalili za kijinga zisizokuwa na misingi za Wapinzani za kujaribu kutaka kumpakazia na kumbambikizia mambo na kashfa ambazo hazimhusu hata kidogo. Hizo zote ni jitihada za siasa za kushindwa lakini itakapofika mwezi Oktoba sisi tutakachofanya ni kupiga dafrao na tutawafanyia kama alivyofanyiwa yule baniani na jirani yake alipokuwa anagombana naye akamwambia: “Hebu piga toto tajama, bu. Hebu piga mama tajama, bu tukapiga. Hebu piga mimi tajama,” tukapiga na ndivyo tutakavyofanya. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgombea wetu kwa hakika ataingia Ikulu akideka na atadeka kwa jinsi siku hadi siku tunavyoolekea Oktoba tunaona namna wananchi wanavyonyanyuka na kujaribu kumbeba huyu mkombozi wao. Vile vile atadeka kwa kazi nzuri ambayo imefanywa na Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa na Serikali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana. Ni kwa wajihî wake mwema na maneno yake mazuri na akili yake iliyokuwa na busara na vile alivyokuwa na *dexterity* ya jinsi alivyokuwa na *public relation* nzuri na Watanzania wenyewe, wahisani na marafiki zetu huko na jinsi alivyoweza kutumia *diplomatic acumen* yake ndio maana tukaweza kunyanya uchumi wetu na kuweza kusamehewa madeni kama tulivyosikia kwa mara ya pili ndani ya miaka mitano. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, popote pale alipo Mheshimiwa Rais mimi nasema ahsante sana. Kwa maana hiyo basi, mgombea wetu atashika nchi hii tayari misingi ya uchumi na hali ya uchumi ikiwa nzuri ya kuwa ndani ya Hazina tuna pesa za kuweza kuendesha nchi hii kwa zaidi ya miezi minne na sidhani kama kuna mtu amebahatika toka tupate uhuru kuwa na hali nzuri ya kiuchumi kama hiyo wakati anapoingia katika awamu yake. Kwa hiyo, atashika nchi hii kuiendeleza sio kuianza kwa alifu kwa kijiti. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hili, Serikali hii lazima imsaidie mgombea wetu tena lazima imsaidie sana na wakati wenyewe ndio huu. Pamoja na kuwa ataingia Ikulu asiingie huku amebeba mizigo (*access luggage*) ambayo siyo yake aingie, awe mwelesi ili utendaji wake wa kazi usiwe na dosari wala mushkeli wa aina yoyote. Tusimbebeshe *IPTL* sio mizigo wake, tusimbebeshe *Songas* siyo mizigo wake, tusimbebeshe *TTCL* sio mizigo na tusimbebeshe *NBC* sio mizigo wake. Mizigo hii siyo yake na Serikali iseme hivyo sasa ili iweze kumsaidia. (*Kicheko/Makofî*)

Si hivyo tu wananchi wana haki hatimaye wajue, tumeshazungumza mambo haya mara nyingi sana lakini kwa hakika hatujapata majibu ya kuridhisha. Nani alihusika katika mambo haya kuandika mikataba mibaya, vipi *cabinet* imeweza kuzugwa hata ikaridhia mambo kama haya, tuweze kuyajua mapema. Miradi ambayo ilidhaniwa inusuru kwa mashirika kuweza kubinafsishwa, kwa hakika yametingwa na mambo ambayo yanaweza kuhisiwa kuwa ni ya udanganyifu na siyo ukweli na kuwa ni mzigo mkubwa kwa wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika hizi za majeruhi tuelenze na kama kusameheana sisi Watanzania ni watu wakarimu tutasameheana lakini ni vema tukajua mapema nini kilichotokea ili maruhani haya tuyamalize kabla ya kuingia katika Awamu ya Nne. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuwa mikataba mibovu ambayo tumeandikiana na mashirika tuyaita, tukae nao upya mezani wala tusione haya ni mambo ambayo yanafanyika nchi za nje.

Nitoe mfano mmoja mzuri. Kuna kampuni moja ya Australia ambao walikuwa wanatafuta dhahabu hapa wamekwenda Eritrea walipofika Eritrea kutafuta dhahabu wakakuta *deposits* nyingi mno za *copper*. Wakaanza kazi wakamima mamilioni ndani ya wiki moja kampuni ile ikatajirika wakaweza kuingia katika *stock exchange* na kadhalika kwa zile *deposits* walizozigundua. Wakaingia mkataba na Serikali ya Eritrea. Baada ya muda mdogo kukawa na *shuffle* na Waziri wa Nishati akabdalishwa akaingia Mwanajeshi mmoja. Mwanajeshi yule akasema simamisha kazi sasa hivi funga virago mrudi kwenu. Wale jamaa wa Australia wakachanganyikiwa. Baada ya mwezi mmoja wakabembeleza wao wenyewe wakutane na Serikali wakae kitako ili wawewe kuzungumza kulikoni? Wakawaambia ninyi mnatuona sisi maskini kwa hiyo, mmetuletea utajiri basi sisi tuko tayari kufa na umaskini wetu vipi mtatupa *royalty* ya 2.5% au 3%? Wakawaambia fungeni virago muondoke. Wakataka wazungumze. Serikali ya Eritrea ikasema *10% or nothing*. Wale jamaa wakakaa pembedi, wakashauriana wakakubaliana kulipa *10% royalty*. Kwa hiyo, si kitu kigeni. (*Makofi*)

Kama anavyosema Rais, Mheshimiwa Benjamin Mkapa huo ndio ujasiri wa uongozi. Yeye mwenyewe amekuwa mjasiri sana na ameonyesha ishara ya ujasiri mara nyingi katika nchi yetu. Yeye mwenyewe Mheshimiwa Benjamin Mkapa anaita *courage of leadership*. Lakini sio yeye peke yake. Juzi juzi hapa tumemuona Mheshimiwa Edward Lowassa na yeye vile vile ametumia ujasiri katika uongozi. Alishatufungulia mlango sisi tunasita kitu gani. Mikataba hii tuitishe tuweze kuzungumza upya na kuzungumza ni kitu halali kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nimewahi kuona kwenye *television* na kusikia kwa masikio yangu, kiongozi mmoja wa Tanzania kakaa anazungumza upande mmoja kuna *lord* mmoja kutoka Uingereza upande wa pili maskini ya Mungu yuko kiongozi mmoja wa PSRC anamwambia unaona umetudanganya kumbe TTCL thamani yake ni dola milioni 5 tu. Nani amesema hivi? Jamaa gani sijui aliyekaa Uingereza. Anatuambia sisi thamani ya TTCL ni *5 million dollars* lakini wao walipotoa

*tender* ya dola milioni mia moja na ishirini walikuwa wanafanya nini, si walikuwa wanajua thamani yake? Sio wao peke yao kulikuwa na kampuni nyingine ika-*tender* dola milioni 100 na wao vile vile walikosea? Haiwezekani! *Vodacom* wapo hapa wanafanya kazi na wao walitenda milioni 80, je na wao vile vile walikosea? Haiwezekani! Lakini unamkuta kiongozi mmoja anamsuta kiongozi mwingine wa Tanzania anasema ya kuwa mmetudanganya. Kwa nini? Kama chiriku anaiga yale yaliyosemwa London.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nasema ufile wakati kunyanyaswa namna hii na kunyonywa namna hii na makampuni binafsi uchwara ya nje, yanakuja hapa yanatuzunguka yanatuzidi akili, tufikie kikomo tusiendelee tena. *This is like a rape of our country.* Kwa kweli nchi yetu inabakwa kiuchumi. (*Makofi*)

### **MBUNGE FULANI:** Sawa sawa!

**MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF:** Ndio, inabakwa na mbaya zaidi kuna watu mionganoni mwetu tunawasakiad katika ubakaji wa nchi hii, tuzuie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi akinamama, kina dada mimi ni rafiki yenu kwa kweli nakufirikieni sana, huu mchezo wa kubaka huu ambao lazima tuulaani, tuulaani na tuwaadhibus vikali sana wala tusiusamehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano kama mwanamke anakabiliwa na tatizo hili la kubakwa ana kitu kimoja kati ya viwili ambavyo anaweza kufanya. Moja anaweza kupiga kelele aombe msaada kama vile sisi tunavyopiga kelele kwenda huko Ulaya, *arbitration* ni njia za kupiga kelele. Akishindwa atachukua *step* ya pili atajaribu kujihami kwa hiyo *ata-struggle* ili kitendo kile kisifanyike lakini atakosea sana ikiwa atageuza uso akasema, wewe endelea tu unapata dhambi, Mungu anakuona.

*Stage* ile yule mtu hamjui Mungu tena na sisi Tanzania ndivyo tunavyofanya hivyo tunawaambia, aah, ninyi endeleeni tu Mungu anakuoneni. Kwa hiyo, mimi nasema tuache, hebu tuheshimu nchi yetu, tuheshimu wananchi wetu, tuwazingatie, tuwawakilishe vizuri tuone ya kuwa neema inakuja katika nchi hii. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme tu ya kuwa naunga mkono hoja hii, hoja hii ni nzuri, hoja hii kwa leo kwa hakika haina mbwembwe wala nini, ni *culmination* ya kazi nzuri kama nilivyosema tulioianza miaka kumi iliyopita. Namshukuru Mheshimiwa Basil Mramba kapewa kazi nzuri kaifanya, namshukuru Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda kapewa kazi nzuri ameifanya na kwa hakika ni wao ambao wamejitahidi kunawirisha sura ya nchi hii, kunawirisha sura ya wananchi wa nchi hii na wao ndio waliosaidia kwa hakika hata nchi za nje zikatutizama sisi vizuri kuona kuwa tunafanya kazi nzuri, tunaimarisha uchumi wetu na tunaendelea vizuri *on the right path*, hata mashirika ya nje ya Benki, *IMF, World Bank* wahisani wetu wale ambao *tunabilateral relationship* nao, wale wanaotutakia kheri na kwa hakika hata wananchi wa nchi hii wameanza kuona ya kuwa ama kweli Serikali ya CCM inafanya kazi kunyanyua nguvu za kiuchumi za nchi hii na kuweza kuhudumia wananchi wa nchi hii. Kama Wapinzani hawaoni hayo, watajiju, lakini kila mtu anaona. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nasema tena kuwa Bajeti hii ni nzuri na naiunga mkono na nawatachia Mawaziri hawa wawili kila la kheri, ahsanteni. (*Makofit*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Wabunge ambao wamebaki kuchangia ambao wamo humu ndani ni hawa wafuataao, Mheshimiwa Damas Paschal Nakei, Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na Mheshimiwa Mariam Mfaki, ndio walioko humu ndani na ndio watakaochangia. Mheshimiwa Damas Nakei.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii jioni hii ya leo ili nami niungane na Wabunge wenzangu kuchangia katika hoja hizi mbili hoja ya Waziri wa Fedha na hoja ya Waziri wa Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, labda niseme naunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia moja. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kutoa salaam za rambirambi kwa wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kuondokewa na Mbunge wao Mheshimiwa Marehemu Abu Kiwanga. Namwomba Mwenyezi Mungu amweke mahali pema peponi. *Amin.*

Vile vile napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kishindo na Chama cha Mapinduzi kugombea Urais katika uchaguzi Mkuu ujao, ye ye akiwa pamoja na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, mgombea mwenza. Lakini pia nampongeza Mheshimiwa Rais Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa kuwa mgombea wetu wa Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi huo wa Oktoba. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye hoja zenyewe, kwanza niwapongeze Mawaziri wote wawili pamoja na wasaidizi wao kwa hotuba nzuri, kwa Bajeti nzuri ilioandaliwa vizuri. Bajeti hii kila mmoja wetu aliyesimama amezungumza habari ya utulivu wake, ni Bajeti nzuri ambayo kweli ina sifa ya kuwa Bajeti ya kuhitimisha Awamu ya Tatu ya uongozi wa nchi yetu, uongozi wa Rais Benjamin Mkapa. Tunasema basi ni Bajeti ya kihistoria katika utulivu wake na jinsi ambavyo imeelezea mafanikio makubwa katika miaka hii kumi ya uongozi wa Awamu ya Tatu katika nchi yetu.

Tunaipongeza Serikali kwa jitihada za kuleta maendeleo kwa wananchi wetu katika maeneo ambayo yametajwa baadhi yakiwa ni uchumi wetu kukua kwa asilimia 6.9 kwa mwaka huu, makusanyo ya kodi kupanda kutoka shilingi bilioni 70 mwaka 2000 na kufikia shilingi bilioni 145 mwaka jana, huduma za kiuchumi na kijamii zimeboreshwa, kila mmoja wetu hapa ni shahidi. Kwa ujumla leo nchi yetu tunakopesheka katika taasisi za fedha za Kimataifa. Tanzania leo ina heshima kubwa mbele ya Mataifa, hadhi yake imepanda na inaonekana vizuri katika ramani ya dunia, yote hii ni kutokana na jitihada

nzuri, kubwa na za kuthubutu za Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, tunampongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa taarifa za kusamehewa madeni. Hizo ni taarifa nzuri na kwa kweli ni za kufanya kazi. Ni fursa ambayo itatuwezesha sisi Watanzania sasa kukimbia katika safari ya kuelekea kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini labda niulize kuhusu mafanikio ya Dira ya Maendeleo yetu tuliojiwekea ya mwaka 2025. Leo tuna miaka mitano muda huo wa dira ya miaka 25 ya maendeleo yetu kuondoa umaskini katika nchi hii. Miaka mitano maana yake tuna asilimia 20 ya muda ambao tumejiwekea ili kuhakikisha kwamba umaskini katika nchi hii umetokomea kabisa.

Sasa sina hakika kama tukiangalia nyuma miaka mitano mpaka leo tunafanana na kipindi hicho ambacho kimeshatumika au tunapaswa sasa kuangalia na kuweka mkakati upya ili kuhakikisha kwamba tunaenda kadri ya muda tuliojiwekea na kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2025 kweli Watanzania wako katika hali nzuri zaidi kuliko ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo moja muhimu katika maendeleo yetu ni kodi. Napenda niipongeze *TRA* kwa kazi nzuri ambayo inaifanya. *TRA* wanafanya kazi nzuri na leo Watanzania wengi zaidi wanalipa kodi, wafanyabiashara wengi zaidi wanalipa kodi. Naamini kwamba wakati utafika itakuwa kulipa kodi ni wajibu na kukwepa kodi ni aibu. Mtu mwenyewe ajue hilo lakini bado hiyo ni kazi kubwa ambayo iko mbele yetu lazima tuifanye na kwamba wigo wa kodi ni lazima upanuliwe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu kwamba kuna haja ya kuangalia mahusiano kati ya walipa kodi na watoza kodi ambao ni *TRA*. Je, uhusiano wao ukoje ni wa ushirikiano au ni wa kukimbizana? Mtu mmoja ni bosí na mwingine ni kati ya bwana mkubwa na bwana mdogo. Ushauri wangu ni kwamba mahusiano yao yawe mahusiano mazuri kuhakikisha kwamba kutegemeana kwao kunadhihirishwa katika kushirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine wafanyabiashara au mtu anawenza kuwa kutokana na kutokuelewa kwake akawekewa kodi kubwa zaidi kwa sababu tu ameshindwa kuweka mahesabu yake vizuri. Nafikiri ni vizuri *TRA* vile vile iboreshe hali hiyo ya kuhakikisha kwamba kunakuwa na ushirikiano mzuri kati yao ili wawewe kupanga kodi ambayo inalipika kuliko kufika mahali ambapo mtu anashindwa kulipa kodi na hatimaye biashara inafungwa na hatimaye hakutakuwa na kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la madini. Nchi yetu inajivunia madini. Tuna madini ya dhahabu mengi sana, ni utajiri mkubwa wa asili katika nchi yetu. Sasa napenda niishauri Serikali kwamba utajiri huo wa asili unapokuwa *exploited* uende sambamba na kushamiri kwa uchumi hususani sekta ya ujenzi, *construction industry* na hususan zaidi ujenzi wa barabara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kuwa Serikali ilekeze fedha zote za madini moja kwa moja kwenye barabara pamoja na kwamba tuna *Road Fund* lakini tuwe

na *source* hii ya madini katika eneo hili la *development budget*, fedha za madini zielekezwe kwamba barabara zote za nchi hii sasa zijengwe kwa lami isionekane ni jambo la kushangaza. Hii habari ya kiwango cha changarawe nadhani ifikie kikomo na kwamba iwe ni historia kuzungumzia habari ya changarawe, changarawe tuanze sasa kugeuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika kadri dhahabu inavyokwisha hatimaye tutakuwa hatuna kitu cha kuonyesha kwamba dhahabu hii imeishia wapi. Sasa ushauri wangu ni kwamba kuisha kwa dhahabu, maana yake itaisha, twende pamoja na kukamilika uwekaji wa lami katika barabara zote nchi hii hasa barabara za Mikoa na barabara kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itakuwa ni ushahidi baadaye kwa vizazi vijavyo kwamba kweli fedha za madini ya dhahabu matokeo yake ndio haya tunayoyaona na hakuna nchi duniani ambayo imeendelea lakini haina barabara. Kwa hiyo, suala la barabara litiliwe mkazo kadri inavyowezekana. Hilo ndio pendekezo langu kwamba ni *source* ya hakika zaidi tunapoongelea juu ya huu mfuko wa barabara unaotokana na *fuel levy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kuzungumzia suala la barabara hapa napenda sasa nizungumze juu ya ahadi ya Rais kwa wananchi wa Mkoa wa mpya wa Manyara. Leo tuna miaka mitatu Mkoa huo bado ni mpya, bado haujakomaa sawasawa. Lakini Mheshimiwa Rais aliahidi kuhakikisha kwamba kutakuwa na *accessibility* kati ya Babati Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara na Wilaya zake ikiwemo Simanjiro ambayo ni Orkesumet. Barabara hiyo inapewa fedha kidogo mno haifanani kabisa na ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Napenda Serikali ituambie kwa nini inasua sua katika suala hili la kutekeleza ahadi ya Rais lakini sio ahadi ya Rais tu kwa sababu Rais aliona kwamba kuna haja ya kuunganisha Wilaya zote na Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kuhusu afya. Tunalo tatizo la mfuko huu wa *CHF*. Katika Wilaya yangu ya Babati, *CHF* ni changa mno, ni watu wachache mno wamechangia katika mfuko huo na hili suala la mfuko wa *CHF* ni sera ya Taifa. Sasa inapokuwa mahali fulani katika nchi yetu hatuendi kadri ya sera zetu, kuna haja ya wahusika wengine kuingilia kati kama ni Wizara au nani kuhakikisha kwamba tunakwenda pamoja. Babati Mfuko wa Afya ya Jamii bado ni ndoto.

Kwa hiyo, ningependa Serikali ifahamu hivyo na inanipa changamoto kwamba jambo hili liangaliwe kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma bora za tiba na kinga upande wa afya. Hii ni kero kubwa na kwa kweli inapaswa kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa zahanati hadi ngazi ya vijiji ni njia pekee ya kuwafikia wananchi wetu walio wengi kwa huduma za tiba. Nashauri Serikali iachane na utaratibu wake wa zamani, mimi nasema ni wa kizamani wa kudhibiti ujenzi wa

zahanati kwenye ngazi ya Kata tu. Sasa hivi masharti ni kwamba huwezi kuwa na zahanati zaidi chini ya Kata na kwamba lazima ihudumie idadi fulani ya watu.

Mimi napenda kushauri Serikali kwamba twende mbele zaidi, zahanati kwa kila kijiji maadam wale wanavijiji wanaweza kujijengea zahanati zao tuwaunge mkono kwa kuwapelekea madaktari na madawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna suala la kijiografia kwamba mtu anatembea kilometra tano, kumi kwenda kutibiwa. Sasa hii haifanani na karne hii ya 21. Naomba Serikali ijaribu kuangalia sera hii ya kudhibiti zahanati katika ngazi ya Kata peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo basi, naomba zahanati katika Jimbo langu la Babati Magharibi, zahanati za Dohomu, Duru, Mandi, Meri, Ari na Qameyu zipelekewe madaktari na dawa na ikiwezekana katika mwaka ujao wa fedha. Kwa sababu hao wametumia nguvu zao kujenga zahanati hizo wakiamini kwamba Serikali sasa itawasaidia, itawaunga mkono kwa kuwapelekea madaktari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kuna zanahati ya Gidasi ambayo iko kilometra 45 kutoka mji wa Babati ambako kuna hospitali ya Wilaya. Zahanati hiyo basi ipandishwe hadhi kuwa kituo cha afya. Hii itawasaidia wananchi wa eneo hilo ambao wako mbali zaidi na kupata huduma hizi za tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo juu ya kilimo. Kila mmoja wetu hapa anayesimama anazungumzia kilimo kwa sababu ya umuhimu wake, lakini lazima Serikali sasa itafute mbinu mpya kwa sababu kuzungumza habari ya kilimo kila mwaka tunapiga *mark time* pamoja na kwamba kuna ongezeko kidogo la uzalishaji, kuna mafanikio kiasi lakini bado hatufanani na mikakati yetu ya kuondoa umaskini hususani kwa wakulima walio wengi. Bado wakulima wetu wanashindwa kumudu bei ya pembejeo hususani mbegu, bado wakulima wetu wanashindwa kumudu bei za zana za kilimo. Basi Serikali ijaribu kuona jambo hili kwamba lazima sasa wimbo huu wa kwamba kilimo bado kiko nyuma, lugha hii ifikie mahali iishe. Mabwawa ya umwagiliaji yachimbwe karibu kila eneo. Sasa hivi mvua inaponyesha maji yote yanaenda baharini badala ya kuyadhibiti na kuhakikisha kwamba maji yanahifadhiwa au mito tuliyonayo ikaboreshw na kuhakikisha kwamba maji yale yanatumika kwa ajili ya umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana na naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa dhati kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja mbili zilizoko mbele yetu, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na hoja ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba hoja, ambazo sitaki kurudia kwa sababu wenzangu wameshazipongeza sana kwamba zimewasilishwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema lolote, nianze kwa kutoa rambirambi zangu kwa kifo cha mwenzetu, ndugu yetu Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea Urais katika uchaguzi ujao. Kama alivyosema ndugu yangu pale, Mheshimiwa Mbunge wa Dodoma Mjini, sina sababu ya kurudia, nina hakika kabisa kwamba atapata ushindani wa *Tsunami* basi nadhani wapinzani watusaidie tu kujazilia zile kura ambazo watazipata kwa wananchi wa kawaida wasisumbuke kuziweka mahali pengine. (*Makofî*)

Nimpongeze pia Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza lakini vile vile nimpongeze Rais wetu Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuteuliwa tena na Chama cha Mapinduzi kubeba bendera ya CCM katika uchaguzi ujao kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, *Inshallah* Mwenyezi Mungu ajalie kila la kheri na wote watatu wapate mafanikio ya kuwezesha. (*Makofî*)

Nimpongeze Mheshimiwa Basil Mramba na wasaidizi wake na Manaibu wake wote wawili kwa kazi nzuri waliyoifanya kwenye Wizara hii na toka sisi wengine ambao tumeingia miaka mitano hii kwa kweli mwaka hadi mwaka tumeona mafanikio ambayo yamekuwa yakionekana. (*Makofî*)

Vile vile kero nyingi za wananchi ambazo zimekuwepo zimetoweka kiasi kwamba sasa Wapinzani wanasma CCM inachukua sera za Wapinzani ni kwa sababu hawana la kusema tena. Kwa hiyo, kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ya awamu hii ya tatu na hasa Mheshimiwa Basil Mramba na wasaidizi wake tunaomba waimalize vizuri na *Inshallah* waikabidhi vizuri kwenye Serikali ya Awamu ya Nne. Lakini niwaombee heri na wao wenyewe watakuwepo kwenye Serikali ya Awamu ya Nne wasiwe na wasiwasi. (*Makofî*)

Nimeshampongeza Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na ninaendelea kumpongeza lakini kwa ujumla na wataalam wote na wasaidizi wote wa Wizara hizi mbili nawapongeza kwa sababu wao ndio wamefanikisha kazi hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Rais, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, kwa kazi nzuri ambayo ameifanya kwa kipindi cha miaka kumi. Sina sababu ya kurudia ya kueleza kazi nzuri ambayo imefanywa, lakini ni kazi ambayo inaonekana ye ye mwenyewe alisema ukitaka kuona mafanikio usikae kwenye siti ya nyuma, kaa siti ya mbele uone mambo yaliyopo mbele. Sasa hawa wenzetu ambao wanakaa siti ya nyuma wanataka waone mambo ya siti ya mbele, haiwezekani. (*Makofî*)

Kwa hiyo, sina sababu ya kurudia lakini nampongeza sana ye ye na Serikali yote ya Awamu ya Tatu kwa kazi nzuri ambazo wamezifanya kiasi kwamba nchi yetu imepata heshima na inaendelea kupata heshima, kiasi kwamba nchi yetu inaendelea kupata misamaha ya madeni, kama ambavyo imepata awamu ya kwanza na safari hii tena tumepata ingawa magazeti ya leo kidogo yanatuyumbisha, yanatuambia mambo mengine

kuhusu msamaha ambao umetokea hivi karibuni ningeomba Mheshimiwa Basil Mramba, atakapokuwa ana *sum up* hii hoja yake kesho walau atupe ufanuzi kwamba mbona magazeti yanataka kuharibu kazi nzuri ambayo sisi tumeshadhani na tunaendelea kuamini kwamba tumepeata msamaha na *Inshallah* tuutumie katika hayo maeneo ambayo tumekuwa tukiyazungumzia. (*Makofi*)

Mimi kwa upande wa kutoka Singida nina kila sababu ya kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Tatu kwa sababu ni kweli kwamba Singida tulikuwa tuko nyuma lakini sasa *Alhamdulilah* mambo yanaonekana. Miradi ambayo imefanyika katika kipindi kifupi inatusaidia sasa kuuona Mkoa wetu sasa nao walau *Alhamdulilah* na wawekezaji sasa wanaweza wakaja. Nasema hivyo kwa sababu barabara hii ya kutoka Dodoma kwenda Singida ikimalizika na baadaye mpaka Mwanza basi hiyo itakuwa ni ahueni kubwa na itasaidia kuwaleta wawekezaji kwenye Mkoa wetu wa Singida kwa hilo nalipongeza sana. (*Makofi*)

Lakini vile vile tumepeata mradi wa maji wa Benki ya Dunia. Sisi Singida kule mnajua mvua mara moja tumekuwa na ukame wa muda mrefu lakini Serikali ya Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Edward Lowasa na wenzake namshukuru sana alikuja Singida, amenisaidia, naendelea kumshukuru, imetukomboa sana, sasa kazi kwetu kushamiri katika kuona kwamba tunatumia fursa hii vizuri ambayo tumeipata ya kujiondolea tatizo la maji. (*Makofi*)

Lakini vile vile Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kupitia Serikali yote hii wanatusaidia kujenga uwanja wa ndege tunauita *Singida International Airport* msiwe na wasi wasi ninyi njooni tu, uwanja wa ndege unajengwa kule *Singida International Airport*. Kwa hiyo, nina hakika Mawaziri sasa mkija msiwe na wasi wasi hamtakwama kama alivyokwama Mheshimiwa Balozi Karume juzi alipokuja, lakini mambo yanakwenda vizuri, kwa hiyo, nashukuru pia hili kwamba walau mkoaa wetu unafunguka, barabara inafunguka, uwanja wa ndege ndiyo huo, maji ndiyo hayo, simu za mkononi hazina shida. Kwa hiyo, kwa kweli tunashukuru kwamba walau Singida sasa mambo yetu nayo yanatuendea mahali pazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia Serikali kwa hatua waliyofikia ya kukubaliana na wafadhili kwamba misaada yote sasa itawekwa kwenye kapu moja na halafu Serikali yetu ndiyo ipange *priority* kwamba misaada hii iende wapi. Nampongeza sana Mheshimiwa Basil Mramba juu ya hilo, kwa sababu kwa kweli hili huko nyuma lilikuwa ni tatizo, tatizo kwa sababu sisi wengine tulipokuwa tunalamika kwamba mbona mikoa yetu inapata kidogo mbona mikoa mingine inapata zaidi? Tunaambiya moja ya sababu ni kwamba wahisani na wafadhili wanachagua wapi waende, wewe ukiwalazimisha waje Singida, hawataki kuja Singida wanataka kwenda Bukene. Sasa siwezi kuwalazimisha. Kwa hiyo, kwa hatua hii ambayo imefikiwa sasa naipongeza Serikali, nampongeza Mheshimiwa Basil Mramba kwamba tatizo hilo sasa halitakuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumaini yangu sasa ni kwamba miradi itakayopangwa sasa, fedha hizi ambazo zitawekwa kwenye kapu moja zitawekewa

vigezo vinavyoolewaka, vigezo vinavyokubalika ili maeneo yote na hasa Wilaya zile ambazo zilikuwa nyuma kama Singida na kadhalika na sisi tufike mahala sasa tuone kwamba tunakuwa *Alhamdulilah*. Kwa hiyo, napongeza lakini ombi langu hasa ni kwamba Serikali itengeneze vigezo vyenye kueleweka, isirudie tena yale yale mambo ya Biblia mwenye nacho anaendelea kuwa nacho na wakati mwingine ananyang'anywa yule asiyenacho kupewa yule mwenye nacho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali ilitangaza kwamba Serikali ya Italy wameamua, wamehari kununua mtama kutoka Tanzania na kwamba Serikali ya Tanzania imechagua au imeamua au imetoa, *ime-delegate* kwamba Mkoa wa Singida ndio utakaota huu mtama uende Serikali ya Italy. Nasema hii ni habari njema kwetu kwa sababu Singida tumekuwa na matatizo ya mazao ya biashara hivi karibuni tumepata zao la alizeti linatusaidia kutuletea maendeleo na kama hii tena itafanikiwa kama inavyokusudiwa basi Mkoa wetu nao utakuwa umeimarika kiuchumi na Pato la Taifa kutoka Mkoa wa Singida nao litafanikiwa.

Sasa ombi langu katika hili ni kwamba ningeomba Serikali na hasa Wizara inayohusika itujulishe kwamba lini mpango huu wa kununua au wa kuuza mtama kwenda Italy utaanza. Lakini vile vile utaratibu maalum au utaratibu husika utakaotumika ili kumwezesha mkulima aliyepo Ikungi, Isuna, Sepuka na hata Mungaa atafikisha fikisha vipi mtama huu ili uweze kufika kwenye hilo soko la Italy. Wananchi wa Singida na hasa kwenye Jimbo langu la Singida Kusini, wanasubiri kwa hamu kupata maelekezo namna ya kufanikisha jambo hili kwa sababu kwa kweli litatukomboa katika katuondolea umaskini kama vile ambavyo tumekuwa tukiomba siku zote. Lakini pia mitama iko ya aina nyingi ni vizuri tungependa kujua ni mtama wa aina gani na ukiisha julikana basi watusaidie kutupatia huo mtama ambaa unahuksika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wameshazungumzia habari ya *community* mimi ni *declare interest*. Mimi nilikuwa mfanyakazi wa *Community*, nafahamu sana mambo hayo. Niipongeze Serikali kwa kuamua kuwalipa wafanyakazi waliokuwa watumishi wa *East Africa* au wa Afrika Mashariki. Ni uamuzi mzuri wa msingi ingawa umechelewa sana, waswahili wanasema heri ya kucheleta kulikoni kukosa kufika, sasa Serikali imefika na wananchi hawa wanaelekea sasa kuwa watafika. Lakini adha na kashikashi ambazo zimewapata wananchi hawa ni kubwa mno jambo ambalo tulifika mahala kama vile kuwadhalilisha watumishi wazuri waliofanya kazi nzuri ya *Community* ya kuiletea sifa nchi yetu na Afrika Mashariki lakini malipo yake yalikuwa sasa ni udhalilishaji. Nasema hayo yameshapita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na pongezi zangu nimpongeze pia Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, katika hotuba yake ya Mei Mosi, kule Songea alieleza wazi baada ya kuliona tatizo hili, hawa wazee kila siku wako CCM pale mara wako kwa Mheshimiwa Basil Mramba, mara wanataka kwenda Ikulu kwa kweli ilikuwa ni adha sasa Mheshimiwa Rais akasema, jamani mimi nitahakikisha kabla sijaondoka nitawalipa na hatua zimeanza kuchukuliwa. Sasa pamoja na pongezi hizo na hasa heshimiwa ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa, kwa kazi nzuri aliyoifanya ili ionekane

kwamba ni kweli amedhamiria kuwasaidia hawa yako maswali ya msingi ambayo hapa yanaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ni shilingi bilioni 400 unapotoa bilioni 50 ni asilimia ngapi ya bilioni hizo 400. Hizo zingine mia tatu na kitu utazilipa lini? Haya ndiyo maswali ya kuijuliza kwa hiyo unaonekana kama vile unawahadaahadaa watu tu hivi. (*Makofi*)

Mimi ningedhani hizi bilioni 50 hazitoshi ni vizuri wenzetu hawa wakalipwa hela zaidi na ileweke kwa watu wasiojua ni kwamba Serikali ya Tanzania ilipokea pesa kutoka *Community* ya kwa *Cambridge* zaidi ya *Stealing Pound* shilingi 14,000 ukizibadilisha leo kwa hela za leo ni bilioni mia nane sasa na wao wanataka milioni 400 tu, nusu nzima hazipo kwa sababu hawa wazee ni haki yao. Zililipwa bilioni 800 na za *Cambridge* ziko wapi? Hasa kama zimetumika wapeni basi wazee hela zao hawa wasiendelee kuhangaika huku na kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba hilo lishughulikiwe. Ningeshauri utaratibu wa malipo uangaliwe vizuri ikiwezekana kila mtu alipwe katika Shirika lake alikotoka ili kuondoa mzigoo pale Hazina, orodha ya wanaostahili malipo haya iwekwe bayana mahali walipo ama ofisi Hazina. Ofisi za Mikoa, Ofisi ya DC na kadhalika na kwamba kila mstaafu apewe ajulishwe kimaandishi umepewa shilingi X, bado shilingi Y, ajulishwe apewe kimaandishi aweke mfukoni, Mungu akimchukua walau mwanae anajua kwamba baba yangu alipewa X, sasa anadai Y. Halafu mwisho tarehe maalum ijulikane lini watalipwa bakaa ambayo imebakia. Kwa kufanya hivyo nadhani tutakuwa tumefanya kazi ya kuwasaidia hawa wenzetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Wizara ya Kilimo na Chakula Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula na Naibu wake hasa rafiki yangu Profesa Pius Mbawala pale kwa kunisaidia ule mradi wa *scheme* ya Mang'onyi. Ni mradi ambao ulikwama miaka mingi, miaka nenda miaka rudi, lakini kwa kweli kwa juhudzi za Wizara ya Kilimo na Chakula sasa *scheme* ile inafanyiwa kazi, inaendelea kukarabatiwa vizuri. Niwaombe sasa basi fedha ambazo zimetoka hazitoshi, *scheme* ile bado inahitaji kushughulikiwa naomba sana sana litafutwe fungu maalum hizi fedha za kila mwaka kwa kutengeneza Bajeti ya kawaida hazitoshi. Ningeomba Wizara itafute fungu maalum la kuwezesha ili *scheme* hii ya Mang'onyi ikamilike na sisi watu wa Mang'onyi, watu wa Singida tuweze kutumia kilimo cha umwagiliaji maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo vijijini. Mikopo inatolewa mijini, *NMB* mijini, *SELF* Mjini, *Pride* Mjini, hawa wananchi wa vijijini mnawaambia MKUKUTA, MKUKUTA, huu utawapata wapi wakati hawana fursa ya kukopa? Hivi haki ya wananchi hii imekuwa ni ya wa mjini tu na watu wa kijijini hawana haki? Naomba na watu wa vijijini nao wafikiriwe kupewa mikopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza nitoe pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, ambaye tumempoteza hivi karibuni tunamwombea Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi na familia yake iwe na subira ndiyo mambo ya dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze waliowasilisha hoja ya Bajeti mwaka 2005/2006. Nimpongeze Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, nimpongeze vilevile Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kwa hotuba zao nzuri ambazo zimezidi kuleta matumaini kwa wananchi wa Tanzania, sisi tumeiona bajeti ya safari hii ni bajeti ya kisayansi, ni wachache kwa wananchi wetu wameweza kuielewa lakini sisi tutakuwa ni wawakilishi kuweza kuieleza vizuri bajeti ya mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze vile vile wagombea wetu wa nafasi za Urais katika uchaguzi huu wa mwaka 2005. Nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi, nimpongeze vile vile Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza na vile vile nimpongeze Mheshimiwa Amani Abeid Karume kuwa mgombea Urais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea lakini labda niseme kwamba nina ushauri ufuatao katika masuala ya *taxation*. Ni kweli kwamba hili Bunge limepitisha sheria katika masuala mazima ya kodi ambazo zinatakiwa wananchi walipe kodi zao kwa sababu ndio msingi imara wa kuweza kuimarisha uchumi wa nchi yetu na kuleta maendeleo, lakini nataka kusema kwamba katika Hotuba ya Waziri wa Fedha alizungumzia masuala mazima ya kuondoa kero katika *taxation* au katika kutoza kodi. Hili ni jambo la msingi kwa sababu yapo yanayojitokeza katika kukusanya kodi, kwanza tunakubali kwamba tulipitisha sheria hapa na tumeona kwamba hivi sasa zile *power* za *taxation* ambazo zimepitishwa hapa kwa mujibu wa sheria kwa kweli zile *power* ni kubwa ambazo zinatekelezwa na binadamu. Lakini nikisema mfano kwamba mkusanyaji kodi anapokwenda kwa mfanyakishara zile *power* tulizompa za *ku-search* pamoja na ile *search* ambayo anaifanya kwa mfanyakishara yule ana uwezo wa *ku-confiscate* vitabu bila sababu ya msingi lakini yanatokea kwa utashi wa baadhi ya *tax collectors* siyo wote.

Vile vile *TRA*, nikizungumzia *TRA* ni watu ambao wanafanya hii kazi inamwona kama mfanyakishara kama adui wakati ni kinyume na matarajio ya mkusanyaji kodi. Lazima amuone mfanyakishara ni mtu rafiki ili aweze kum-*convince* au aweze kumpa maelezo ya kutosheleza ili aweze kulipa kodi yake. Vile vile *TRA* isiweke *target* tu Wilayani, isipokuwa katika Wilaya wafanyakishara wetu ni wachache sana wataendelea kuwakamua wale wale kutoka Wilayani nafikiri uwekwe utaratibu wa *assessment* kama ilivyo kwa kiwango cha mkoa hii inaweza ikasaidia. Ndiyo hiyo nasema *tax collector* siyo *business friend*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfanyakishara anaweza akatumia hizi *harassment* za baadhi ya *tax collectors*, mkamtia ujanja wa kuzidi kufanya mbinu na kuweka mbinu za

kukwepa kodi. Sasa haya yote yatakuwa ni dosari katika ukusanyaji wetu wa mapato. Sheria itazame upya kanuni za kodi ili mlipa kodi alipe kodi halali, hiyo ndiyo la msingi tufike mahali mlipa kodi aji-*assess* mwenyewe na alipe kodi, awe na *confidence* ijengeke *confidence* na ikiwepo hiyo nina hakika kwamba mlipa kodi ataweba kulipa kodi zake kihalali na hatimaye kuweza kuinua kipato cha kodi katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la bajeti yetu safari hii au sera za nchi ni kwamba tukuze uchumi wetu na kupunguza umaskini, lakini yapo matatizo ambayo kwamba yamekuwa ni vikwazo katika kukuza uchumi wetu labda nizungumze mawili, matatu.

Kwanza ni suala zima la kilimo ambalo mimi nalionna limepewa bajeti ndogo na kilimo ndiyo chanzo cha kukuza uchumi wetu ukilinganisha na mambo mengine ambayo yataweza kusaidia kilimo hicho ili kukuza uchumi huu kwa upande wa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile viwanda vyetu ni vichache, uzalishaji wake ni mdogo na ubora wa bidhaa vile vile ni dhaifu na haya yanatokana na matatizo makubwa labda mawili au matatu. Lakini kubwa ninalotaka kulizungumzia kubwa zaidi linalosababisha viwanda vyetu visiendeshe kibiashara au visitoe tija nzuri kwa sababu ya tarrif ya umeme, hili ni la msingi sana. Serikali inafahamu kwamba *tarrif* ya umeme ni kikwazo katika kukuza uchumi wetu, tunashindwa kupata uwekezaji mkubwa kwa sababu moja ya sababu ya *tarrif* ya umeme. Sasa hili hebu jamani Serikali litazameni tumeshapiga kelele mara nyingi na tutaendelea kurudia suala hili kwa sababu ni la msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya nchi imezungumzia uchumi wa nchi ulivyokuwa kutoka sasa hivi tuko katika asilimia 6.7 hapa *target* yetu Mheshimiwa Waziri wa Fedha umesema tunatakiwa tufike asilimia 10 ya kukuza uchumi wetu na wewe mwenyewe umesema kukuza kufikia asilimia 10 siyo kazi ndogo na hivi tutakuza je asilimia 10 kama hatupati *investors* wakubwa wakaweza kuja kuwekeza hapa ili angalau huu uchumi uibuke haraka kabisa, masuala ya kuwekeza katika nchi yapo maeneo mengi ambayo kwamba labda watu wangeweza kuja kuwekeza, Serikali ikafuta wawekezaji wakubwa *Giant Investors* waje wawekeze.

Lakini vile vile tutazame sasa yale mambo ambayo yatawawutia wawekezaji hawa moja ni *tarrif* ya umeme, nyingine ni *skills*, watu wa kwenda kufanya kazi katika vile viwanda pia hili ni tatizo. Lingine ni kwamba suala zima la barabara ni tatizo katika kukuza uchumi wetu na hasa *feeder roads* kutoka vijijini kwenda katika barabara kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumambwa hapa na tumepeata taarifa za uhakika kwamba nchi yetu itasamehewa madeni 100%. Mimi nina uhakika haya madeni ambayo tunasamehewa ni yale madeni ya nyuma ambayo kwamba yamekaa kwa muda mrefu.

Sasa inaweza ikachukua muda mrefu kuyalipa haya madeni labda pengine Serikali itakuwa ina *save* kiasi fulani cha pesa katika kusamehewa madeni haya ambayo tulitakiwa sisi tulipe haya madeni lakini sasa hivi tutakuwa hatulipi isipokuwa pesa zile

itabidi sasa sisi wenyewe tuzielekeze katika maendeleo yetu. Sasa naamini kama pesa hizi kwa mfano niseme kama tutaweza kuwa tuna save kama bilioni 150 sasa Serikali iwe na *priority* katika hizi bilioni 150 ambazo hatukutarajia kuingia katika bajeti yetu kwa hiyo itakuwa ni *access* ya pesa ambazo ni zile ambazo tumesamehewa katika madeni basi tuzipeleke katika *priority* muhimu.

Mimi nasema *tarrif* ya umeme imepanda kwa sababu tuna madeni makubwa ya mitambo ya umeme ambayo imejengwa hapa nchini. Sasa pesa hizi hizi sasa zitumike *ku-subsidize* au kupunguza *tarrif* ya umeme angalau sasa tuweze kuwa na viwanda ambavyo vitazalisha kwa gharama nafuu na kuongeza ajira kwa wananchi na tupate bidhaa ambazo ni *quality* ambazo zinaweza zikauzika hata Kimataifa. (*Makofî*)

Sasa hili ni la msingi kwamba pesa hizi za madeni tulizosamehewa zielekezwe katika kuteremsha *tarrif* ya umeme, pesa hizi zitumike katika kujenga barabara za lami bora. Tuna barabara hapa muhimu katika nchi hii lazima zifunguliwe ambazo ni maeneo yenye utajiri mkubwa na barabara ndiyo kikwazo. Ukienda maeneo ya kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga, Rukwa barabara kule ni mbaya. Ukienda barabara ya Kigoma, ukienda maeneo ya Bukoba, kote kule kunahitaji barabara nzuri kwa ajili ya kukuza uchumi, kule kuna raslimali nyingi ambazo zitawasaidia wananchi lakini kikwazo kikubwa ni barabara ambayo itaweza kufika bandarini au ni barabara ambayo itaweza kufika katika kituo cha reli na hatimaye kuweza kusafirishwa nje ya nchi au nchi jirani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna barabara zingine zinatakiwa ziongezewe thamani kwa sababu kuongeza thamani kwa maana ya kukuza uchumi. Tuna barabara za kiutalii, sasa hivi tuna barabara inayotika Dar es Salaam kwenda Bagamoyo imeishia pale lakini sasa tunahitaji barabara ya kutoka Bagamoyo kupita Pangani hadi Tanga. Hata wewe Mheshimiwa Basil Mramba, barabara ile wewe ni mdau, wewe itakuwa ni *shortcut* kufika Rombo kuliko kuzunguka huko unakozunguka, sasa sijui wewe, mimi nakuhisni ni mdau mkubwa katika barabara hiyo, hebu tutazame, tukae, pamoja tuone tunafanya nini angalau katika pesa hizi za kusamehewa madeni tufikirie basi katika hizi. Barabara ile vile vile acha kiuchumi lakini hata kiusalamu, sasa hivi tunaona tunapopita pale Mlandizi au kwenye Daraja la Ruvu hali yake tunajia ilivyo, Mungu apishie mbali labda lile daraja limepata matatizo tumekuwa *cut off* na ukitaka kupita sasa Bagamoyo uende Pangani utapambana sasa na vivuko na madaraja mengine ambayo magari makubwa hayawezi kupita. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile ziko barabara ambazo unaweza ukaunganisha kutoka Kilimanjaro kuititia Handeni, kuititia Mtibwa na kutokea Morogoro au kutokea Gairo. Kwa hiyo, hizi zote ni barabara ambazo kwamba zitakuza uchumi wa wananchi katika yale maeneo. (*Makofî*)

Mimi nakuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango hebu mkae muone hizi pesa za kusamehewa madeni yatu tunazifanyaje katika kuzipa *priority* katika kukuza na *ku-add value* katika uchumi wetu ambao utaweza kukua kama tunavyotaka uende mpaka asilimia 10 basi mimi nafikiri tukiweka *priority* katika hilo tunaweza tukafanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hoja hizi za kuzungumza, mimi niseme kwamba naunga hoja mkono kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kuniweka wa mwisho kuchangia Wizara zote hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kama walivyoanza wenzangu kwanza kutoa rambirambi kwa ndugu yetu Mheshimiwa Abu Kiwanga na niwape pole wananchi wa Jimbo lake kwa kuondokewa na Mbunge wao, namuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina.

Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kuchaguliwa na Chama cha Mapinduzi kugombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Kikwete, tunaamini anakubalika na wananchi wote kwa hiyo, tuna uhakika na ushindi wa Chama cha Mapinduzi. Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza, naamini hawa watu wawili kwa kweli Chama cha Mapinduzi mwaka huu kitashinda kwa kura za kimbunga. (*Makofî*)

Vile vile nimpongeze Ndugu yetu Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa kugombea Urais Zanzibar na yeze tuna uhakika Zanzibar atashinda, pamoja na mbwemwe za wapinzani lakini hawaoni ndani. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri pamoja na wataalam wa Wizara zote mbili kwa maandalizi mazuri waliyoyafanya na hotuba zao kuwasilishwa na Waheshimiwa Mawaziri katika Bunge lako Tukufu. Hotuba zote mbili zote zimeeleza mafanikio na Bajeti itakavyokwenda mwaka huu, kwa hiyo, tuna uhakika zikisimamiwa vizuri Wizara hizi tutakuwa na mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali za Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi alivyofanya kazi nzuri katika miaka yake 10 ya uongozi. Ameijengea heshima nchi yetu nje na ndani. Kwa kweli tumepata mafanikio makubwa chini ya uongozi wake. Tumtakie kila la kheri kwa kuwa ndiyo anaelekea kumalizia kipindi chake Mungu ampe afya na aweze kuishi na familia yake vizuri na tunaamini atakuwa mshauri mzuri katika uongozi wa Rais ajaye. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na mimi nitoe machache katika kuchangia yale ambayo yamezungumzwa katika hotuba zote mbili.

Kwanza niipongeze Serikali kwa jinsi ilivyosimamia suala zima la mfumuko wa bei katika nchi yetu na hili ni suala ambalo linawagusa wananchi na ndiyo wanaamini kabisa sasa Serikali yao ipo kwa sababu hakuna hata siku moja imeonekana leo kibiriti kimepanda, kesho kutwa sukari imepanda, kwa kweli kumekuwa na utaratibu mzuri na kwa kweli siku hadi siku kama nilivyoeleza hotuba hizi mbili za Waheshimiwa Mawaziri kwamba bei ilikuwa inapungua. Kwa hiyo, kwa hilo ninawapongeza sana na ninaipongeza Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda niseme kwamba labda limebaki eneo ambalo vile vile linagusa wananchi, nalo ni kuhusu suala zima la mafuta ya magari, dizeli na petroli. Kupanda kwa mafuta haya bado vile vile kunakuwa ni mzigo kwa wananchi kwa sababu bei ya petroli na dizeli ikipanda maana yake kila kitu kinapanda. Mwananchi akisafiri atatozwa nauli kubwa katika mabasi, mwananchi akienda kusaga mahindi akinamama watatozwa fedha nyangi kwa sababu inatumia dizeli na vile vile inafanya baadhi ya shughuli ziweze kutokwenda vizuri. Kwa hiyo, tuiombe Serikali ifanye mkakati wowote inayoona ili kuhakikisha pamoja na kwamba bei yake si bei tunayopanga sisi wenyewe tu nchini. Lakini vile vile Serikali inao uwezo wa kutafuta mbinu mbalimbali angalau za kudhibiti hii bei ya mafuta isipande ovyo na kwa kweli wananchi wataweza kunufaika na utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nichangie upande wa mifugo. Suala zima la mifugo kama tunavyoona sasa hivi pamoja na kwamba wananchi wetu wengi ni wafugaji lakini bado hawajanufaika na ufugaji mzuri. Wananchi wetu bado wanahitaji kuelimishwa, bado wanahitaji kuongezewa au kutafutiwa utaratibu mzuri wa ufugaji kwa maana kwamba ufugaji walio nao ni ule ambao kwa kweli hauwaleti tija. Lakini Serikali kama itashughulikia suala hili kwa kutafuta ng'ombe amba ni wa maziwa na vile vile wakaelekeza juu ya ufugaji huu kwa sababu tukiwahimiza tu wapunguze mifugo haileti maana yoyote na wala hawatatuuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa la msingi ni kuwafanya wananchi wetu utaratibu ili waweze kupata mifugo bora, kidogo kidogo wenyewe wataona ni mifugo gani ambayo inawaletea faida na matokeo yake baadaye wenyewe bila hata kuhimizwa wataamua kuanza kubadilisha mifugo yao. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iweke mkakati mzuri ambao kwa kweli wananchi watanufaika nao kwa Serikali kuwaelekeza na kuwapatia mifugo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la mazingira. Sasa hivi nchi yetu karibu maeneo mengi miti imefyekwa na unaweza kukuta eneo kubwa katika nchi yetu sasa hivi limebaki wazi. Sasa sijui tunaelekea wapi maana yake itafika mahali vyanzo vya maji vyote vitakauka, hata visima vingi vitakauka kwa sababu bado wananchi wetu hawajapata elimu juu ya suala zima la mazingira. Sasa tunaiomba Serikali iweke utaratibu mzuri hasa katika kuwaelimisha kuhusu suala la upandaji miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili kwa kweli tunaomba na tunaomba sana wenzenetu wasomi, hebu sasa wabadilishe mawazo. Yale mawazo ya kutegemea tu kwamba wananchi wetu Vijijini ndio watanze misitu, wao hawaelewi, anachoelewa mwananchi ni kuingiza ng'ombe zake wale, achome moto mle ili wanyama wakali wakimbie na nyoka wasiwe karibu. Haoni kwamba kuchoma moto na kuteketeza misitu kwake bado ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba wasomi pia wabadilishe mawazo na ikiwezekana hata katika suala la kilimo, wao ndio waweze kuanzisha mashamba

makubwa, waweze kutunza mazingira na waweze hata kupanda miti katika mashamba makubwa ili iwe mfano kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasomi wakianza hivyo, tuna uhakika kwamba hali hii itajirekebisha, lakini sasa waking'ang'ania kwamba ni lazima wapate ajira, wapate ajira, wakati wenzao ndio wanaanzisha miradi baadaye wanawaajiri, kwa kweli si vizuri. Kwa hiyo, tunaomba wasomi wetu sasa wafike mahali wabadilike, waache kung'ang'ania ajira, waanzishe ajira wenyewe na waweze kuwaajiri wenzao. Wao wanategemea mwananchi wa kawaida ambaye hana kisomo alime yeye ndio ale. Sasa yeye lini atalima ili wananchi wengine wale? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba vile vile nizungumzie suala la ajira kwa vijana na hasa wale ambao wanamaliza Vyuo Vikuu. Tunaamini Serikali imeweka utaratibu mzuri wa kuajiri kufuatana na maeneo mbalimbali katika sekta mbalimbali ili waweze kufanya kazi za Serikali. Lakini vile vile kuna baadhi wengine bado wanakosa ajira, sasa tunaomba basi wasomi wetu wao pamoja na kwamba wanategemea tu kuajiriwa hawataki kuanzisha vyao kwa kutumia elimu walijonayo, lakini bado pia tunawatetea waajiriwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningezungumzia ajira hii hasa kwa upande wa Wizara ya Afya. Sasa hivi ukienda hospitalini kuna upungufu mkubwa wa Wauguzi, Wakunga, Madaktari na watumishi mbalimbali na hasa ukizingatia Wakunga ambao wanawasaidia akina mama wakati wanapojifungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, saa hizi kwa kweli unaweza kukuta hospitalini wanawake wanapata matatizo, si kwa sababu kwamba labda amepata matatizo mengine, unakuta inawezekana wanawake wapo pale wanaojifungua labda watano, sita, Wakunga wapo wawili, je, watasaidia viyi hawa akinamama na inawezekana kabisa unakuta wanapata matatizo ni kwa sababu ya upungufu wa Wakunga waliopo pale.

Kwa hiyo, ili kuwawezesha akinamama wasipate matatizo mbalimbali ya kupungukiwa damu wakati mwingine hata ya kukosa watoto na kushindwa kusimamia kujifungua kwa ajili ya upungufu wa wauguzi. Kwa hiyo, mimi naiomba sana Serikali ili angalile eneo hilo ili hawa akinamama wasipate matatizo kwa kukosa Wakunga wa kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naona ni muhimu kwa hawa Wakunga, unakuta semina mara nyingi zinafanyika. Zinapofanyika semina hizi zinakuwa kwa upande pengine wa madaktari au viongozi wao, lakini wale ambao wanashughulika na akinamama siku hadi siku, wengine toka waajiriwe hawajapewa mafunzo hata siku moja na wala hajaitwa hata kwenye semina. Sasa unakuta ndugu zetu hawa wasipokumbushwa na wakati mwingine kupewa hata maneno ya kumhamasisha, unakuta hata kauli zao zinakuwa si nzuri. Si kana kwamba kauli yake imekuwa si nzuri kwa sababu tu hawesi kufanya kazi au ni tabia yake, lakini wakati mwingine unakuta wanachoka na wakati mwingine ni kwa kuwa kila siku ye ye upo pale pale hajaitwa hata siku moja kwenye kasemina kadogo akapewa maadili upya kuhusu kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba Serikali iliangalie eneo hilo. Semina zisiwe kwa viongozi tu, ziwe hasa kwa wale ambao wanashughulika na akinamama, wanashughulika na wagonjwa siku kwa siku ili kupunguza au kuwafanya wauguzi hawa na madaktari hawa waweze kuwa na kauli nzuri, waweze kuwahudumia wagonjwa vizuri na waweze kuwasaidia kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja zote mbili mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivytangaza huyo ndiye msemaji wetu wa mwisho, si kwa leo tu bali hata katika orodha ambayo tulikuwa nayo ya wachangiaji huyu ndiye msemaji wa mwisho. Kwa hiyo, kesho, Serikali itaanza kujibu hoja zetu, halafu tutakuwa na kipindi cha kupiga kura jina kwa jina. Kwa hiyo, ni muhimu kwa Wabunge wote kesho kuwepo katika Bunge hili.

Baada ya kusema hayo, naomba niahirishe kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.36 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano  
Tarehe 15 Juni, 2005 saa tatu asubuhi)*